

REPOTI YA DUNIA YA
UFUATILIAJI WA ELIMU
KWA WOTE

2

0

1

51



Elimu Kwa Wote



ELIMU KWA WOTE

2000-2015:
MAFANIKIO NA CHANGAMOTO



United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

Muhtasari

**ELIMU KWA WOTE
2000-2015:
MAFANIKIO NA CHANGAMOTO**

Muhtasari

Ripoti hii ni chapisho linalojitegemea lililoandaliwa na UNESCO kwa niaba ya jumuiya ya kimataifa. Ni zao la juhudi za pamoja zilizohusisha wajumbe wa Timu ya Ripoti na watu wengine wengi, mawakala, taasisi na serikali.

Uteuzi uliofanyika na uwakilishi wa yaliyomo kwenye ripoti hii hauonyeshi maoni au hisia za yeyote yule kwa upande wa UNESCO kuhusiana na hali ya kisheria kuhusu nchi yoyote ile, bara, jiji au eneo, au kuhusu mamlaka zake, au kupunguzwa kwa mipaka yake.

Timu ya Ripoti hii inawajibika kutokana na uchaguzi na uwakilishi wa mambo yaliyoandikwa ndani ya kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezwa ndani yake, ambayo si lazima yawe ni yale ya UNESCO na hayaliwajibishi Shirika. Uwajibikaji wa jumla wa mawazo na maoni yaliyoelezwa ndani ya Ripoti hii ni wa Mkurugenzi wake.

Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote 2015

Mkurugenzi: Aaron Benavot

Manos Antoninis, Ashley Baldwin, Madeleine Barry, Nicole Bella, Nihan Köseleci Blanchy, Emeline Brylinski, Erin Chemery, Marcos Delprato, Joanna Härmä, Cornelia Hauke, Glen Hertelendy, Catherine Jere, Andrew Johnston, Priyadarshani Joshi, Helen Longlands, Leila Loupis, Giorgia Magni, Alasdair McWilliam, Anissa Mehtar, Claudine Mukizwa, David Post, Judith Randrianatoavina, Kate Redman, Maria Rojnov, Martina Simeti, Emily Subden, Felix Zimmermann na Asma Zubairi.

Wajumbe wa zamani

Tungependa kuwashukuru wakurugenzi na wajumbe wa zamani wa timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ambayo michango yao yenye thamani imewezesha kuwepo kwa ripoti hii tangu mwaka 2002. Shukurani kwa wakurugenzi wa zamani ambao ni Nicholas Burnett, Christopher Colclough, Pauline Rose na Kevin Watkins, na kwa wajumbe watimu ya zamani Carlos Aggio, Kwame Akyeampong, Samer Al-Samarrai, Marc Philippe Boua Liebnitz, Mariela Buonomo, Lene Buchert, Fadila Caillaud, Stuart Cameron, Vittoria Cavicchioni, Mariana Cifuentes-Montoya, Alison Clayson, Hans Cosson-Eide, Roser Cusso, Valérie Djioze, Simon Ellis, Ana Font-Giner, Jude Fransman, Catherine Ginisty, Cynthia Guttman, Anna Haas, Elizabeth Heen, Julia Heiss, Keith Hinchliffe, Diederick de Jongh, Alison Kennedy, Léna Krichewsky, François Leclercq, Elise Legault, Agneta Lind, Anaïs Loizillon, Patrick Montjourides, Karen Moore, Albert Motivans, Hilaire Mputu, Michelle J. Neuman, Delphine Nsengimana, Banday Nzomini, Steve Packer, Ulrika Peppler Barry, Michelle Phillips, Liliane Phuong, Pascale Pinceau, Paula Razquin, Isabelle Reullon, Riho Sakurai, Marisol Sanjines, Yusuf Sayed, Sophie Schlondorff, Céline Steer, Ramya Subrahmanian, Ikuko Suzuki, Jan Van Ravens, Suhad Varin, Peter Wallet na Edna Yahil.

Ripoti ya Dunia ya Elimu kwa Wote ni chapisho huru la kila mwaka. Limewezesha na kufadhiliwa na UNESCO.

Kwa taarifa zaidi kuhusu Ripoti hii, tafadhali wasiliana na:

Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote
c/o UNESCO, 7, place de Fontenoy
75352 Paris 07 SP, France
Email: efareport@unesco.org
Tel.: +33 1 45 68 07 41
www.efareport.unesco.org
efareport.wordpress.com

Makosa yoyote ya kiuchapaji au kuondolewa baadhi ya maneno vitarekebishwa kwenye toleo la kwenye tofuti
www.efareport.unesco.org

© UNESCO, 2015

Haki zote zimehifadhiwa

Toleo la Kwanza

Limechapishwa 2014 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni
7, Place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP, France

Library of Congress Cataloging in Publication Data
Data available

Ripoti zilizotangulia

2013/4 Kufundisha na kujifunza: Kufanikisha ubora kwa wote
2012 Vijana na stadi: Kufanya elimu yenye manufaa kwa kazi
2011 Mgogoro uliofichika: Vita na Elimu
2010 Kuzifikia jamii ambazo hazijafikiwa
2009 Kuushinda Ubaguzi: Umuhimu wa utawala bora
2008 Elimu kwa wote ifikapo mwaka 2015: Je, tutaweza?
2007 Misingi Imara: Malezi na elimu ya awali
2006 Kisomo (kusoma, kuandika na kuhesabu) kwa ajili ya kuishi
2005 Elimu kwa wote: Umuhimu wa ubora
2003/4 Jinsia na elimu kwa wote: Kuelekea usawa
2002 Elimu kwa wote: Je, dunia inafuata mwelekeo sahihi?

Mpango wa uchapaji umefanywa na UNESCO

Ubunifu wa vielelezo na FHI 360

Mpangilio wa Jarida na FHI 360

Picha jaladani kutoka kulia kwenda kushoto: Karel Prinsloo, Mey Meng, UNICEF/NYHQ2004-0991/Pirozzi, Nguyen Thanh Tuan, UNICEF/NYHQ2005-1176/LeMoyné, Magali Corouge, Benavot, Eva-Lotta Jansson, BRAC/Shehzad Noorani, UNICEF/NYHQ2005-1194/LeMoyné, Karel Prinsloo, Magali Corouge, Tutu Mani Chakma, Benavot, Amima Sayeed

Dibaji

Mwaka 2000, kwenye kikao cha Baraza la Dunia la Elimu kwa Wote lililokutana Dakar, nchini Senegal, serikali 164 zilikubaliana na utekelezaji wa Mwongozo wa wa Dakar, wa Utekelezaji wa Elimu kwa Wote: Kutekeleza Ahadi Zetu za Pamoja, kuzindua ajenda yetu yenye shauku ya kuyafikia malengo mapana sita ya elimu ifikapo mwaka 2015. Ndipo UNESCO ikaanzisha Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote.

Kumekuwa na maendeleo makubwa duniani kote tangu mwaka 2000-lakini bado hatujafikia malengo. Mbali na kuwepo kwa juhudi zote za serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na jumuiya za kimataifa, dunia bado haijafanikisha Elimu kwa Wote.

Kwa upande wa mafanikio, idadi ya watoto na vijana waliobalehe ambao walikuwa nje ya shule imepungua kufikia nusu tangu mwaka 2000. Inakadiriwa kuwa watoto 34 milioni walijiunga na shule baada ya maendeleo ya haraka tangu kikao cha Dakar. Mafanikio makubwa zaidi yamepatikana kwenye usawa wa kijinsia, hasa kwa elimu ya msingi, ingawa tofauti za kijinsia zimeendelea kuwepo kwenye takribani moja ya tatu ya nchi zinazotunza takwimu. Serikali pia zimeongeza juhudi za kupima matokeo ya elimu kwa viwango vya kitaifa na kimataifa, zikifanya hivi ili kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata elimu bora waliyoahidiwa.

Pamoja na hayo, kwa maendeleo yote haya, miaka 15 ya usimamizi inaonyesha matokeo yasiyoridhisha.

Bado kuna watoto 58 milioni duniani ambao hawako shuleni na watoto wapatao 100 milioni ambao hawamalizi elimu ya msingi. Ukosefu wa usawa katika elimu umeongezeka, huku maskini na wale walioko kwenye mazingira magumu ndio wanaobeba mzigo mzito zaidi. Watoto maskini zaidi duniani ndio wanaokabiliwa na uwezekano wa kutokwenda shule, mara nne zaidi ya watoto matajiri zaidi duniani, na uwezekano wa kutomaliza elimu ya msingi ni mara tano zaidi. Migogoro ndio kikwazo kigumu, kikiwa na uwiano mkubwa unaoendelea kukua miongoni mwa watoto ambao hawako shuleni wanaoishi kwenye maeneo yenye migogoro. Kwa ujumla, ubora mdogo wa elimu ya msingi bado unasababisha mamilioni ya watoto kuhitimu shule bila ujuzi wa msingi.


Zaidi ya hayo, fedha zinazotengwa kwa ajili ya elimu ni ndogo. Serikali nyingi zimeongeza matumizi, lakini ni chache tu ndizo zimeipa elimu kipaumbele kwenye bajeti zao za taifa, na zilizo nyingi zinashindwa hata kutenga asilimia 20 iliyopendekezwa ili kufidia upungufu wa fedha. Taswira hii inawiana na ile ya wafadhili, ambaobaada ya awali kuongeza bajeti za msaada, wamepunguza bajeti ya elimu tangu mwaka 2010 na hawajazipa kipaumbele nchi ambazo zina mahitaji makubwa zaidi.

Ripoti hii inajikita kwenye uzoefu huu wote, kutoa mapendekezo muhimu kwa ajili ya ajenda ya maendeleo endelevu ya ulimwengu ujao Mafunzo haya yanaeleweka. Malengo mapya ya elimu ni lazima yawe mahususi, ya kufaa na yanayopimika. Makundi ya walio pembezoni na walio kwenye mazingira magumu, yasiyofikika kirahisi na ambayo bado hayajanufaika na haki

yao ya elimu, ni lazima yapewe kipaumbele. Lazima kuwe na utekelezaji imara zaidi kwenye ufadhili. Wakati mzigo wa gharama utabebwa na serikali, jumuiya ya kimataifa lazima ihusike ili kuendeleza na kuongeza misaada kwenye elimu-hasa kwa nchi za kipato cha chini na cha kati ambazo mahitaji yao ni makubwa zaidi. A jenda itakay- ofuata itahitaji juhudi kubwa zaidi za ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi na usambazaji, ili kuendelea kushirikiana na wadau.

Kuelekea mwaka 2015, Ripoti za Dunia za Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote zimefanya kazi kubwa ya kuzisaidia nchi, kwa kutoa tathmini na uchambuzi thabiti ili kuwezesha uundaji wa sera, ikiwa ni pamoja na kuwa chombo cha utetezi kwa ajili ya serikali na asasi za kiraia. Jambo hili litaendelea kadiri tunavyotekeleza malengo mapya ya maendeleo endelevu. Baada ya 2015, Ripoti zitaendelea kupaza sauti za kuaminika na huru juu ya hali ya elimu duniani, zikitoa mapendekezo yenye tija kwa nchi zote na wabia.

Hatua kubwa imefikwa tangu mwaka 2000 lakini tunahitaji kufanya zaidi kuhakikisha elimu bora na ujifunzaji wa kila mtu maisha yake yote Hakuna uwekezaji wenye nguvu zaidi na wa kudumu kwenye haki za binadamu na utu, kwenye ujumuishi wa kijamii na masendeleo endelevu. Uzoefu wa tangu mwaka 2000 unaonyesha mambo yanay- oweza kufanyika; hivyo tunahitaji kurejea jambo hili ili kupiga hatua zaidi.



Irina Bokova
Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO

Muhtasari wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote ya Mwaka 2015

Mwaka 2000, kwenye kikao cha Baraza la Dunia la Elimu kwa Wote jijini , Dakar, Senegal, nchi 164, pamoja na wawakilishi wa makundi ya kikanda, mashirika ya kimataifa, mashirika ya wafadhili, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na asasi za kiraia , waliuridhia Mwongozo wa Utekelezaji wa ahadi za kutoa , Elimu kwa Wote. Mwongozo wa Dakar ulijumuisha malengo 6 na shabaha zake husika za kufikiwa mwaka 2015, pamoja na mikakati 12 ambayo wadau wote wangechangia.

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote imefuatilia maendeleo ya karibu kila mwaka kuelekea malengo ya ELIMU KWA WOTE na 'Malengo mawili ya Maendeleo ya Milenia yahusianayo na elimu' Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ya mwaka 2015 inatoa tathmini kamili ya maendeleo tangu mwaka 2000 kuelekea tarehe iliyolengwa kufikia malengo ya Mwongozo wa Dakar wa Utekelezaji . Ripoti inatathmini iwapo dunia ilifikia malengo ya ELIMU KWA WOTE na kama wadau walitimiza ahadi zao. Aidha, inafafanua mambo yanayoweza kuwa yamechangia hatua iliyofikiwa. . Mwisho, ripoti inabainisha mafunzo muhimu kwa ajili ya kuboresha ajenda ya dunia ya elimu baada ya mwaka 2015.

Upimaji wa maendeleo ya ELIMU KWA WOTE

Lengo la 1- Malezi na elimu ya awali

Kupanua na kuboresha huduma ya malezi na elimu ya awali, hasa kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi na magumu zaidi.

- Pamoja na kupungua kwa vifo vya watoto kwa takribani 50%, watoto milioni 6.3 chini ya miaka 5 walikufa mwaka 2013 kutokana na sababu zinazoweza kuzuilika.
- Hatua za kuboresha lishe kwa watoto zimechukuliwa. Lakini bado, mtoto mmoja kati ya wanne duniani anakua chini ya umri wake - hii ni ishara ya upungufu sugu wa virutubisho muhimu.
- Mwaka 2012, watoto milioni 184 waliandikishwa elimu ya awali duniani kote, hili ni ongezeko la takribani theluthi mbili tangu mwaka 1999.

Lengo la 2- Elimu ya Msingi kwa wote.

Kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2015 watoto wote, hasa wasichana, watoto waishio kwenye mazingira magumu, na wale wanaotoka kwenye makundi madogo ya jamii, wanapata na kumaliza elimu msingi, bure, ya lazima na iliyo bora.


- Uwiano wa uandikishwaji wa watoto kwenye shule za msingi ulikuwa asilimia 84 mwaka 1999 na unakadiriwa kufikia 93% mwaka 2015.
- Uwiano wa jumla wa uandikishwaji, ulipanda angalau kwa asilimia 20 kutoka mwaka 1999 hadi mwaka 2012 katika nchi 17, kati ya hizo ni za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.
- Wakati sehemu ya ongezeko la uwiano wa uandikishwaji lilikuwa dhahiri, takribani watoto milioni 58 hawakuwa shuleni mwaka 2012, na juhudi za kupunguza idadi hii zimekwama.

Theluthi mbili zaidi ya watoto waliandikishwa shule ya msingi mwaka 2012 kuliko ilivyokuwa mwaka 1999

Ifikapo mwaka 2015, mtoto mmoja kati ya watoto sita kutoka nchi zenye kipato cha chini na cha kati hatakuwa amemaliza elimu ya msingi

Kielelezo cha 1: Makumi ya mamilioni ya watoto bado hawatakuwa shuleni ifikapo 2015

Watoto wenye umri wa shule ya msingi walio nje ya shule, duniani na kanda zilizochaguliwa, 1990-2012 na 2015 (makadirio)



Vyanzo: Takwimu za UIS ; Bruneforth (2015).

- Pamoja na maendeleo ya upatikanaji wa elimu, suala la kutomaliza shule bado ni tatizo: katika nchi 32, nyingi za Kusini mwa jangwa la Sahara, angalau 20% ya watoto walioandikishwa hawatazamiwi kufikia ukomo wa elimu ya msingi.
- Ifikapo mwaka 2015, mtoto mmoja kati ya watoto sita wa nchi zenye kipato cha chini na cha kati- au takribani watoto milioni 100- hawatakuwa wamemaliza elimu ya msingi.

Lengo la 3- Stadi za vijana na watu wazima.

Kuhakikisha kwamba mahitaji yote ya kujifunza ya vijana wote na watu wazima yanatekelezwa kupitia upatikanaji ulio sawa wa mafunzo na programu stahiki za stadi za maisha.

- Kutafakari viwango vya mpito vilivyoboreshwa na viwango vya juu vya watoto kubaki shuleni, uwiano wa jumla wa uandikishwaji kwa elimu ya sekondari umeongezeka kutoka 71% mwaka 1999 hadi 85% mwaka 2012. Ushiriki wa elimu ya sekondari umeongezeka kwa kasi tangu mwaka 1999. Nchini Afghanistan, China, Ecuador, Mali na Morocco, uwiano ghafi wa uandikishwaji wa wanafunzi wa sekondari umeongezeka walau kwa asilimia 25.
- Ukosefu wa usawa unaendelea kuwepo kutoka shule ya msingi hadi sekondari. Kwa mfano, nchini Ufilipino, ni asilimia 69 tu ya wahitimu wa shule ya msingi kutoka familia maskini zaidi waliendelea na elimu ya sekondari ngazi ya chini, ukilinganisha na asilimia 94 kutoka kwenye familia tajiri zaidi.
- Nchi nyingi zaidi miongoni mwa nchi 94 za kipato cha chini na cha kati zenye takwimu, zimetunga sheria ya kutoa elimu bure kwa elimu ya sekondari tangu 1999. Kati ya hizi, 66 zina dhamana ya kikatiba na 28 zilipitisha hatua nyingine za kisheria. Kwa mwaka 2015 ni nchi chache tu ndizo zinatoza ada kwa shule za sekondari ngazi ya chini. Nchi hizi ni pamoja na Botswana, Guinea, Papua New Guinea, Afrika Kusini na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


Lengo la 4 - Kisomo (kusoma, kuandika na kuhesabu) cha Watu wazima

Kufikia asilimia 50 ya uboreshaji wa viwango vya kisomo cha watu wazima ifikapo mwaka 2015, hususani kwa wanawake, na upatikanaji sawa wa elimu ya msingi na ya kuwaendeleza, kwa watu wazima wote.


- Kuna watu wazima wapatao milioni 781 wasiojua kusoma na kuandika. Kiwango hiki kilipungua polepole kutoka asilimia 18 mwaka 2000 na kufikia kadiri ya asilimia 14 mwaka 2015, hii inamanisha kuwa lengo la Dakar la kupunguza nusu ya wasiojua kusoma na kuandika halikufikiwa.

Kielelezo cha2: Dunia bado iko nyuma sana kuweza kufikia malengo ya kujua kusoma na kuandika

a. Kiwango cha watu wazima kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, duniani na kanda zilizochanguliwa, 1990, 2000, 2010, na 2015 (makadirio)



b. Kiwango cha vijana kujua kusoma, kuandika na kuhesabu katika dunia na kanda zilizochanguliwa, 1990, 2000, 2010, na 2015 (makadirio)



Takwimu za kujua kusoma, kuandika na kuhesabu hazikusanyiwi kila mwaka. Takwimu za kikanda na dunia hazirejei sensa za miongo. Kielelezo hiki kinarejea takwimu za 1990 kutoka kwenye sensa ya 1985-1994; kwa 2000 kutoka sensa ya 1995-2004 na kwa 2010 kutoka takwimu za karibuni kabisa 2005-2012.

Chanzo: Takwimu za UIS.

- Ni nchi 17 tu kati ya 73 zilizokuwa na kiwango cha kutojua kusoma na kuandika chini ya 95% mwaka 2000 ndizo ziliweza kupunguza viwango vyao kwa nusu.
- Kumekuwa na maendeleo kuelekea usawa wa kijinsia katika kujua kusoma na kuandika, lakini hayatoshi. Nchi zote 43 ambako wanawake pungufu ya 90 kwa kila wanaume 100 walikuwa wanajua kusoma na kuandika mwaka 2000, zimeelekea kwenye usawa, lakini hadi mwaka 2015, hakuna hata nchi moja iliyofikia usawa.

Lengo la 5- Usawa wa kijinsia

Kuondoa tofauti za kijinsia kwenye shule za msingi na sekondari kufikia mwaka 2005, na kufikia usawa wa kijinsia ifikapo mwaka 2015, kwa lengo la kuhakikisha kuwa wasichana wanapata elimu ya msingi iliyo bora, kwa usawa na ukamilifu.

- Kwa ngazi ya shule za msingi, 69% ya nchi zenye takwimu zinatarajiwa kufikia usawa wa kijinsia katika elimu ifikapo mwaka 2015. Kasi ni ndogo zaidi kwa elimu ya sekondari, kwenye matarajio ya 48% kufikia usawa wa kijinsia mwaka 2015.
- Kumekuwa na maendeleo katika kukabiliana na tofauti za kijinsia. Kati ya mwaka 1999 na mwaka 2012, idadi ya nchi zenye wasichana pungufu ya 90 kwa kila wanaume 100 waliondikishwa shule ya msingi ilipungua kutoka 33 hadi 16.
- Miongozi mwa watoto walio nje ya shule, wasichana ndio wenye uwezekano mkubwa wa kutoandikishwa kabisa shuleni (48% ukilinganisha na 37%) wakati wavulana ndio wenye uwezekano mkubwa wa kuacha shule (26% ukilinganisha na 20%). Wasichana wakishaandikishwa ndio wenye uwezekano zaidi wa kufika madarasa ya juu.
- Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, wasichana masikini zaidi ndio wenye uwezekano mkubwa zaidi wa kushindwa kabisa kuhudhuria shule ya msingi. Mnamo mwaka 2000, nchini Guinea na Niger, zaidi ya 70% ya wasichana maskini zaidi hawakuwahi kabisa kuhudhuria shule ya msingi, ukilinganisha na pungufu ya 20% kwa wavulana matajiri zaidi.

**Takribani
theluthi mbili za
nchi zitakuwa
zilifikia ulingani
wa kijinsia
kwenye elimu
ya msingi
ifikapo 2015**

Lengo la 6 - Ubora wa elimu


Kuboresha nyanja zote za ubora wa elimu na kuhakikisha ubora wa yote ili matokeo ya kujifunza yanayotambulika na kupimika yafikiwe na wote, hasa katika kusoma na kuandika, kuhesabu na stadi za msingi za maisha.

- Uwiano wa mwanafunzi/mwalimu ulishuka kwenye 83% ya nchi 146 zenye takwimu ngazi ya elimu ya msingi. Hata hivyo chini ya 75% ya walimu wa shule za msingi ndio waliopata mafunzo kufikia viwango vya kitaifa.
- Kwa ngazi ya chini ya elimu ya sekondari, nchi 87 kati ya 105 zenye takwimu, zina uwiano wa wanafunzi/walimu ni chini ya 30:1
- Mwaka 1990, tathmini 12 za mafunzo zilifanyika kwa kuzingatia viwango vya kitaifa, lakini hadi mwaka 2013, idadi hiyo iliongezeka kufikia 101.

Watoto milioni 34 zaidi wamekwenda shule kwa mara ya kwanza, ambao wasingeweza kama si malengo ya ELIMU KWA WOTE

Kielelezo cha 3: Mkazo kwenye tathmini za kujifunza umeongezeka kwenye nchi nyingi tangu 2000

Asilimia ya nchi ambazo zimefanya angalau tathmini moja ya taifa ya kujifunza, kwa kanda, 1990–1999, 2000–2006 and 2007–2013



Chanzo: Mahesabu ya timu ya Ripoti ya Dunia ya ufuatiliaji wa ELIMU KWA WOTE (2014) kwa mujibu wa kiambatisho cha takwimu kuhusu tathmini za mafunzo za taifa

Kisanduku cha 1: Je, maendeleo yalikuwa kwa kasi zaidi baada ya mkutano wa Dakar?

Maendeleo ya uwiano wa jumla wa uandikishwaji wa wanafunzi kwenye elimu ya awali yalikuwa makubwa zaidi. Miongoni mwa nchi 90 zenye takwimu, kama uandikishwaji ungeongezeka kwa kiwango kile kile kama ilivyokuwa miaka ya 1990, wastani wa uwiano wa uandikishwaji kwenye elimu ya awali ungekuwa 40% mwaka 2015; badala yake, unatarajiwa kufikia 57%

Maendeleo kuelekea elimu ya msingi kwa wote yalikuwa duni zaidi. Miongoni mwa nchi 52 zenye takwimu za uwiano wa uandikishwaji halisi wa msingi, kama uandikishwaji ungekuwa kwa kiwango kile cha miaka ya 1990, wastani wa uwiano halisi wa msingi wa uandikishwaji ungekuwa 82% mwaka 2015; badala yake unaweza kufika hadi 91%.

Ushahidi kutoka nchi 70 kuhusu kiwango cha ustahimilivu wa kufikia darasa la mwisho la shule ya msingi kinaashiria kwamba sehemu ya ongezeko kwenye uandikishwaji ilisababishwa na maendeleo duni. Kiwango cha ustahimilivu kiliongezeka katika nchi 23 na kikapungua katika nchi 37. Kiwango cha dunia cha ustahimilivu kinakadiriwa kuwa zaidi ya 76% mwaka 2015, ambapo kwa kiwango cha miaka ya 1990, kingekuwa kimefika 80%

Inakadiriwa kwamba zaidi ya watoto milioni 34 waliozaliwa kabla ya 2010 watakuwa wameweza kwenda shule kwa mara ya kwanza ifikapo mwaka 2015, ikilinganishwa na kile ambacho kingetokea endapo mwelekeo wa zamani ungeendelea kuwepo. Pia inakadiriwa kuwa zaidi ya watoto milioni 20 waliozaliwa kabla ya mwaka 2005 watakuwa wamehitimu elimu ya msingi, tofauti na makadirio ya mwelekeo wa Dakar.

Maendeleo kuelekea usawa wa kijinsia yanaonekana kuongezeka kwenye elimu ya msingi, japokuwa usawa huo ulipaswa kuwa umefikiwa ulimwengu kote hata kabla ya mkutano wa Dakar. Dai lililotolewa kwenye Mwongozo wa Dakar kwamba lengo la kufanikisha Elimu kwa Wote ifikapo mwaka 2015 lilikuwa 'halisi na linalowezekana' linaweza kuwa limetiwa chumvi, hata kama lengo hilo lingepunguzwa na kulenga tu elimu ya msingi kwa wote. Hata hivyo, wakati lengo hilo la dunia halikuwa limefikiwa, maendeleo ya wastani yalifikiwa yakionyeshwa matumaini yakilinganishwa na rekodi ya kihistoria

Kuelezea maendeleo kuelekea mpango wa Elimu kwa Wote: Kutathmini wajibu wa vuguvugu la ELIMU KWA WOTE ngazi ya dunia.

Ahadi za dunia zilizotolewa kwenye Mwongozo wa Dakar zilitekelezwa kwa sehemu tu. Hata hivyo, baadhi ya mbinu zilizobuniwa zilifanya vizuri, zikipandisha hadhi ya hali ya elimu kutoka mwaka 2000. Huu ni mwanzo wa matumaini kwa Mwongozo wa dunia wa elimu wa baada ya 2015.

Mwongozo wa Utekelezaji wa Dakar ulipendekeza aina tatu ya uingiliaji kati wa dunia kuzisaidia nchi:

- Taratibu za uratibu, baadhi tayari zilikuwepo; nyingine ziliorodheshwa mara ya kwanza kwenye Mwongozo wa Dakar na baadaye zikaboreshwa.
- Kampeni zilizolenga maeneo maalumu ya ELIMU KWA WOTE, kama vile kisomo cha watu wazima, au kwenye changamoto maalumu kama vile mgogoro.
- Jitihada, ambazo baadhi yake ziliainishwa kwenye Mwongozo wa Dakar na nyingine zilibunwa baadaye, kutoka kwenye mamlaka yake.

Ilitumainiwa kwamba, endapo uingiliaji kati huu ungetekelezwa ipasavyo ungewezesha matokeo matano ya muda wa kati, ambayo yangesaidia kuongeza kasi ya kufanikisha malengo ya ELIMU KWA WOTE. Uingiliaji kati huo ulitarajiwa kufanya yafuatayo:

- Kusisitiza na kuendeleza ahadi za kisiasa kwa mpango wa Elimu kwa Wote.
- Kusaidia uwasilishaji na matumizi ya aina tofauti za maarifa, ushahidi na utaalumu
- Kushawishi na kuimarisha sera za kitaifa za ELIMU KWA WOTE na utekelezaji wake.
- Kukusanya ifaavyo rasilimali fedha kwa ajili ya ELIMU KWA WOTE.
- Kuanzisha ufuatiliaji na utoaji taarifa huru wa maendeleo ya malengo ya ELIMU KWA WOTE

Mwongozo wa Dakar ulipendekeza mikakati 12 ili kuwezesha matokeo haya. Je, ni kwa jinsi gani wabia wa ELIMU KWA WOTE kwa pamoja walitekeleza mikakati hii ngazi ya dunia?

Mkakati wa 1: Uwekezaji muhimu katika elimu ya msingi

Nchi za kipato cha chini na cha kati-chini zimeelekeza asilimia kubwa zaidi ya mapato yake ya taifa kwenye elimu tangu mwaka 1999, na kiuhalisia, misaada kwenye sekta ya elimu imeongezeka mara mbili zaidi. Lakini kuna ushahidi kwamba uingiliaji kati wa ELIMU KWA WOTE ngazi ya dunia – kama vile jitihada za haraka kwa ELIMU KWA WOTE, ambao baadaye uliitwa Ubia wa Kidunia kwa elimu- ulisababisha matumizi makubwa ya kitaifa kwenye elimu ya umma au misaada kwa elimu.

Mkakati wa 2: Sera za ELIMU KWA WOTE katika mifumo ya kisékta iliyo tangamanishwa vizuri na kuhusishwa na ufutwaji wa umaskini

Mwongozo wa Dakar ulifafanua kwamba mipango ya ELIMU KWA WOTE ilipaswa kuwa ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa ahadi. Ulinganisho wa pande mbili za mipango ya kitaifa kutoka nchi 30 za kipato cha chini na cha kati unaonyesha kwamba ubora uliongezeka. Mipango ambayo huonekana kuwa mizuri kwenye karatasi, hata hivyo, huweza kuwa na uhusiano mdogo na hali halisi ya michakato na mifumo ya elimu ya nchi.

Kulikuwa na mikakati 12 iliyopendekezwa kwenye mwongozo wa Dakar ili kufanikisha malengo ya ELIMU KWA WOTE

Mkakati wa 3: Uhusishwaji wa asasi za kiraia kwenye mikakati ya maendeleo ya kielimu

Kuongezeka kwa ushiriki wa asasi za kiraia imekuwa ni moja ya sifa kuu za sekta ya elimu tangu mwaka 2000. Msaada huu, hata hivyo, umekuwa na matokeo kidogo hasa katika uundaji wa mifumo shirikishi madhubuti ya kitaifa ya elimu ambayo ina uwezo wa kuleta mabadiliko muhimu.

Mkakati wa 4: Uwajibikaji katika utawala na menejimenti.

Ushirikishaji wa wenyeji na ugatuzi wa madaraka vilichukuliwa kama njia muhimu katika kuboresha utawala kwenye sekta ya elimu. Zaidi ya yote, uhamasishaji wa ushiriki wa wenyeji na kuzifanya shule ziweze kujibu mahitaji ya wanafunzi, wazazi na jamii ulibaki kuwa changamoto, hasa kwa kaya maskini zenye ufinyu wa muda wa ushiriki huo. Katika nchi maskini zaidi na zenye uwezo mdogo, ugatuzi wa madaraka na shule kujitawala vimeonekana kutokuwa na na faida kwenye ufaulu wa wanafunzi na mifumo ya elimu.

Mkakati wa 5: Kutimiza mahitaji ya mifumo ya elimu iliyoathiriwa na migogoro na kutotengemaa .

Kwa ujumla, changamoto za utoaji elimu kwenye matukio ya dharura zimepata mwamko mkubwa tangu mwaka 2000. Uvunjifu wa haki za binadamu katika sehemu zenye migogoro unaongezeka. Utetezi umesaidia kuendeleza ajenda ya elimu kwenye maeneo yenye migogoro na hali za hatari . Wabia waliotekeleza ahadi zao stahiki za Dakar wanapaswa kupongezwa kwa hili.

Mkakati wa 6: Mbinu tangamano kwa ajili ya usawa wa jinsia.

Utaratibu wa dunia ulio wazi zaidi unaohusiana na usawa wa jinsia ni Jitihada ya Umoja wa Mataifa ya Elimu kwa Wasichana [United Nations Girls' Education Initiative (UNGEI)]. Tathmini ilithibitisha mchango wake kwenye kongamano la dunia la sera na utetezi, japokuwa kikanda lilifanyika kwa asilimia ndogo. Kwenye ngazi ya kitaifa, Jitihada hiyo (UNGEI) imejiweka kwenye nafasi nzuri ya thamani kupitia ubia imara wa kitaifa. Kwa ujumla, wabia wa ELIMU KWA WOTE wameweka uangalifu wa kutosha kwenye usawa wa jinsia katika maendeleo ya lengo hili.

Mkakati wa 7: Hatua za kupambana na VVU na UKIMWI

Mwaka 2000, janga la UKIMWI lilikuwa linatishia misingi ya mifumo ya elimu kwa nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika. Mwaka 2015, wakati vita bado haijamalizika kwa ushindi, jambo baya kuliko yote limekwishazuiwa. Jitihada za elimu zilikabiliana na changamoto ya VVU zikizingatia kwa dhati udharura na kuandaa elimu pana ya uzazi Nchi nyingi ziliamua kufuata mtazamo huu mpana, ambao unawiwa na juhudi za dunia kama zao la mkutano wa Dakar.

Mkakati wa 8: Mazingira ya kielimuyenye rasilimali salama, ya kiafya, jumuisi na sawa .

Mwongozo wa Dakar ulisisitiza jinsi mazingira bora ya kujifunzia yalivyochangia kufikiwa kwa malengo yanayohusiana na usawa wa kijinsia na elimu yenye ubora. Lakini upangaji wa mikakati kwenye makundi tofauti tofauti, kutoka kwenye ufundishaji hadi kwenye ulinzi wa kijamii hadi miundombinu, ni ishara ya kukosa mwelekeo. Utekelezaji kwenye viwango vya kimataifa umechangia kidogo mno kuzisaidia nchi husika kuweka mazingira bora ya kujifunzia.

Elimu kwenye matukio ya hatari imepokelewa zaidi tangu 2000, shukrani kwa jitihada dhabiti za utetezi

Mkakati wa 9: Hadhi, hamasa na weledi wa walimu

Kikosi-kazi cha kimataifa kuhusu walimu kwa ajili ya ELIMU KWA WOTE kiliundwa mwaka 2008 ili kuratibu juhudi za kimataifa katika kujaza pengo la mwalimu. Tathmini inapendekeza kwamba kikosi-kazi hicho kilikuwa na manufaa, lakini malengo yake yanapaswa kuhusiana kwa karibu zaidi na mahitaji ya nchi husika. Kamati ya pamoja ya wataalamu ya ILO-UNESCO juu ya Ombi la Mapendekezo Kuhusu Watumishi Wanao-fundisha haijathibitika kuwa na nguvu ya kuleta badiliko. Tangu 2000, kumekuwa hakuna maendeleo kwenye ufuatiliaji wa hadhi ya walimu.

Mkakati wa 10: Utumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano

Mwongozo wa Dakar ulisisitiza nguvu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika kuwezesha ELIMU KWA WOTE. Shauku hii imekumbwa na changamoto ya maendeleo duni katika ukuzaji wa miundombinu kwenye nchi maskini zaidi, msambao wa polepole wa teknolojia na kukosekana kwa uratibu mkubwa wa dunia wa TEHAMA kuhusiana na elimu.

Mkakati wa 11: Ufuatiliaji makini wa maendeleo

Mwongozo wa Dakar ulihitaji takwimu za elimu zilizo thabiti na zenye kuaminika. Tathmini iliyofanyika ilitambua mfumo wa Taasisi ya Takwimu ya UNESCO (UIS) kama zana muhimu katika suala hili. Tangu 2000, ongezeko kubwa katika upatikanaji wa takwimu za tafiti za kaya umewezesha ufuatiliaji wa ukosefu wa usawa. Takwimu kuhusu matumizi ya fedha kwenye elimu ya umma zina upungufu, lakini kumekuwa na maendeleo muhimu kwa jinsi wafadhili wanavyoripoti matumizi ya fedha. Tathmini ya karibu zaidi ilionyesha kuwa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ilichukuliwa na wengi kuwa ni ripoti yenye ubora wa juu, kwa mujibu wa utafiti na uchambuzi thabiti. Kwa ujumla, kumekuwa na maendeleo ya wazi tangu 2000 kwa jinsi malengo ya ELIMU KWA WOTE yanavyofuatiliwa na maendeleo yanavyoripotiwa.

Mkakati wa 12: Kujenga juu ya taratibu zilizopo

Mkakati wa mwisho ulisisitiza kwamba shughuli zote zierendane na mashirika, mitandao na jitihada zilizopo. Swali la muhimu lilikuwa ni kama taratibu zilizopo zingeweza kuifanya jumuiya ya kimataifa iwajibike. Ni dhahiri kuwa taratibu za dunia za uratibu wa elimu kwa wote zisingeweza kutekeleza wajibu huo, ingawa utaratibu wa Kimataifa wa kupitia kumbukumbu za haki za binadamu ulioanzishwa 2006, ungeweza kuwa umetumika kutathmini maendeleo ya ELIMU KWA WOTE. Uwajibikaji ulikuwa ni kiungo muhimu kilichokosekana kwenye mzunguko wa ELIMU KWA WOTE na linabaki kuwa ni suala linalopaswa kushughulikiwa baada ya mwaka 2015.

Uratibu wa ELIMU KWA WOTE Duniani

Uchambuzi wa jinsi wabia wa ELIMU KWA WOTE walivyoweza kutekeleza mikakati ya Dakar kwa kiwango cha kimataifa unahitaji tathmini ya ujumla ya uratibu wa mashirika. Jinsi isivyo bahati, kadi ya ripoti, haisaidii. Kwa ujumla, utaratibu wa zamani wa uratibu wa ELIMU KWA WOTE, ulioongozwa na UNESCO, haukuhakikisha uwajibikaji wa kisiasa wa kudumu na ulikuwa na ukomo wa mafanikio kwenye ushirikishaji wa mashirikia na wadau wengine. Tathmini ijayo ya utaratibu wa uratibu wa kidunia wa ELIMU KWA WOTE unaofanywa na UNESCO International Oversight Service inatarajiwa kutoa mwanga thabiti kuhusu masuala haya.

Kuunganisha ushahidi

Je, ile mikakati 12 kutoka kwenye Mwongozo wa Dakar ilitosha kuchangia kwenye matokeo matano ya msingi ya muda wa kati yaliyotarajiwa kwenye muundo wa ELIMU KWA WOTE? Katika kutahmini ikiwa uwajibikaji wa kisiasa kwenye ELIMU KWA WOTE

Kumekuwa na mafanikio dhahiri tangu mwaka 2000 kutokana na malengo ya ELIMU KWA WOTE yanavyofuatiliwa

ulithibitishwa na kuendelezwa kipindi chote, ni dhahiri kuwa vuguvugu la ELIMU KWA WOTE lilizorota punde baada ya Malengo ya Maendeleo ya Millenia kugeuka kuwa ajenda kuu ya maendeleo. Matokeo yake yalikuwa ni msisitizo uliopitiliza kwenye elimu ya msingi kwa wote. UNESCO ilikuwa makini sana kwenye ushiriki wake wa ngazi ya juu wa kisiasa, hivyo, uchaguzi wa baraza kwa ajili ya watekelezaji wa sera za dunia kwenye elimu ulihamishwa kutoka Kundi la Mamlaka ya Juu. Dhana ya kwamba mikutano ya kidunia na ya kikanda ina nguvu ya kuweza kuziwajibisha nchi na jumuiya ya kimataifa imethibitika kuwa si kweli.

Tangu mwaka 2000, aina tofauti za maarifa, ushahidi na ubingwa zimekusanywa, kuwasilishwa na kutumika. Ushahidi mwingi mpya na sera nyingi na ari katika utafiti havikulazimika kuhusiana na shughuli za ELIMU KWA WOTE, na mara nyingi vilikuja kutoka nje ya sekta ya elimu. Wakati baadhi ya ushahidi mpya ulifika kwenye mikutano ya uratibu ya ELIMU KWA WOTE, haikuonekana kutumika kwenye utayarishaji wa sera.

Tangu mwaka 2000, hapajatokea upungufu wa mipango ya kitaifa ya elimu. Hata hivyo, si dhahiri kwamba maarifa au zana mpya vimekuwa vikitumika kukuza uwezo katika kuandaa sera ya taifainayozingatia ushahidi uliopo au kwamba wameimarisha sera ya taifa ya ELIMU KWA WOTE na utekelezaji wake.

Tokeo tarajiwa la msingi la mchakato wa Dakar lilikuwa ni kwamba mipango yenye kuaminika ingesaidia uhamasishaji wenye tija wa rasilimali fedha kwa ajili ya ELIMU KWA WOTE. Ongezeko la matumizi ya ndani kwenye elimu katika nchi zenye kipato cha chini lilikuwa la kuridhisha, lakini chanzo chake kikuu kilikuwa ni ongezeko kwenye uhamasishaji wa rasilimali za ndani kuliko kuipa elimu umuhimu wa kwanza. Msaada wa kimataifa uliongezeka mno, lakini bado kiwango chake hakikutosheleza mahitaji.

Uamzi wa kuanzisha utaratibu unaojitegemea wa kusimamia na kuripoti maendeleo ya malengo ya ELIMU KWA WOTE unaweza kuwa wa hatari katika kuendeleza msukumo na wajibu wa ELIMU KWA WOTE. Lakini uboreshaji wa utaratibu wa kuripoti ulikuwa ndio shukrani ya pekee kwa uboreshaji mkubwa wa takwimu na uchambuzi, mara nyingi ulifadhiliwa na wabia wa ELIMU KWA WOTE.

Vuguvugu la
ELIMU
KWA WOTE
liliathirika pale
ambapo Malengo
ya Maendeleo ya
Millenia
yalipofanywa
kuwa ajenda
kubwa ya
maendeleo



Credit: Eva-Lotta Jansson

Hitimisho

Juhudi za kuanzia mwaka 2000 katika kuendeleza elimu duniani kote zimekuwa karibu zinafanana na uhakikishaji kuwa kila mtoto angekuwa shuleni. Kusudi la ELIMU KWA WOTE (na Malengo ya Maendeleo ya Millenia) la fursa ya elimu ya msingi kwa wote hasa ulifaa kwa nchi maskini zaidi, lakini nchi nyingine hazikuhusika sana. Kwa wakati huu, msisitizo kwenye uandikishaji wa elimu ya msingi kwa wote haukuzingatia sana kwenye maeneo mengine muhimu, kama vile ubora wa elimu, malezi na elimu ya awali, na kisomo cha watu wazima.

Kwa ujumla, hata lengo la elimu ya msingi kwa wote halikufikiwa, licha ya malengo mengi zaidi ya ELIMU KWA WOTE, na wale walioko kwenye hali ngumu walibaki kuwa wa mwisho kunufaika. Lakini kumekuwa na maendeleo ambayo hayafai kubezwa. Dunia itakuwa imeendelea ifikapo 2015 zaidi ya pale ambapo ingekuwa imefika kama ile mielekeo ya miaka ya 1990 ingeendelea kuwepo. Aidha ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu tangu Dakar umeimarika na kupanuka.

Mwishoni, vuguvugu la ELIMU KWA WOTE linaweza kuainishwa kama ni mafanikio yenye sifa zinazostahili, hata kama wabia wa ELIMU KWA WOTE wanaweza wasiwe wametekeleza ahadi zao. Lakini somo ambalo limejitokeza kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita ni kwamba, wakati suluhisho za kiufundi ni za muhimu, ushawishi na nguvu za kisiasa ni zaidi, na ni vya muhimu zaidi katika kubaini kipimo cha marekebisho na matendo kinachohitajika kufanikisha ELIMU KWA WOTE katika ngazi ya kitaifa. Majadiliano juu ya agenda za baada ya 2015 yanaweza kutoa fursa kufanikisha kiwango kinachohitajika.

Ajenda ya
baada ya
2015 inatoa
fursa ya kufikia
kiwango
kukubwa zaidi
cha mageuzi
na hatua za
kuchukua
katika ngazi ya
kitaifa

KADI YA RIPOTI 2000-2015

LENGO LA 1 Malezi na elimu ya awali

Kupanua na kuboresha malezi na elimu ya awali ya kina, hasa kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi zaidi na wale wasiojiweza

<p><i>Alama za kimataifa *</i></p> <p>* kati ya nchi 148 zenye takwimu</p>	<p>mbali sana na lengo</p> <p>20%</p>	<p>mbali na lengo</p> <p>25%</p>	<p>karibu na lengo</p> <p>8%</p>	<p>waliofikia lengo</p> <p>47%</p>
<p><i>Mafanikio</i></p> <p>✓✓</p>	<p>Vifo vya watoto</p> <p>↓ 139%</p> <p>2000</p> <p>2015</p>	<p>Uandikishwaji elimu ya awali</p> <p>184 milioni</p> <p>watoto waliaandikishwa (2012)</p>	<p>Elimu ya awali ya lazima</p> <p>kwenye nchi 40 kufikia mwaka 2014</p>	<p>% wanaokwenda shule ya awali *</p> <p>*takwimu za 2012</p>
<p><i>Jitihada zilizo-fanyika</i></p> <p>✓</p>	<p>Mabadiliko ya uelewa wa mahitaji ya utotoni ya awali</p> <p>Vitabu + Mchangamsho ufahamu + Uwepo wa wazazi</p> <p>Mifumo ya elimu yenye kuzingatia hisia za kitamaduni + Vidude vya kujifunzia</p> <p>Cheza + Nafasi salama</p>	<p>Njia tofauti katika kuongeza upatikanaji</p> <p>Kufuta ada za shule (Ghana)</p> <p>Uhamishaji wa pesa (China)</p> <p>Shule za chekechea zitembeazo (Mongolia)</p> <p>Kufanya elimu iwe ya lazima (Mexico na Myanmar)</p>	<p>Kuongezeka kwa mahitaji</p> <p>KAMPENI ZA KUHAMASISHA JAMII</p> <p>(Ghana na Thailand)</p>	
<p><i>Cnhangamoto zilizoopo bado</i></p> <p>X</p>	<p>Vifo vya watoto</p> <p>watoto 6.3 milioni walikufa kabla ya kufikisha miaka 5 kwa mwaka 2013</p>	<p>Uandikishwa kwenye elimu ya awali kwenye moja ya tano ya nchi, pungufu ya 30% ya watoto watakuwa wameandikishwa ifikapo 2015</p>	<p>Ubora wa chini</p> <p>Walimu na walezi waliofunzwa zaidi wanahitajika</p>	
<p><i>Mafanikio yanayotofautiana</i></p>	<p>Vifo vya watoto</p> <p>Mtoto anayeishi Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara ana uwezekano x 15 zaidi wa kufa kabla ya kufikisha miaka 5 kuliko mtoto wa nchi zilizoendelea</p>	<p>Mahali</p> <p>Watoto waishio maeneo ya vijijini wana uwezekano x2 zaidi wa kutokwenda shule kama wenzao wa mijini kuliko ilivyokuwa mwaka 2000 (Togo, Chad na Lao PD)</p>	<p>Utajiri</p> <p>Pengo kati ya watoto matajiri na maskini walioko mashuleni ni kubwa mara 2 zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 2000 (Niger, Togo, Jamhuri ya Afrika ya Kati Bosnia/Herzegovina na Mongolia)</p>	<p>Shule za bibafsi za awali lddadi ya watoto walioandikishwa kwenye shule za binafsi za awali imeongezeka tangu 1999</p>
<p><i>Mapendekezo kwa ajili ya kipindi kufuatia mwaka 2015</i></p>	<ol style="list-style-type: none"> 1. Elimu ya awali lazima ipanuliwe kwa watoto wote, hasa wale wa pembezoni zaidi 2. Takwimu bora zaidi kuhusu aina zote za <u>Umakini zaidi unahitajika malezi ya awali ya utotoni zinahitajika</u> 3. Watoto wote wanahitaji angalau elimu ya awali ya lazima ya mwaka mmoja 			

LENGO 1

Malezi na elimu ya awali

Kupanua na kuboresha malezi na elimu ya awali, hususan kwa watoto walioko kwenye mazingira hatarishi na wenye hali ngumu

Kusaidia maendeleo ya watoto katika hatua za mwanzo kabisa za maisha kuna mchango mkubwa mno kwenye matokeo bora ya kielimu na kijamii. Mirejesho ya juu zaidi ya kiuchumi ya uwekezaji kwenye elimu iko katika hatua za awali kabisa za utoto. Jamii zisizo na uwezo, hususan kwenye nchi maskini zaidi, hunufaika zaidi, jambo ambalo ni ushahidi wa zaida katika uwekezaji mkubwa kwenye hatua hii.

Tangu 2000, maendeleo yamefikwa kwenye idadi ya watoto duniani kote, walioandikishwa kwenye programu za malezi na elimu ya awali. Bado watoto kutoka makundi yaliyosahauliwa wananyimwa fursa kutokana na ukosefu wa fedha, miundo isiyo sawa na kukosa umakini kwenye masuala ya ubora.

Kuna maendeleo kiasi cha kiwango cha kudumisha uhai na lishe, lakini malezi bado ni duni.

Lishe duni inaweza kusababisha ucheleweshwaji kwenye makuzi ghafi wa mwili wa mtoto. Lakini lishe bora haitoshi. Ushirikiano miongoni mwa huduma za afya, elimu na ulinzi wa jamii unahitajika ili kupambana na visababishi hatarishi vinavyochangiwa na kuenea kwa umaskini.

Vifo vya watoto vimepungua

Kati ya 1990 na 2013 kiwango cha vifo vya watoto kilishuka kutoka 90 hadi vifo 46 kwa kila watoto hai 1000. Hata hivyo, punguzo hili la takribani 50% kwenye vifo vya watoto halitoshi kufikia lengo la Malengo ya Maendeleo ya Milenia, lililowekwa mwaka 2000, la punguzo la theluthi mbili kutoka viwango vya miaka ya 1990. Watoto - 6.3 milioni miongoni mwao katika mwaka 2013-wanaendelea kufa kabla ya kufika umri wa miaka 5, wengi wao vifo vyao vingezuilika. Watoto wako kwenye hatari kubwa zaidi kama wanazaliwa kwenye umaskini, maeneo ya vijijini na/au na mama mwenye elimu ya chini. Katika kushughulikia suala la vifo vya watoto, utashi wa kisiasa na upatikanaji wa fedha ni mambo muhimu sana.

Lishe ya watoto imeboreshwa-lakini bado haitoshi

Nchi nyingi zaidi zimepiga hatua katika kupunguza idadi ya watoto wenye matatizo ya kudumaa tangu miaka ya 1990. Nchi nyingi za kusini mwa jangwa la Sahara zimepiga hatua tangu mwaka 2000, lakini kanda hii kwa mbali bado ina sehemu kubwa ya watoto wenye utapiamlo, wakikadiriwa kufika 45% ya dunia ifikapo 2020.

Likizo ya uzazi na huduma nzuri za malezi vinaweza kusaidia makuzi ya watoto

Watoto wanapaswa kusaidiwa ili wastawi, na si waendeleo kuishi tu. Kwenye nchi nyingi zenye kipato cha kati na cha juu, likizo ya uzazi yenye malipo wakati wa miezi ya awali ya maisha ya mtoto ni muhimu sana kwa afya na ustawi wa mama na mtoto. Inagawa karibu nchi zote kisheria hutoa likizo hiyo, ni 28% tu ya wanawake walioajiriwa duniani kote wanaweza kulipwa mafao ya likizo ya uzazi. Uhusishwaji wa wazazi wa kiume pia ni muhimu kwa maendeleo ya mtoto. Hadi 2013, likizo ya uzazi kwa baba ilikuwa imetolewa kwenye nchi 78 kati ya nchi 167 zenye takwimu, na likizo yenye malipo kwenye nchi 70. Lakini wanaume wanaweza wasiwe tayari kuchukua likizo hiyo kwani viwango vya malipo huwa ni chini zaidi.

Wazazi wanaweza kuboresha makuzi tambuzi na makuzi hisia za kijamii kwa watoto wao kupitia programu za ndani na nje ya nyumba wanamoishi, kwenye makundi au peke yao. Programu za kutembelea nyumbani hutoa usaidizi wa ana kwa ana na zinaweza kuwa na manufaa mapana zaidi.

Nchi nyingi zinafuata mwelekeo wa kuwa na sekta mchanganyiko kwenye huduma za awali za watoto

Katika kuhamasisha nchi ziongeze na kuboresha malezi na elimu ya awali hususan kwa maskini na wale wa pembezoni, Mwongozo wa Dakar ulipendekeza sera za kitaifa na kissekta ziwezeshe kwa

Kuweka misingi sawa kuna faida kubwa za baadaye

rasilimali za kutosha. Kwa mwaka 2014, nchi 78 zimekuwa zikitekeleza sera za sekta nyingi na 23 zilikuwa zinaandaa sera hizo. Viambato vinavyochangia mafanikio ya sera za sekta nyingi ni pamoja na ushirikiano, vipimo vilivyokubalika vya maendeleo miongoni mwa wizara na mashirika na wafanyakazi.

Mifumo ya elimu ya awali na viwango vya uandikishaji vimepanda ghafla kwenye baadhi ya nchi.

Kuongezeka kwa fursa kwenye elimu ya awali, iwe ni kupitia programu rasmi au zisizo rasmi, ni muhimu katika kuboresha fursa za maisha ya mtoto, kuongeza ufanisi wa mfumo wa elimu na rasilimali, na kupunguza ukosefu wa usawa kwenye jamii kwa ujumla.

Uandikishaji umepanda kwa takribani theluthi mbili kwa kipindi zaidi kidogo ya muongo mmoja, lakini ubora bado ni duni.

Kati ya 1999 na 2012, uandikishaji kwenye elimu ya awali umeongezeka kwa 64% (kufikia 184 milioni) kwa hali ya kutofautiana kabisa kijinsia. Baadhi ya nchi zimepanua kwa kiasi kikubwa mifumo yao ya elimu ya awali ya umma, ikiwa ni pamoja na Kazakhstan na Vietnam. Hata hivyo, maendeleo hayo yamekuwa sio sawa, yakitofautiana kabisa kijinsia kati ya maeneo ya mijini na yale ya vijijini, na jamii na mikoa ndani ya nchi husika. Tofauti ya kipato imechangia sana mahudhurio kwenye nchi kama Jamhuri ya Kidemorasia ya Watu wa Lao, Tunisia na Mongolia. Njia za kuchochea zaidi ongezeko kwenye uandikishwaji ni pamoja na:

- Sheria zinazoongoza ushiriki. Hadi mwaka 2014, nchi 40 zilanzisha elimu ya lazima ya awali
- Sera zinazohusisha elimu ya awali kwenye mzunguko wa elimu ya msingi. Nchi nyingi zina sera hizi lakini hakuna usaidizi wa kifedha kwenye utekelezaji wake
- Ufutaji wa ada kwa elimu ya awali. Nchi nyingi zilizofanya hivyo zimepata ushiriki mkubwa, ingawa baadhi ya serikali zimehangaika kutafuta rasilimali zinazohitajika.
- Motisha ya kifedha kwa uandikishaji. Kwenye vijiji vya China, watoto kutoka familia zenye msamaha wa ada ya masomo na zinazopewa pesa, kwa sharti la kuhudhuria shule, uwezekano wao wa kuhudhuria shule ya awali ulikuwa 20% zaidi.
- Kuwafanya wazazi na watoto wavutiwe zaidi na usomaji wa elimu ya awali. Nchini Thailand, utoaji mpana pamoja na kampeni za kuhamasisha umma vimeongeza mahudhurio ya elimu ya awali kwa takribani 93% ya watoto wenye umri wa miaka 4 hadi 5.


Uhusishwaji wa Sekta binafsi bado uko juu

Kati ya 1999 na 2012, asilimia za uandikishwaji wa elimu ya awali kwenye shule binafsi ulipanda kutoka 28% hadi 31%, kwa nchi 100 zinazotunza takwimu. Kupanda kwa uandikishwaji kwenye sekta binafsi kumesababisha matatizo mawili. Pale ambapo upatikanaji wa malezi na elimu ya awali hutegemea ada inayolipwa, maskini wengi zaidi waliachwa nyuma. Na wagavi/ wawekezaji binafsi hawapendelei kuwekeza kwenye maeneo yenye idadi ndogo ya watu na yale yaliyotengwa/jitenga. Pamoja na hayo, kwenye nchi zenye kipato cha chini na kati, shule nyingi binafsi zenye gharama za chini huendeshwa kwenye hali duni na pasipo usajili wa

Hadi 2014, nchi 40 zilikuwa zimeanzisha elimu ya awali ya lazima

Kielelezo cha 4: Viwango vya uandikishwaji kwenye shule za awali unakadiriwa kuwa umeongezeka kwa robo tatu wakati wa kipindi cha Mwongozo wa Dakar

Uwiano wa jumla wa uandikishwaji wa elimu ya awali, ulimwengu na kanda, 1990–2012 and 2015 (makadirio)




Vyanzo: Takwimu za UIS ; Bruneforth (2015).

serikali. Hata kwenye nchi zenye kipato cha juu, kama vile Uingereza, watoto wengi maskini hufelishwa na shule za awali zisizo na ubora, zenye gharama nafuu zilizokusanyika/ jazana kwenye maeneo duni.

Safari ya ubora haijashughulikiwa kwa usahihi

Watoto ambao hawapati elimu bora ya awali wana uwezekano mdogo wa kufaulu kwenye shule ya msingi na zaidi. Wakati ambapo hata elimu duni huleta manufaa kiasi, kadiri ubora unavyozidi, ndivyo manufaa nayo huongezeka.

Kuandaa walimu wa elimu ya awali ni ufunguo wa kuongeza ubora, lakini bado walimu wasiofunzwa ndio mara nyingi huajiriwa, na hadhi duni na kipato kidogo husababisha kupatikana kwa idadi kubwa ya watu, na hivyo kuathiri matokeo ya elimu. Sekta binafsi hulipa walimu fedha kidogo kadiri inavyowezekana ili kupunguza matumizi. Nchi kama Kenya, Singapore na Columbia zimebainisha kwa uwazi mahitaji ya mafunzo kwa walimu wa elimu ya awali, lakini wengi wao bado hawajafikia hata vile viwango vya chini kabisa vilivyowekwa.



Credit: Olivier Culmann/Tendance Floue

KADI YA RIPOTI 2000-2015

LENGO LA 2 Elimu ya msingi kwa wote

Hakikisha kwamba ifikapo 2015 watoto wote, hususan wasichana, watoto walioko kwenye mazingira magumu na wale wanaotoka makundi madogo wanapata elimu ya lazima bure, iliyo kamili na yenye ubora

<p><i>Alama za kimataifa*</i></p> <p><small>*kati ya nchi 140 zenye takwimu</small></p>	<p>mbali sana na lengo 9%</p> <p>mbali na lengo 29%</p> <p>karibu na lengo 10%</p> <p>waliofikia lengo 52%</p>
<p><i>Mafanikio</i> ✓✓</p>	<p>Watoto wa shule ya msingi walioandikishwa</p> <p>1999 84% Sasa 91% = 48 milioni zaidi</p> <p>Kumaliza shule ya msingi</p> <p>Ongezeko la kumaliza shule ya msingi kwa pointi zaidi ya 20%</p> <p>Mali, Guinea, Sierra Leone, Benin, Ethiopia, Mozambique</p>
<p><i>Jitihada zilizofanyika</i> ✓</p>	<p>Kufuta ada za shule</p> <p>Hifadhi za jamii (k.m. utoaji wa pesa watoto wasiojiweza)</p> <p>Shule, maji, umeme na miundombinu ya afya</p>
<p><i>Cnhangamoto zilizopo bado</i> X</p>	<p>Walio nje ya shule</p> <p>Wasiomaliza shule 34 milioni huacha shule mapema kila mwaka</p> <p>Vikwazo 36% ya watoto walio nje ya shule hutoka maeneo yalioathiriwa na migogoro</p> <p>Elimu ya kiwango cha chini</p> <p>Elimu ya bure haijawafikia wote</p> <p>Watoto 58 milioni bado wako hawako shuleni Katio yao, 25 milioni hawatakwenda kabisa shule</p> <p>64% Asia ya Kusini/ Magharibi 58% Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara</p> <p>1999 2011</p>
<p><i>Mafanikio yanayotofautiana</i></p>	<p>Watoto walio nje ya shule Kikanda</p> <p>Vijijini/ mijini Nchi za kipato cha chini na kati</p> <p>Makundi ya pembezoni yameachwa nyuma</p> <p>Watoto maskini zaidi ni vigumu zaidi kumaliza shule ni pungufu x5 zaidi kuliko tajiri zaidi kwa mwaka 2010</p> <p>maeneo mengine ya dunia</p> <p>Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara</p> <p>Asia Kusini na Mashariki</p> <p>2000 3X wanaweza wasiende shuleni kabisa</p> <p>2008 4X wanaweza wasiende shuleni kabisa</p> <p>migogoro, kazi, walemavu, makundi madogo, UKIMWI, wasichana wa vijijini</p>
<p><i>Mapendekezo kwa ajili ya kipindi kufuatia mwaka 2015</i></p>	<p>1. Ubaguzi lazima ushughulikiwe ikiwa tunataka kufikia lengo la elimu ya msingi kwa wote</p> <p>2. Zipatikane takwimu bora zaidi ili kufuatilia maendeleo ya wale wasiojiweza <i>nafasi ya kuboresha</i></p>

LENGO 2

Elimu ya msingi kwa wote

Kuhakikisha kwamba ifikapo 2015 watoto wote, hususan wasichana, watoto walio kwenye mazingira magumu na wale wa jamii za makundi madogo, wanapata kuanza na kumaliza, elimu bora ya msingi ya lazima itolewayo bure.

Elimu ya msingi kwa wote ilikuwa ndio lengo kuu zaidi la ELIMU KWA WOTE, pale ilipopindishwa na mwingiliano wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Nchi ambazo haziwafikii wale wa pembezoni haziwezi kulifikia lengo la elimu kwa wote. Uboreshaji unahitajika ili kuwafikia watu maskini zaidi, makundi madogo, wasichana wa vijijini, watoto walioko kwenye ajira, jamii za wahamamaji, watoto walioathiriwa na VVU na UKIMWI, wanaoishi kwenye makazi holela, watoto wenye ulemavu na wale wanaoishi kwenye maeneo changamani ya dharura.

Kufuatilia maendeleo

Mnamo mwaka 2012, takribani watoto 58 milioni wenye umri wa shule ya msingi hawakuwa wameandikishwa shuleni. Sababu zilizochangia ni pamoja na mwingiliano wa watu na mazingira, hali za migongano, kutengwa kwa makundi kadhaa ya kijamii na kiuchumi, na kukosekana kwa uwajibikaji sahihi kwenye baadhi ya nchi zenye idadi kubwa ya watoto walio nje ya shule.


Pamoja na changamoto hizi, nchi kama Burundi, Ethiopia, Morocco, Msumbiji, Nepal na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimefikia maendeleo makubwa, japokuwa hayana usawa, katika kupunguza ukosefu wa usawa wa kijinsia na kipato kwenye fursa za elimu ya msingi, na kuongeza uwiano halisi wa uandikishwaji na ufanikishaji.

Uwiano halisi wa uandikishwaji uliongezeka kwa uthabiti

Miongoni mwa nchi 116 zenye takwimu, nchi 17 ziliongeza uwiano halisi wa uandikishwaji kwa zaidi ya 20% kati ya 1999 na 2012. Bhutan, Jamhuri ya Kidemorasiasia ya Watu wa Lao na Nepal zimekuwa ni mfano wa mafanikio ya kung'ara kwenye uwiano halisi wa uandikishwaji barani Asia. Nchi za Amerika ya Kusini, El Salvador, Guatemala na Nicaragua zimeongeza uwiano halisi wa uandikishwaji kwa zaidi ya 10%. Kusini mwa Jangwa la Sahara, Burundi, uwiano halisi wa uandikishwaji uliongezeka kutoka pungufu ya 41% mwaka 2000 hadi 94% katika mwaka 2010.

Lengo la 2 lilijulikana zaidi lakini bado halitakuwa limefikwa ifikapo 2015

Kielelezo 5: Viwango vya uandikishwaji halisi wa msingi vilikua kwa kasi mwanzoni mwa miaka ya 2000 lakini vikapungua baada ya 2007
Uwiano uliorekebisha wa uandikishwaji halisi wa msingi, duniani na kanda, 1990–2012 and 2015 (makadirio)



Vyanzo: Takwimu za UIS; Bruneforth (2015).

Kumaliza shule ya msingi kuliongezeka kwenye nchi nyingi

Watoto wachache zaidi hawakuwahi kwenda shule

Asilimia ya watoto ambao hawakuwahi kabisa kwenda shule ilipungua kwenye nchi nyingi. Miongoni mwa nchi ambako angalau 20% ya watoto hawakwenda shule katika mwaka 2000, 10 kati yao zilipunguza asilimia hiyo kwa zaidi ya nusu ilipofika 2010. Asilimia ya watoto ambao hawakuwahi kabisa kwenda shule ilipungua kwa kiwango cha ajabu nchini Ethiopia (kutoka 67% mwaka 2000 hadi 28% mwaka 2011) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kutoka 47% mwaka 1999 hadi 12% mwaka 2010).

Idadi kubwa ya watoto wasiokwenda shule bado iko kwenye baadhi ya nchi

Nchi zenye watu wengi bado ziliendelea kuwa na idadi kubwa ya watoto wasiokwenda shuleni kwenye mwaka 2012. India iliongeza uwiano wake halisi wa uandikishwaji kutoka 86% hadi 99%, lakini Nigeria na Pakistan walipata maendeleo kidogo sana kuliko ilivyotarajiwa, hii ilichangiwa na vita vya kimakabila na kidini, demokrasia duni na uongozi wa kisiasa uliojaa rushwa.



Nchi nyingi bado zina safari ndefu kwenye ukamilishaji wa elimu ya msingi, hasa kwa watu maskini zaidi

Kuhitimu elimu ya msingi kuliongezeka kwa kiwango kikubwa kwenye baadhi ya nchi. Nchi nane ziliongeza viwango vya kumaliza elimu ya msingi kwa zaidi ya 20%: Benin, Cambodia, Ethiopia, Guinea, Mali, Msumbiji, Nepal na Sierra Leone. Lakini maendeleo hayo bado hayatoshi kabisa, ikiwa ni ishara ya elimu kuwa na matatizo ya kutomudu gharama, upungufu wa ubora na kutowiana na mahitaji kimaisha.

Maendeleo hutofautiana miongoni mwa nchi

Kukatiza masomo ni tatizo kubwa kwenye nchi za kipato cha chini, hususan miongoni mwa watoto waliochelewa kuingia shule na wale wanaotoka familia maskini. Miongoni mwa nchi 139 zilizo na takwimu za kutosha, kwenye nchi 54 – zaidi Asia ya Kati, Ulaya ya Kati na Mashariki, na Ulaya Magharibi – karibu watoto wote walioandikishwa elimu ya msingi walikuwa na uwezekano mkubwa wa kufika darasa la mwisho kwa mwaka 2015. Lakini kwenye nchi 32, zaidi Kusini mwa Jangwa la Sahara, angalau 20% ya watoto wana uwezekano wa kukatiza masomo.

Mendeleo makubwa yalipatikana kwenye maeneo ambayo ada ilifutwa

Kimsingi, elimu sasa ni bure kwenye nchi nyingi. Kwenye nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, nchi 15 zimepitisha sheria ya kufuta ada za shule tangu mwaka 2000. Katika kuthibitisha vikwazo vinavyohusiana na gharama, uondoshwaji wa ada umeleta matokeo chanya kuhusiana na uandikishwaji baada ya kuanza kutekelezwa. Maendeleo hayo, kwa sehemu yalitokana na ongezeko la kifedha kwa ajili ya elimu. Uondoshwaji wa ada pia ulihamasishwa na siasa za ndani: ilikuwa ni ajenda maarufu ya uchaguzi kwenye nchi zenye kipato cha chini katika nchi za Afrika.

Ongezeko la ghafla kwenye uandikishwaji kufuatia uondoshwaji wa ada linaweza kuvutia mfumo wa elimu ya msingi, kama miaka ya 1990 ilivyoonyesha. Na matokeo yake, tangu hapo nchi nyingi zimekuwa zikitumia mwelekeo wa mfuatano. Hata hivyo, fedha za ruzuku maalumu zilizotolewa kupitia uondoshwaji wa ada ili kupanua mifumo ya elimu hazikuwa zinatoshwa, zililetwa kwa utaratibu duni na malengo yake hayakuwa bayana.

Baadhi ya mielekeo ilifanikiwa kwa kuongeza uhitaji

Ni mara chache elimu kuwa ya bure, ingawa sheria na sera zinaahidi uondoshwaji wa ada, ziko gharama nyingine nyingi kwenye familia. Utaratibu wa

kuongeza uhitaji wa elimu ya msingi kwenye familia hupunguza mizigo mingine ya kifedha kama usafiri, chakula cha mchana shuleni na sare za shule. Programu za kinga ya kijamii huhusisha vipimo vya uhitaji ili kuboresha elimu, kama vile utoaji wa pesa, programu za kulisha wanafunzi shuleni, ufadhili wa masomo, posho na misaada ya masomo.

Proramu za kulisha wanafunzi shuleni

Jitihada za chakula kwenye elimu zimewafikia watoto 368 milioni kwenye nchi 169. Si tu kwamba programu hizi husaidia kuhakikisha kwamba watoto wanaohudhuria shuleni wanakuwa na afya, bali pia washiriki huwa na uandikishwaji na mahudhurio bora zaidi kuliko wasio washiriki.

Programu za utoaji wa fedha

Utoaji wa fedha kwa kaya zisizo salama, ulioanzishwa huko Amerika ya Kusini, umeenea kwenye nchi za kipato cha chini na kati za Asia na Kusini mwa jangwa la Sahara. Programu nyingi za utoaji wa fedha zimeongeza uandikishwaji na mahudhurio, na zimepunguza idadi ya watoto wanaoacha shule. Hata hivyo, utoaji wa fedha si mara zote huboresha matokeo ya elimu kwa makundi yaliyoko kwenye mazingira hatari. Kuna mjadala kama utoaji huo wa fedha uwe wa masharti ama la. Programu hizo zinaweza kuungwa mkono kisiasa kwa urahisi ikiwa zitatolewa tu kwa wale wanaohudhuria shule. Utoaji wa fedha ambao unategemea mahudhurio ya mtoto una matokeo makubwa zaidi kwenye elimu kuliko utoaji wa fedha usio na masharti.

Usaidizi kwenye ugavi umesaidia kuongeza upatikanaji wa elimu ya msingi

Miradi ya miundombinu kama vile ujenzi wa shule na barabara imeleta matokeo thabiti kwenye upatikanaji wa elimu. Kumekuwa na ongezeko kwenye usaidizi wa kiafya ambao pia unaweza kuathiri pakubwa matokeo ya elimu. Na taasisi nyingi zisizo za kiserikali kama vile shule za binafsi, za jumuiya na zile zisizo rasmi kwa pamoja ziko bega kwa bega na shule za serikali katika utoaji wa elimu.

Ujenzi wa shule na madarasa

Upatikanaji wa jengo la shule mara nyingi huchukuliwa kama hatua ya kwanza katika kuhakikisha kwamba watoto wanahudhuria shule. Nchini Msumbiji, kwa mfano, uondoshwaji wa ada na kuongeza idadi ya shule za msingi na sekondari mara tatu kati ya 1992 na 2010 kwa kiasi kikubwa vimepunguza idadi ya wanafunzi ambao hawajawahi kabisa kwenda shule.

Kuboresha miundombinu na seka afya

Nchi nyingi kwa kiasi kikubwa zimeboresha miundombinu ya barabara, umeme na maji, na hivyo kuongeza upatikanaji wa shule. Uandikishwaji wa wasichana kipekee hutegemea zaidi umbali wa mahali shule ilipo na ubora wa miundombinu, nchi ya India ikiwa ni mfano muhimu.

Taasisi binafsi na nyingine zisizo za Serikali zimekuwa watoaji muhimu wa elimu

Uwajibikaji wa shule za binafsi kwenye elimu umeongezeka kwa miongo miwili sasa. Huko Asia ya Kusini, karibu theluthi ya watoto wenye umri wa miaka 6 hadi 18 husoma shule za binafsi. Uandikishwaji kwenye shule za msingi za binafsi angalau umeongezeka mara dufu kwenye nchi nyingi za Uarabuni, Ulaya ya Kati na Magharibi, na nchi za Kusini mwa jangwa la Sahara.

Shule za kijamii mara nyingi ni rahisi kurekebisha, hazina gharama kubwa, hulenga mahitaji ya wanafunzi na ya wanajamii wa eneo husika kuliko shule za serikali. Nyingi hutoa huduma za elimu kwenye maeneo yaliyotelekezwa na serikali, kwa mfano, nchi ya Ghana, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zambia.

Vituo vya elimu visivyo rasmi hutoa programu nyumbufu za elimu na za haraka kuziba pengo la mfumo rasmi au kwa watoto wadogo waliokosa shule. Nchini Bangladesh, BRAC, shirika kubwa lisilo la kiserikali, huendesha maelfu ya shule zisizo rasmi.

Shule za mashirika ya kidini huziba pengo la elimu kwa wazazi wengi. Nchini Afghanistan, Bangladesh na Pakistan, shule za kiislamu, ziiitwazo madrasas, zimebeba wajibu mkubwa wa kutoa elimu kwa makundi yaliyokosa haki za kimsingi za kijamii. Shirika la Jesuit Network Fey Alegria huko Marekani ya Kilatino (Latin America) limeongeza uandikishwaji wa watoto shuleni kwenye nchi 17 kwa takribani watoto milioni 1.

Kuwafikia watoto walioko pembezoni ni muhimu kwa elimu ya msingi kwa wote

Kuboreshwa kwa sheria na sera kumeongeza ushiriki wa makundi mengi ya walionyimwa haki za kimsingi za kijamii kwenye shule za msingi. Hata hivyo, makundi ya pembezoni, huendelea kukumbana na vikwazo kwenye elimu kwa misingi ya umaskini, jinsia, hadhi katika jamii, kundi-asili na lugha ya jamii, rangi, ulemavu, mazingira ya kijiografia na shughuli za kipato. Watoto walioko pembezoni hukumbwa na viziwi vingi ambavyo huimarishana vyenyewe kwa vyenyewe.

Shule za msingi za binafsi zimeongezeka angalau mara mbili katika nchi nyingi

Kwenye nchi nyingi, watoto wa shule wanaofanya kazi huwa wako nyuma ya wenzao

Makundi madogo ya kijamii na lugha

Kwenye nchi nyingi, kuna pengo kubwa la ushiriki na upatikanaji wa elimu kati ya makundi ya walio wengi, ambao huongea lugha maarufu zaidi na makundi ya wachache ambao huongea lugha nyingine. Katika mazingira mengine maelekezo yaliyoko kwenye lugha ya mtu ya asili na lugha mbili yanaonekana kuboresha upatikana wa elimu kwa makundi madogo yanayoongea lugha zisizo maarufu.

Watoto walioko kwenye ajira

Ajira za utotoni huathiri mafanikio ya elimu. Upatikanaji wa elimu na utekelezaji wa sheria za elimu unaweza kupunguza ajira za utotoni, na hivyo kuboresha matokeo ya elimu na kupunguza umaskini. Idadi ya watoto wenye umri miaka 5 hadi 11 walioko kwenye ajira ilipungua kutoka 139 milioni mwaka 2000 hadi 73 milioni mwaka 2012. Kwenye nchi nyingi, watoto wa shule wenye umri wa miaka 13 wanaofanya kazi huwa nyuma ya wenzao wasiofanya kazi.

Jamii zinazohamama

Jamii za wafugaji zinaendelea kuwa nyuma sana kielimu. Tangu mwaka 2000, mipango mahususi kwa jamii zinazohamama zimejitokeza nchini Ethiopia, Nigeria, Sudan na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini yumkini hazijaongeza uandikishwaji. Elimu huria na ya masafa, mfumo ambao umeokana kufaa kwa jamii zinazohamama, haujasambaa.

Watoto waathiriwa wa VVU na UKIMWI

Tangu Dakar, ongezeko kwenye ufadhili, sera na huduma za misaada kwa watoto waathiriwa wa VVU na UKIMWI umelenga zaidi kwenye malezi, matibabu na ustawi wa kijamii lakini haujatoa kipaumbele kwenye elimu. Sera za kwanza kujikita kwenye upatikanaji wa elimu kwa watoto yatima na wale walioko kwenye mazingira hatarishi zilijitokeza katikati ya miaka ya 2000. Tangu hapo nchi nyingi za Kusini mwa jangwa la Sahara na Asia ya Kusini na Magharibi zimeanzisha mipango kazi ya kitaifa kwa watoto kama hao.



Credit: Philippe Body

Watoto wanaoishi kwenye maeneo duni

Mnamo mwaka 2000, serikali nyingi hazikuwa na uhakiki kuhusu utoaji wa elimu kwenye maeneo duni. Tangu wakati huo, suala la watoto wanaoishi kwenye maeneo duni limekuwa zito zaidi likiwa na ongezeko kubwa la watu kutoka vijijini. Kukiwa na ukosefu wa sera na mipango ya serikali za kufaa, mashirika yasiyo ya serikali na sekta binafsi zimechangia pakubwa. Shule binafsi zinazotoza ada nafuu zimeenea kwa kasi kwenye mitaa duni katika nchi nyingi kama India, Kenya na Nigeria.

Watoto wenye ulemavu

Inakadiriwa kuwa kati ya watoto 93 milioni na 150 milioni wanaishi na ulemavu, jambo ambalo huongeza uwezekano wa wao kuwa kwenye hatari ya kutengwa kwenye elimu. Katika nchi zinazoendelea, ulemavu huhusishwa moja kwa moja na umaskini, na huzuia upatikanaji wa elimu kuliko hata hadhi/ hali ya kijamii na kiuchumi, maeneo ya vijijini au jinsia. Wasichana wenye ulemavu wako kwenye hatari ya kutengwa zaidi. Upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu mara nyingi huzuiwa na ukosefu wa ufahamu kuhusu aina tofauti za ulemavu na mahitaji ya watoto walemavu, vilevile upungufu wa mafunzo ya walimu na nyenzo halisi za mafunzo, na mitazamo ya kibaguzi kwenye ulemavu na tofauti ya hali za maisha.

Nchi nyingi zimeanza kuwahusisha watoto wenye ulemavu kwenye elimu jumuishi, ingawa baadhi yao bado wanapendelea utengano. Kwa kawaida, nchi nyingi zina sera chotara (mchanganyiko) na zinaendelea kuboresha utendaji jumuishi. Mielekeo inayohusisha jamii, wazazi na watoto wenyewe inaonekana kufaa zaidi katika kutoa ufumbuzi endelevu wa kufaa.

Elimu kwenye maeneo yenye hatari changamani ni tatizo linalokua

Elimu kwenye maeneoyenye hatari changamani -kama vile vita, vurugu za kijamii na uhamaji mkubwa wa watu - ni tatizo zito linalokua. Matukio hatarishi yanaweza kusababisha uvamizi mkubwa kwenye shule, au vurumai za za kingono, na hivyo kuyatenga zaidi makundi ambayo tayari yako kwenye mazingira magumu. Wavulana na wasichana wako kwenye hatari ya kuingizwa jeshini kwa nguvu, wakati mwingine kutolewa darasani na kufanywa askari wapiganaji, majajusi, wauaji wa kujilipua kwa mabomu au kuwa watumwa wa ngono. Wasichana huathiriwa zaidi na hali za migogoro.

Tangu mwaka 2000, Mtandao wa kimataifa unaojijuhisha na elimu kwenye maeneo ya hatari (Inter-Agency Network on Education in Emergencies) umekua na mtandao mpana wa mashirika na watu binafsi kwenye zaidi ya nchi 170. Uanzishwaji wa vigezo vya chini kabisa vya elimu kwenye maeneo hatarishi mwaka 2003 ilikuwa ni hatua muhimu: kilichofuata ni ukuzaji wa ahadi za kifedha kwa mataifa duni/dhaifu kutoka shirika la Ubia wa Dunia kwa Ajili ya Elimu (Global Partnership for Education). Pamoja na kukua huko, upungufu wa ufadhili kwenye elimu kutoka kwenye bajeti ya misaada ya kibinadamu bado ni tatizo kubwa.

Migogoro bado kikwazo kikubwa cha elimu kwa watu wengi

KADI YA RIPOTI 2000–2015

LENGO LA 3 Stadi na elimu ya sekondari ngazi ya chini

Kuhakikisha kuwa mahitaji ya kujifunza kwa vijana wote na watu wazima yanatimizwa kupitia upatikanaji sawa wa programu za kujifunza na stadi za maisha

<p><i>Alama za kimataifa*</i></p> <p>*kati ya nchi 75 zenye takwimu</p>	<p>mbali sana na lengo 11%</p> <p>mbali na lengo 35%</p> <p>karibu na lengo 9%</p> <p>waliofikia lengo 45%</p>
<p><i>Mafanikio</i></p> <p>✓✓</p>	<p>Uandikishwaji ↑27% kidunia Uiongezeka zaidi ya mara 2 nchi za Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara</p> <p>1999 sasa</p> <p>Uwiano wa uandikishwaji wa jumla umeongezeka</p> <p>1999: sekondari ngazi ya chini 71%, sekondari ngazi ya juu 45%</p> <p>2012: sekondari ngazi ya chini 85%, sekondari ngazi ya juu 62%</p> <p>Idadi ya watoto waliobalehe walioko nje ya shule imepungua</p> <p>1999: 99 milioni</p> <p>2012: 63 milioni</p>
<p><i>Jitihada zilizofanyika</i></p> <p>✓</p>	<p>shule ya sekondari ngazi ya chini</p> <p>94 nchi zilozifanya elimu bure</p> <p>27 nchi zilizoifanya elimu kuwa ya lazima</p> <p>Maendeleo ya tathmini ya moja kwa moja ya stadi</p> <p>PIAAC, STEP</p> <p>Uelewa bora wa VVU/UKIMWI tangu 2000</p>
<p><i>Changamoto zilizopo bado</i></p> <p>X</p>	<p>watoto waliobalehe walioko nje ya shule</p> <p>63 milioni mwaka 2012</p> <p>waliomaliza sekondari ngazi ya chini</p> <p>1/3 ya watoto waliobalehe kwenye nchi za kipato cha chini na kati hawatakuwa wamemaliza sekondari ngazi ya chini ifikapo 2015</p> <p>Stadi/ ujuzi</p> <p>Ukosefu wa kueleweka kwa aina za stadi/</p> <p>vijana wanaofanya kazi</p> <p>Idadi haijapungua</p> <p>Fursa ya pili ya kupata elimu</p> <p>hitaji sugu la upatikanaji zaidi</p>
<p><i>Mafanikio yanayotofautiana</i></p>	<p>Uandikishwaji sekondari ngazi ya chini/juu</p> <p>Utajiri</p> <p>Mahali</p> <p>Tangu 2000, pengo kati ya tajiri na maskini wanaomaliza sekondari ngazi ya chinina kuingia ngazi ya juu ni kama halikupungua</p> <p>Ni nchi chache tu ndizo zilipungua kwa kasi tofauti ya upatikanaji wa shule za sekondari baina ya vijijini na mijini (hasa Viet Nam, Nepal na Indonesia)</p>
<p><i>Mapendekezo kwa ajili ya kipindi kufuatia mwaka 2015</i></p>	<ol style="list-style-type: none"> 1. Elimu ya sekondari lazima iwafikie wote 2. Programu za utoaji wa fursa ya pili ya elimu fursa za kuboresha lazima zipanuliwe 3. Fasili bora zaidi za stadi na takwimu zinazoelekeana za baada ya 2015 zinahitajika

LENGO 3 Ujuzi kwa vijana na watu wazima

Kuhakikisha kwamba mahitaji ya mafunzo kwa vijana wote na watu wazima yanatoshelezwa kwa usawa katika upatikanaji wa programu mwafaka za mafunzo ya stadi za maisha.

Lengo la 3 la ELIMU KWA WOTE siyo tu ni la elimu rasmi shuleni lakini pia kwenye matukio ya nje ya shule, kama vile utoaji mafunzo kazini na fursa nyingine za maisha. Mlengo mpana wa lengo namba 3 haukueleweka vizuri: ulikosa shabaha iliyo wazi na inayopimika na hurejea kwenye matokeo –stadi za maisha-ambazo zinaweza kueleweka kwa namna nyingi.

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ya 2015 inalenga kwenye aina tatu za stadi. Stadi za msingi ni zile zinazohitajika kuwezesha upatikanaji wa kazi au mafunzo yanayoendelea. Stadi za kuhawilishwa zinaweza kurekebisha kwenye mazingira tofauti, ikiwa ni pamoja na yale yanayohusiana na kazi. Stadi za ufundi na kazi ndio zilizo mahususi kwa ujuzi wa kutenda kulingana na kazi husika.

Kiashirio muhimu zaidi cha maendeleo kuhusu upatikanaji wa fursa za stadi za msingi ni kupata shule ya sekondari. Ingawa kumekuwa na maendeleo makubwa katika kupanua upatikanaji wa elimu ya sekondari ngazi ya chini na hata ya juu, bado hakuna usawa wa kipato na mahali pa kuishi. Watoto wengi, hususani wale wanaotoka kaya maskini, mara nyingi hulazimika kufanya kazi, jambo ambalo huathiri vibaya ushiriki, kumaliza shule na mafanikio kitaaluma kwenye elimu ya sekondari. Hadhi ya kisheria isiyo ya uhakika kwa watoto wahamiaji

kutaendelea kuwaweka kwenye hatari ya kuendelea kutengwa zaidi, hadi pale nchi husika zitakapowaha kikishia upatikanaji wa shule za sekondari.

Stadi za msingi: Ushiriki kwenye elimu ya sekondari umeongezeka

Stadi za msingi huhusisha ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu unaohitajika kumwezesha mhusika kupata kazi nzuri itakayompa kipato cha kujikimu kwenye mahitaji yake ya kila siku. Stadi za msingi zipatikanazo katika shule ya sekondari ni muhimu kwa ukuaji kitaaluma, uraia hai na uchaguzi salama kuhusu afya binafsi. Ushiriki kwenye shule ya sekondari umeongezeka kwa haraka tangu 1999, kukiwa na wanafunzi 551 milioni walioandikishwa mwaka 2012. Uwiano ghafi wa uandikishwaji kwenye elimu ya sekondari uliongezeka katika nchi za kipato cha chini (kutoka 29% hadi 44%) na kipato cha kati (kutoka 56% hadi 74%).


Ufutaji wa ada za shule umechangia kuongezeka kwa uandikishwaji kwenye shule za sekondari. Kati ya nchi 107 za kipato cha chini na kati zenye takwimu, 94 zimepitisha sheria ya elimu bure kwenye elimu ya sekondari ngazi ya chini. Kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaomaliza elimu ya msingi kwenye nchi nyingi pia kumechangia na kuwezesha watoto wengi kuwa na sifa ya kuendelea na masomo ya juu.

Mlengo mpana wa lengo la 3 haukueleweka vizuri:

Kielelezo 6: Uwiano wa vijana waliobalehe shuleni uliongezeka kwa 12% wakati wa kipindi cha

Mwongozo wa Dakar

Uwiano halisi wa uandikishwaji (jumla) wa sekondari ngazi ya chini, katika dunia na kanda 1999–2012 and 2015 (makadirio)



Vyanzo: Takwimu za UIS; Bruneforth (2015).

Uhitaji na upendeleo wa watu kwenye shule za binafsi umeongezeka. Kati ya 1999 na 2012, asilimia ya uandikishwaji kwenye shule za sekondari za binafsi ulipanda kutoka 15% hadi 17% katika nchi zinazoendelea; ongezeko hilo lilijulikana wazi kwenye nchi za Kiarabu na Asia Mashariki.

Ukosefu wa usawa kwenye elimu ya sekondari bado upo

Huku upatikanaji wa elimu ya sekondari ukienea polepole kwa wote, mara zote wale walioko kwenye makundi bora hufikiwa kwanza na baadaye wale walioko pembezoni, maskini na wale wa maeneo ya vijijini. Ukosefu wa usawa kwenye upatikanaji wa elimu ya sekondari ngazi ya chini mara nyingi humaanisha pia ukosefu wa usawa kwenye elimu ya sekondari ngazi ya juu. Hali hii huonekana hata katika nchi ambazo huahidi fursa za elimu kwa watoto wote bila kujali uwezo wao wa kulipa.

Hata kama upatikanaji wa shule umeongezeka, idadi kubwa ya watoto waliobalehe wenye umri wa shule ya sekondari wameendelea kufanya kazi nje ya shule kwenye nchi nyingi sana. Baadhi yao huacha kabisa shule, huku wengine wakisoma huku wakifanya kazi. Wanafunzi walioko kwenye ajira hukawia kupata stadi za msingi. Asilimia ya wanafunzi walio kwenye ajira inaelekea hupewa kipimo cha chini, kwa kuwa wazazi husita kuwaeleza wahojaji kuwa watoto wao wako kwenye ajira.

Namna ya kuelezea mahitaji ya vijana wahamaji katika kupata stadi ni jambo linaloleta hofu kwenye kanda zote na pia huhitaji fedha zaidi. Uchunguzi wa sera za uhamiaji kwenye nchi 14 zilizoendelea na 14 zinazoendelea ulibaini kuwa 40% ya nchi zilizoendelea na zaidi ya 50% ya nchi zinazoendelea hazikuruhusu watoto wenye hadhi isiyoeleweka ya kisheria kupata elimu shuleni. Sera zinazohusu lugha ya kufundishia ni muhimu kwa elimu ya vijana wahamaji na ushiriki wao wa siku za mbele kwenye soko la ajira.

Mbadala wa elimu unahitajika kwa vijana na watu wazima ambao hawako shuleni

Pamoja na upanuzi wa elimu rasmi, nchi nyingi zimejitolea kutimiza mahitaji ya kielimu kwa vijana ambao hawako shuleni na watu wazima ambao fursa zao za elimu rasmi zilikatizwa. Hapa chini ni mifano ya programu mbadala, 'nafasi ya pili' na zisizo rasmi.

Nchini Bangladesh, programu za BRAC hulenga kuwapa watoto walio nje ya shule elimu ya msingi na kuwandaa kwenda ngazi ya sekondari. Zaidi ya 97% ya wahitimu wa shule za msingi za BRAC huendelea kwenye shule rasmi za sekondari.

Nchini India, Taasisi ya Taifa ya Elimu Huria hutoa programu za elimu ya msingi huria kwa watoto wenye

umri wa miaka 19 na kuendelea. Wanafunzi hao pia hupata nafasi kwenye kozi za ufundi na programu za ustawishaji maisha. Ambapo kwa mwaka 2011, jumla ya wanafunzi 2.2 milioni walinufaika na programu hizi.

Nchini Thailand, mpango kazi wa kitaifa uliunganisha malengo ya 3 na 4 ya ELIMU KWA WOTE na kuwa lengo moja lililounganishwa likilenga kisomo cha watu wazima na elimu ya msingi na endelevu kwa watu wazima wote. Mpango huu ulitoa mbadala wa elimu kwa watu wengi wa namna mbalimbali, wakiwemo wafungwa na watoto wa mitaani.

Stadi hawilishwi: Uwezo unaosaidia maendeleo ya jamii

Ikiwa ni nyongeza ya ahadi ya lengo la 3 ya kuhakikisha kwamba vijana na watu wazima wanapata fursa sawa za masomo na stadi za maisha, Mwongozo wa Dakar ulieleza: "Ni lazima vijana na watu wazima wote wapewe fursa ya kupata maarifa na kuendeleza maadili yao, mitazamo na stadi ambazo zitawawezesha kukuza uwezo wao wa kufanya kazi, kushiriki kikamilifu kwenye jamii yao, kudhibiti maisha yao wenyewe na kuendelea kujifunza. Ufuatiliaji wa lengo hili pana unahitaji taarifa za kina kuhusu madili, mitazamo na stadi zisizo za kitaaluma ambazo hazipimwi kimataifa na hazimo kwenye mifumo ya taifa ya elimu.

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ya mwaka 2015 inaziweka wazi aina mbili za stadi za maisha zinazohusu afya na jamii, maarifa juu ya VVU na UKIMWI, na mitazamo kuhusu usawa wa jinsia.

Elimu kuhusu VVU na UKIMWI imeongezeka lakini bado haijawafikia wote: Tafti za hivi karibuni zinaonyesha maendeleo kwenye maarifa ya VVU na UKIMWI miongoni mwa vijana wa kiume kwenye nchi 9 na vijana wa kike kwenye nchi 13. Nchi zinazoonyesha maendeleo makubwa zaidi ni zile ambazo UKIMWI ulikuwa umeenea zaidi. Ni kana kwamba msisitizo wa elimu ya UKIMWI shuleni kwenye nchi hizi ni mkubwa zaidi, na kwamba elimu ya stadi za maisha imekuwa na mchango mkubwa.

Mitazamo kuhusu usawa wa kijinsia haijawa bora ipasavyo: Kwa zaidi ya miaka 20, Utafiti wa dunia kuhusu maadili na imani za watu umekuwa ukiwauliza wahojiwa endapo walikubali kwamba elimu ya chuo kikuu ilikuwa muhimu zaidi kwa wanaume kuliko wanawake. Kwa miaka ya hivi karibuni kwenye baadhi ya nchi (kwa mfano, Ukraine na Morocco) wahojiwa wengi hawakubaliana na kauli hiyo, na hivyo kubainisha mitazamo chanya kuhusu wanawake kwenye elimu ya juu. Lakini kwenye nchi nyingine hapakuwa na badiliko, na baadhi (kwa mfano, Kyrgyzstan na Pakistan) mitazamo ya wahojiwa kuhusu usawa wa kijinsia ilikuwa mibaya zaidi.

Stadi za ufundi na kazi: Mielekeo inajitokeza

Mtu anaweza kupata stadi za ufundi kupitia elimu ya sekondari na shule rasmi za ufundi, au kupitia mafunzo ya kazini, ikiwa ni pamoja na uanagenzi wa kimapokeo mafunzo kupitia vyama vya ushirika vya kilimo. Kulikuwa na nchi 28 ambazo baadhi zilionesha ongezeko kubwa kwenye asilimia ya wanafunzi walioandikishwa kwenye mkondo wa ufundi tofauti na mikondo ya kawaida, ukilinganisha na uandikishwaji wa wote wa sekondari; miongoni mwa nchi hizi, 12 zilionyesha ongezeko na 16 viwango vilishuka.

Mwaka 2000, watetezi wa stadi za ufundi na kazi walikuwa wachache, kwani Baraza la Dunia la Elimu la Dakar, na matokeo ya lengo namba 3 vilikuwa bado kuainishwa vema. Hata hivyo, umakini kwenye elimu ya ufundi umeongezeka zaidi kwa miaka ya hivi karibuni, hususan kutoka Muungano wa Ulaya na OECD. Sababu nyingine kwa mlengo huu ni kwamba fasili ya stadi imepanuliwa zaidi ya yale yanayohusiana na kujipatia riziki. Watetezi wengi zaidi sasa hawaoni tena mafunzo ya stadi kama ni mafunzo nje ya mfumo wa kawaida wa elimu, kama kiungo muhimu katika kukamilisha mfumo huo, wakitoa stadi za msingi na zile zinazohawilishika wakati huo huo kama stadi za kazi.

Elimu endelevu na elimu ya watu wazima: mifano minne inayotofautiana

Endapo fursa hazitaandaliwa kwa umakini, basi fursa ya elimu ya watu wazima hujikuta ikichukuliwa na wale ambao tayari walishanufaika na mfumo wa elimu rasmi. Nchi nne ambazo kwa miaka ya hivi karibuni zimejaribu kushughulikia usawa wa fursa kwenye elimu ya watu wazima, zimepata matokeo tofauti tofauti

Programu ya stadi za Elimu ya Vijana na Watu Wazima nchini Brazil imejielekeza kwa wale wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ambao hawakuweza kumaliza elimu rasmi. Mwaka 2012, zaidi ya wanafunzi milioni 3 waliandikishwa, hawa ni pamoja na wahamiaji, wafanyakazi wa vijijini na watu kutoka familia maskini au zile za wafanyakazi wa kawaida. Hata hivyo, ubora wa elimu iliyopatikana una kasoro na idadi ya wale wanaoshindwa kumaliza ni kubwa.

Mwaka 2006, Norway ilihamasisha jitihada kubwa ambazo zilielekeza fedha kwa waajiri kwa ajili ya mafunzo kwa wafanyakazi wao wenye viwango duni vya ujuzi kwenye kusoma na kuandika, kuhesabu, TEHAMA na mawasiliano ya moja kwa moja ya mdomo. Mfumo wa nchi wa elimu ya watu wazima ni mpana: programu za nje ya mfumo rasmi wa elimu huhusisha pia ‘sekondari za juu za wazee’, mashirika ya elimu, vituo vya mafunzo ya lugha kwa wahamiaji, na elimu ya masafa.

Mwaka 2007, Jamhuri ya Korea ilipitia upya uratibu, maendeleo na utekelezaji wa elimu ya watu wazima. Shughuli nyingi zilisanifiwa upya ili kuwezesha uhamasishaji wa wadau, kama vile kampeni ya kuchagua na kukuza miji ya ujifunzaji maisha yote Viwango vya ushiriki viliongezeka kutoka takribani 26% mwaka 2008 hadi 36% mwaka 2012. Serikali pia ilianzisha mifumo minne ya kukuza stadi zinazohusiana na kazi kwa waajiriwa wa makampuni madogo na yale ya kati.

Mnamo mwaka 2005, nchini Vietnam, mfumo usio rasmi wa elimu ya watu wazima na kisomo cha watu wazima viliingizwa kwenye vipengele vikuu vine vya mfumo wa kawaida wa elimu. Kwa mwaka 2008, kulikuwa na takribani washiriki 10 milioni kwenye elimu ya watu wazima na programu za elimu isiyo rasmi, ikilinganishwa na zaidi kidogo tu ya watu nusu milioni kwa mwaka 1999.

Vipimo vya moja kwa moja vya stadi ngumu na nyepesi vinaibuka kwenye nchi nyingi

Stadi zenye hisia za kijamii (nyepesi) zinaweza kufundishwa kupitia matukio chanya ya shuleni na zinaweza kuwa na umuhimu sawa na ule wa stadi tambuzi (ngumu) katika kufikia matokeo chanya ya soko la ajira. Mifano miwili ya vipimo vya moja kwa moja vya stadi ngumu na nyepesi ni programu za OECD kwa ajili ya Tathmini ya Kimataifa ya Stadi za Watu Wazima (OECD's Programme for the International Assessment of Adult Competencies -PIAAC), na tafiti inayoendelea ya Benki ya Dunia kuhusu Stadi Kuelekea Ajira na Tija (Skills Toward Employment and Productivity- STEP). Matokeo yake yanaweza na yanapaswa kujibu swali la msingi kuhusu jinsi ambavyo aina tofauti za elimu zinavyochangia kwenye stadi na mafunzo, na jinsi stadi hizi zinavyoweza kukuza fursa za ajira kwa mtu binafsi na ushiriki wa umma.

PIAAC ilitathmini stadi zinazotumiwa na watu wazima kujua kusoma na kuandika na kuhesabu na uwezo wa hizo stadi kutatua matatizo kwenye mazingira yenye aina nyingi za teknolojia. Ushahidi unaonyesha kuwa licha ya kwamba mtu aliyekwisha acha shule anaweza kujifunza stadi hizo, bali pia zinaweza kupotea kama hazitumiki mara kwa mara. Pia unaashiria kwamba wale waliokwisha hudhuria programu za ufundi, viwango vyao vya ujuzi ni vya chini zaidi kuliko wale walioko kwenye programu za kawaida.



















STEP imelenga zaidi sampuli za kaya na makampuni kwenye maeneo ya mjini kwenye nchi za kipato cha kati. STEP inatafiti ustadi wa kusoma na pia stadi za kazi maalumu, ikiwa ni pamoja na kuhesabu na matumizi ya kompyuta, stadi ambazo hutumika ndani na nje ya kazi. Kwa ujumla, STEP ilihakiki umuhimu wa stadi nyepesi, na kipekee zaidi ilibainisha kuwa uwazi hukuzi matokeo, hata pale ambapo miaka ya elimu inazingatiwa.

Takribani watu wazima milioni 10 walishiriki kwenye programu za elimu nchini Vietnam mwaka 2008

KADI YA RIPOTI 2000–2015

LENGO LA 4 Kisomo cha watu wazima na elimu

Kufikia 50% ya maendeleo katika ngazi zote za kisomo cha watu wazima na elimu ifikapo 2015, hasa kwa wanawake, na upatikanaji sawa wa elimu ya msingi na endelevu kwa watu wazima wote

<p><i>Alama za kimataifa*</i></p> <p>* kati ya nchi 73 zenye takwimu</p>	<div style="display: flex; justify-content: space-around;"> <div style="text-align: center;"> <p>mbali sana na lengo</p>  <p>32%</p> </div> <div style="text-align: center;"> <p>mbali na lengo</p>  <p>26%</p> </div> <div style="text-align: center;"> <p>karibu na lengo</p>  <p>19%</p> </div> <div style="text-align: center;"> <p>waliofikia lengo</p>  <p>23%</p> </div> </div>			
<p><i>Mafanikio</i></p> 	<p>Kiwango cha watu wazima kujua kisomo Mwenendo wa dunia</p>  <p>2000 2015</p> <p>Asia ya Kati na Ulaya ya Kati na Mashariki ndio wanatarajiwa kupunguza viwango vya kutokujua kisomo angalau kwa nusu ifikapo 2015</p> 	<p>Tangu 2000, kiwango cha kutokujua kisomo kilishuka kwa:</p> 		
<p><i>Jitihada zilizofanyika</i></p> 	<p>Kampeni nyingi zaidi na ahadi za dunia</p>  <p>Hitaji zaidi la kujua kisomo</p>	<p>Tathmini za kujua kisomo 2000</p> <p>.....</p> <p>Unaweza kusoma na kuandika</p> <p>N <input type="checkbox"/> H <input type="checkbox"/></p> <p>Sasa Moja kwa moja</p> <p>Soma sentensi hii na uandike jina lako</p> 		
<p><i>Changamoto zilizopo bado</i></p> 	<p>Angalau watu wazima 781 milioni hawana stadi za msingi za kujua kisomo</p> 	<p>Wanawake watafikia 64% ya watu wazima wasiojua kisomo mwaka 2015</p>  <p>– hakuna mabadiliko tangu 2000</p>	<p>Maendeleo ya kujua kisomo kwa watu wazima hasa yanasababishwa na vijana waliosoma kuingia umri wa utu uzima</p> 	
<p><i>Mafanikio yanayotofautiana</i></p>	<p>Ukusanyaji bora Teknolojia mpya wa takwimu</p> 	<p>Uelewa bora zaidi wa stadi za kisomo kama kipimo</p>  <p>wanaojua kisomo wasiojua kisomo</p>	<p>Uelewa bora wa matokeo ya kutokujua kisomo kwenye elimu, demokrasia na uwezeshaji</p> 	
<p><i>Mapendekezo kwa ajili ya kipindi kufuatia mwaka 2015</i></p>	<ol style="list-style-type: none"> 1. Takwimu zinahitajika ili kuaksi mikataba inayojitokeza ambayo haielezwi kwa uwazi lakini ipo kwenye kipimo 2. Nchi zinapaswa kuainisha kiwango cha wanaojua kusoma na kuandika, kulingana na mikataba, kwamba watu wazima wote lazima wafikiwe <p><i>Fikiri upya</i></p>			

LENGO 4

Kisomo (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) cha Watu Wazima

Kufikia mafanikio ya 50% ya viwango vya kisomo cha watu wazima ifikapo 2015, hususan kwa wanawake, na upatikanaji sawa wa elimu ya msingi na endelevu kwa watu wazima wote.

Ni lazima tuzipongeze jitahada nyingi chanya zilizofanywa kuhusu mielekeo ya kisomo cha watu wazima tangu mwaka 2000. Kumekuwa na mwelekeo wazi kwenye upimaji wa stadi za kisomo kwa uendelevu, tofauti na tathmini ambazo ziliainisha watu wazima ama kama wenye stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu au kinyume chake; mwelekeo ambao, ambao umeathiri sera na maendeleo ya programu kwenye nchi nyingi. Hata hivyo, ni nchi chache sana zilifikia lengo la kisomo cha ELIMU KWA WOTE la kupunguza kwa nusu, ifikapo mwaka 2015, kiwango cha watu wazima kutojua kusoma na kuandika kilichokuwepo mwaka 2000.

Maendeleo kuelekea lengo la 4 la ELIMU KWA WOTE yamekuwa na kasi ndogo zaidi kuliko kwenye malengo mengine. Karibu watu wazima 781 milioni hawana stadi za kusoma na kuandika. Kupungua kwa idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kwa sehemu kunaaksi ingizo la vijana wadogo zaidi kiumri, ambao wamesoma zaidi wanaoingia utu uzima, kuliko kuwainua watu wazima waliopitiliza umri wa shule.

Nchi nyingi bado hazijatimiza lengo la 4

Kufuatilia kisomo cha watu wazima kunahitaji taarifa thabiti kuwezesha ulinganishi. Lakini kwa sababu fasili za kisomo (uwezo wa kusoma na kuandika) zimebadilika tangu mwaka 2000, upatikanaji wa taarifa hizo unaweza kuwa ni changamoto. Kwa kulenga nchi ambazo kiwango cha kisomo kiko chini ya 95% kwa kipindi cha 1995-2004 na mahali ambapo taarifa zilitoka kulingana na matamko binafsi, ni nchi 17 tu kati ya 73 ndizo zinakaridiwa kupunguza angalau nusu viwango vyao kufikia mwaka 2015. Nchi maskini ziliendelea kuwa mbali zaidi katika kufikia lengo.

Uchambuzi wa nchi hizi 73 unaonyesha badiliko lilokadiriwa hadi kufikia 2015 ni la haraka zaidi kwa wanawake kuliko wanaume. Nchi zote ambazo zina wanawake pungufu ya 90 kwenye kila wanaume 100 kwa mwaka 2000 zimekaribia usawa wa kijinsia.

Tafti za kimataifa na kitaifa husaidia tathmini ya moja kwa moja ya kisomo

Viwango vingi vya tafti za kaya ambazo hutathmini stadi za kisomo huegemea zaidi kwenye mgawanyo rahisi wa jozi kati ya kujua na kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Tangu mwaka 2000, hata hivyo, kisomo kimeongezeka kukubalika kama mwendelezo wa stadi. Nchi na mashirika ya kimataifa si tu yameanza kufanya uchunguzi wa kisasa zaidi ili kutathmini kama watu wazima wanajua au hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu, lakini pia viwango vyao vya kisomo.

Tangu mwaka 2000, programu mbili kuu za kimataifa za tafti za kaya, Tafti za Demografia na Afya (Demographic and Health Surveys) na Tafti za kundi-ashiria la mchanganyiko (Multiple Indicator Cluster Surveys), zinajaribu kutathmini uwezo wa kujua kusoma na kuandika kwa kuwaomba moja kwa moja wahojiwa kusoma sentensi iliyoandikwa kwenye kadi. Pale makadirio yanapoegemea kwenye tathmini ya moja kwa moja, watu wazima wengi zaidi walionekana kukosa stadi za kusoma kuliko pale ambapo makadirio yalitoka kwenye tamko binafsi.

Programu ya OECD ya PIAAC, ambayo ilifanyia utafiti watu 166,000 wenye umri wa miaka 16 hadi 65 kwenye jamii 25 zenye viwango wa juu vya watu kusoma na kuandika, ulionyesha kwamba, hata kwenye nchi zenye kipato kikubwa, watu wazima wachache walionekana kuwa na uwezo mdogo wa kusoma. Kwenye nchi kama Ufaransa, Italia na Uhispania, zaidi ya mtu mmoja kati ya watu wazima wanne alikuwa na uwezo wa chini wa kusoma na kuandika.

UIS ilianzisha Programu ya Kutathmini na Kufuatilia Uwezo wa kisomo (Literacy Assessment and Monitoring Programme –LAMP) ili kuangazia ukubwa tofauti wa uwezo wa kisomo kama ilivyopimwa kwenye kusoma lugha ya mjazo, nyaraka na kuhesabu. LAMP ilichukua sampuli za watu wazima kutoka maeneo ya mijini na vijijini huko Jordan, Mongolia, Palestina na Paraguay. Programu ilifasili aina tatu za viwango vya mafanikio ya kujua kusoma na kuandika. Matokeo kutoka Paraguay yalionyesha kuwa watu wazima kutoka maeneo ya vijijini walikuwa na uwezo duni wa kusoma lugha ya mjazo kuliko wakazi wa mijini, labda kwa sababu wakazi wa vijijini waliojitambulisha kuwa lugha yao ya asili ni Kihispaniola walikuwa wachache zaidi kuliko wale wa mijini.

Nchi 17
zita kuwa
zimefikia
lengo la
kisomo
ifikapo 2015

Tathmini za kitaifa za kisomo cha watu wazima

Nchi nyingi zenye viwango vya chini zaidi vya wanaojua kusoma na kuandika zimeanza kutumia tathmini mfuatano za kisomo. Tathmini hizi hutoa matokeo sahihi zaidi kuliko tafiti za matamko ya kaya kuhusu wanaojua kusoma na kuandika ukilinganisha wasiojua. Kwa mfano, Utafiti wa Kitaifa wa Kisomo cha Watu Wazima nchini Kenya mwaka 2006, ulibainisha tofauti kubwa kati ya vijijini na mijini na kwamba kiwango cha taifa cha watu wazima kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kilikuwa 59% kwa wanawake, pointi 13 pungufu ya makadirio ya UIS ambayo yaliegemea zaidi kwenye matamko binafsi kuhusu uwezo wa kusoma. Matokeo kwa wanaume yalikuwa ni 64%, pointi 15 pungufu ya makadirio ya UIS.

Kulinganisha makundi fungamano (cohort) kunaonyesha kuwa karibu hakuna maendeleo katika kisomo cha watu wazima tangu 2000.

Thamani ya kiwango cha watu wazima kujua kisomo katika kutathmini upatikanaji wa maendeleo ya programu za kujua kusoma na kuandika huathiriwa na ukweli kwamba tathmini hiyo huegemea kwenye makundi tofauti ya watu wazima kwa nyakati tofauti. Na matokeo yake, hata kama hakuna mtu miongoni mwao atakayebadilisha hali yake, kiwango cha kujua kisomo kwa watu wazima hao kinaweza kubadilika – kuongezeka; kwa mfano, kama vijana wenye stadi za juu za kisomo wataingia kwenye kundi la watu wazima huku watu wazima wenye stadi hafifu za kisomo wakiondoka.

Iwapo, kwa upande mwingine kundi la watu – au kundi fungamano - limeonekana kuwa na umri wa kati ya miaka 20 hadi 30 mwaka 2000 na 30-40 mwaka 2010, badiliko lolote halitasababishwa na kubadilisha shule bali upatikanaji wa stadi za kusoma na kuandika kupitia programu za kusoma na kuandika au fursa nyingine za maisha. Uchambuzi mpya kwa Ripoti ya Dunia ya Uchambuzi mpya wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ya 2015 unafuata mwelekeo huu.

Matokeo ni kwamba baadhi ya nchi zinaweza kuonekana kwenye mstari wa chini lakini zikawa na maendeleo thabiti ya viwango vya kisomo kwa vijana wanawake, lakini maendeleo haya yanayoonekana hupotea kutoka kundi moja hadi jingine. Kwa mfano, nchini Malawi kiwango cha kisomo kwa wanawake wa umri wa miaka 20 hadi 34 kilikuwa 49% mwaka 2000 na 63% mwaka 2010. Hata hivyo, kiwango cha kisomo kwa wanawake waliokuwa na umri wa miaka 20 hadi 34 mwaka 2000 na 30 hadi 44 mwaka 2010 kilibaki kuwa 49%.

Nchi nyingi zaidi miongoni mwa 30 zilizofanyiwa utafiti, uwezo wa kisomo kwenye kundi husika haukusogea, au hata kushuka pale ambapo stadi hazikutumika ipasavyo. Nepal ilikuwa nchi pekee ambayo ilithibitishwa kuwa na maendeleo endelevu ya kiwango kwenye kundi kwa zaidi ya tafiti tatu. Sababu mojawapo ni mafanikio ya uwekezaji wa serikali wa US\$ 35 milioni kwenye kampeni yake ya Kitaifa ya Kisomo ya 2008-2012.

Maelezo ya maendeleo kidogo katika kisomo cha watu wazima

Kama stadi za kisomo kwa watu wazima ambao wako juu ya umri wa shule hazikuimarika kwenye nchi nyingi zinazoendelea, basi kuna mashaka ya kutosha kwenye matokeo ya jitihada za uboreshaji wa stadi za kujua kisomo tangu mwaka 2000. Dalili nne zinaweza kusaidia kuelezea maendeleo hayo duni: kiasi cha ahadi za kisomo duniani, nguvu za kampeni na programu za kisomo, mawanda ya majaribio ya kuhamasisha programu za kisomo kwa lugha ya asili na mwitikio wa programu kwa uhitaji kisomo.


Ahadi za dunia kwa kisomo cha watu wazima zilikuwa utata

Kwa takribani robo karne iliyopita, jumuiya ya kimataifa mara nyingi imekuwa ikitoa matamko ya kuhamasisha kisomo cha watu wazima. Malengo yaliyotajwa yameinua matarajio kwamba kutojua kisomo kungefuata

Mafanikio mengi ya lengo la 4 yamechangiwa na vijana wenye elimu kufikia utu uzima

Kielelezo cha7: Stadi za kisomo cha watu wazima, kwenye nchi zinazoendelea, zimeboreshwa kiasi kidogo tu

Kiwango cha wanawake wanaojua kisomo, kwenye nchi na makundi umri yaliyochaguliwa mnamo 2000 na 2010



Maelezo: 1. Uwezo wa kujua kusoma na kuandika ulipimwa moja kwa moja. 2. Kwa kila nchi, mstari wa moja kwa moja huwafuatilia kwa muda wanawake ambao walikuwa na umri wa miaka 20-34 wakati wa uchunguzi wa kwanza; kwa mfano, mstari wa moja kwa moja nchini Malawi huwafuatilia wanawake wenye umri wa miaka 20-34 mwaka 2000 ambao walifikisha 30-44 mwaka 2010. Mstari wenye mvumburuko hufuatilia kundi rika hilo hilo; kwa mfano, mstari wenye mvumburuko nchini Malawi unawafuatilia wanawake waliokuwa na miaka 20-34 mwaka 2000 na 2010. Mwaka 2001, utafiti wa idadi ya watu na afya ulifanywa kwa wanawake waliokuwa pekee, lakini mwaka 2006 na 2011, utafiti huo ulihusisha wanawake wote.

Chanzo: Barakat (2015) na Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu Kwa Wote, kulingana na uchambuzi wa takwimu za Utafiti kuhusu Idadi ya Watu na Afya

mwelekeo wa ugonjwa wa polio na kwamba ungeweza kukomeshwa. Uchambuzi wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji kwenye mipango ya kitaifa ya elimu ya nchi 30 kwenye miaka ya 2000 na baada ya 2007 ulionyesha kwamba kisomo cha watu wazima kimepuuzwa ukilinganisha na malengo mengine ya ELIMU KWA WOTE.

Pamoja na juhudi kadhaa za dunia tangu mwaka 2000 ili kubuni upya kisomo cha watu wazima na kuanzisha programu (kama vile Juhudi za Kisomo kwa Ajili ya Kuwezesha), zinazobeba dhana mpya, kufaa kwa programu hizo kwenye utekelezaji kumekuwa ni kidogo. Wengi wao hawakuwa na dira ya muda mrefu sambamba na mikakati ya elimu kitaifa.

Kampeni na programu za kisomo zimebadilika, lakini matokeo yake bado si dhahiri.

Shauku ya mashirika ya kikanda na serikali kuanzisha kampeni za kisomo imeongezeka tangu mwaka 2000, hususan Amerika ya Kusini. Kampeni nyingi zaidi zimewekewa malengo makubwa, lakini muda wa mwisho kutekeleza baadhi ya malengo tayari umeshakwisha pita, na kwa mambo kadhaa malengo hayo hayakutimizwa.

Kampeni kubwa hubeba mashaka. Zinaweza kubeba matarajio yasiyo halisi na si mara zote huandaliwa kitofauti. Lugha ya kampeni mara nyingi huonyesha kutojua kisomo kama ugonjwa wa kijamii ambao unaweza kuondoshwa kama kutakuwa na uingiliaji kati ulio sahihi. Hii inaweza kunyanyapaa na kuwakatisha tamaa wale wenye ujuzi duni wa kisomo na kuwapelekea kuficha hali zao. Kwa ujumla, kampeni za kujua kisomo tangu mwaka 2000 zimekuwa hazina matokeo makubwa ya dunia katika kuboresha stadi za kisomo.

Mendeleo katika kutambua umuhimu wa lugha ya asili

Tangu 2000, masharti yamezipendelea zaidi nchi nyingi zenye viwango duni vya kisomo kuongeza matumizi ya lugha ya asili kama lugha ya mafunzo kwenye programu za kisomo cha watu wazima. Hata hivyo, kutokana na vikwazo vya utaratibu wa maandalizi au hisia kinzani kutoka kwa viongozi wa kisiasa, programu hizo hazijaleta mchango mkubwa katika kuboresha stadi za kisomo cha watu wazima kwa kiwango chochote cha maana.

Mabadiliko katika maisha ya kila siku hayajaleta ongezeko thabiti kwenye uhitaji wa kisomo.

Kisomo kinahitaji siyo tu upatikanaji bora wa fusa za kujifunza, lakini pia huhitaji fursa zaidi za kutumia, kuboresha na kuendelea stadi za kisomo. Fursa hizo zimekuwa zikiongezeka tangu mwaka 2000. Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ya mwaka 2015 inachunguza mifano kwenye soko la kilimo, uingiliaji kati kwenye afya ya umma, mipango ya uwekezaji kwenye biashara ndogondogo za kukopesha fedha na usimamizi wa maji. Pamoja na kuendelea kutambulika kwamba programu za kisomo zinahitaji kuunganishwa kwenye fursa kama hizo, mfiko kwenye upatikanaji wa stadi za kisomo bado haujaonekana.

Hata hivyo, badiliko lingine, kuenea kwa haraka kwa TEHAMA, linaonyesha matumaini makubwa. Inawezekana kutumia vizuri kuenea kwa matumizi makubwa ya simu za kiganjani kutakuza mazingira thabiti zaidi ya kisomo na mazoezi ya kusoma, ingawa bado hakuna ushahidi dhahiri wa matokeo ya TEHAMA kwenye stadi za kisomo.

Matumizi ya TEHAMA na simu ya mkononi yanaweza kusaidia kukuza mazingira thabiti zaidi ya kisomo



KADI YA RIPOTI 2000–2015

LENGO LA 5 Usawa na ulinganifu wa kijinsia

Kukomesha tofauti za kijinsia kwenye elimu ya msingi na sekondari ifikapo 2015, na kufikia usawa wa kijinsia kwenye elimu ifikapo 2015, kwa mlengo wa kuhakikisha ushiriki kamili na sawa kwa msichana kwenye elimu ya msingi

<p><i>Alama za kimataifa/*</i></p> <p>*miongoni mwa nchi 170 zenye takwimu za shule ya msingi na 157 zenye takwimu za sekondari</p>	<p>mbali sana na lengo: 0.6% → 10%</p> <p>mbali na lengo: 21% → 35%</p> <p>karibu na lengo: 10% → 7%</p> <p>waliofikia lengo: 69% → 48%</p> <p>Shule ya msingi Shule ya sekondari</p>		
<p><i>Mafanikio</i></p> <p>✓✓</p>	<p>Tofauti za kijinsia kwenye elimu ya sekondari zinapungua</p> <p>Nchi zenye idadi ya wasichana walioandikishwa pungufu ya 90 kwa kila wavulana 100 = 30 → 19 sasa (kati ya nchi 133)</p>	<p>Dhamana ya utoaji wa haki</p> <p>40 kati ya mataifa wanachama 59 yaliyoahidi ndiyo hutekeleza haki ya elimu kwa wanawake</p>	<p>Wasichana wanaomaliza elimu ya sekondari ngazi ya chini</p> <p>2000: 81 kwa wavulana 100</p> <p>2010: 93 kwa wavulana 100</p>
<p><i>Jitihada zilizofanyika</i></p> <p>✓</p>	<p>Utetezi wa elimu ya msichana</p> <p>ngazi za kitaifa na kimataifa</p>	<p>Mipango ya utoaji posho (pesa)</p> <p>imeongeza idadi ya wasichana wanaojiandikisha kwenye baadhi ya nchi</p>	<p>Walimu wengi zaidi wa kike</p> <p>k.m. nchini Nepal</p> <p>1999: 23%</p> <p>2012: 42%</p> <p>(60% ya hawa walikuwa walimu wapya)</p>
<p><i>Changamoto zilizopo bado</i></p> <p>X</p>	<p>Ndoa na mimba za utotoni</p> <p>kwenye milengo yenye hisia za kijinsia yanahitaji kuongezwa</p>	<p>Matukio ya unyanyasaji wa kijinsia shuleni</p>	<p>Usawa wa kijinsia Ugumu katika kufafanua na kupima</p>
<p><i>Mafanikio yanayotofautiana</i></p>	<p>wasichana maskini zaidi bado wana uwezekano mdogo zaidi wa kujiandikisha</p> <p>nchini Pakistan wasichana pungufu ya 70 kwa kila wavulana 100 hawajakwenda kabisa shuleni</p>	<p>Wasichana hufanya vibaya zaid kwenye Hisabati</p> <p>na wavulana kwenye kusoma</p>	<p>Tofauti za kijinsia zinazowaathiri zaidi wavulana kwenye elimu ya sekondari huko Amerika ya Kusini na Caribbean na baadhi ya nchi maskini zaidi</p> <p>(hasa Bangladesh, Myanmar na Rwanda)</p>
<p><i>Mapendekezo kwa ajili ya kipindi kufuatia mwaka 2015</i></p>	<p>1. Ni lazima shule ziwe salama, zizingatie hisia za kijinsia, mifumo ya kufundisha na kujifunza iwawezeshe wanafunzi kukuza uhusiano chanya ya kijinsia</p> <p>2. Rasilimali lazima zielekezwe kwenye jamii ambazo tofauti za kijinsia zimeenea sana</p> <p><i>Jitihada zaidi zinahitajika</i></p>		

LENGO 5

Ulingano na usawa wa kijinsia

Tangu mwaka 2000, maendeleo kuelekea usawa wa kijinsia kwenye elimu ya msingi yamekuwa si sawa. Lengo la usawa wa kijinsia kwenye uandikishwaji elimu ya msingi mwaka 2005 halikufikiwa, huku 69% tu ya nchi zitakuwa zimefikia mwaka 2015. Kwenye elimu ya sekondari, 48% tu ya nchi ndizo zitakuwa zimefikia usawa wa kijinsia ifikapo 2015.

Usawa wa kijinsia ni mgumu zaidi kuliko ulingano wa kijinsia na ni vigumu zaidi kuupima. Inahitaji kugundua aina ya uzoefu wa wasichana na wavulana wakiwa darasani na kwenye jamii, mafanikio yao kwenye taasisi za elimu na matamano yao ya baadaye.

Maendeleo kuelekea ulingano wa kijinsia

Ukosefu wa usawa kwenye uandikishwaji wa elimu ya msingi umepunguzwa sana tangu mwaka 1999, lakini bado haujakomeshwa. Miongoni mwa nchi 161 zenye takwimu kwa mwaka 1999 na 2012, idadi kwenye usawa-iliyopimwa kwa kutumia kielelezo cha ulingano wa kijinsia (gender parity index-GPI) cha kati ya 0.97 na 1.03 – kilipanda kutoka 83 hadi 104. Idadi ya nchi zenye GPI chini ya 0.97- idadi ya wasichana walioandikishwa ni ndogo zaidi kuliko wavulana – ilipungua kutoka 73 hadi 48. Miongoni mwa nchi ambazo hazikufikia usawa kwa mwaka 2012, nyingi zilikosa usawa kwa wasichana na tisa tu zilikosa usawa kwa wavulana.

Kulikuwa na maendeleo ya kuridhisha katika kupunguza ukosefu wa usawa kijinsia kwenye uandikishwaji wa elimu ya msingi nchi za Asia ya Kusini na Magharibi, ambapo GPI iliongezeka kutoka 0.83 mwaka 1999 hadi 1.00 mwaka 2012. Ukosefu wa usawa wa kijinsia pia ulipunguzwa nchi za Dola za Kiarabu (kutoka 0.87 hadi 0.93) na nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara (kutoka 0.85 hadi 0.92) lakini bado kufikia usawa.

Maendeleo kwenye nchi ambazo wasichana walipatwa na kasoro kubwa zaidi

Tangu mwaka 1999, matokeo makubwa yamefanyika katika kupunguza pengo la jinsia kwenye

uandikishwaji wa elimu ya msingi kwenye nchi nyingi ambazo wasichana walikumbwa na kasoro mbaya zaidi. Kati ya nchi 61 zenye takwimu, nchi 33- pamoja na 20 za Afriza za Kusini mwa Jangwa la Sahara – zilikuwa na GPI chini ya 0.9 mwaka 1999; na ilipofika 2012, idadi hiyo ilishuka hadi 16.

Wasichana maskini zaidi ndio huandikishwa kwa idadi ndogo zaidi

Kwenye nchi ambazo zina idadi kubwa za watoto wenye umri wa kwenda shule ya msingi ambao hawajahudhuria kabisa shule, uwezekano wa wasichana kwenda shule ni mdogo kuliko wavulana, hususan miongoni mwa watoto maskini zaidi. Takribani 43% ya watoto walio nje ya shuleni hawatakwenda kabisa shuleni: 48% ya wasichana wanaweza wasiende kabisa shuleni, ikilinganishwa na 37% ya wavulana.

Wakiwa shuleni, wasichana hufanya vema kama wavulana

Pale wanapoandikishwa, wasichana huwa na nafasi sawa au hata nzuri zaidi, ikilinganishwa na wavulana, ya kuendelea kwenda madarasa ya juu ya shule za msingi: viwango vya ustahimilivu kwa wasichana wa darasa la 5 umekuwa sawa au wakati mwingine juu zaidi ya wavulana kwenye nchi nyingi. Kati ya nchi 68 zenye takwimu kwa miaka yote miwili, 57 mwaka 2000 walikuwa na ama viwango sawa vya ustahimilivu kwenye darasa la 5 au GPI ndogo kwa wavulana, na 58 kwa mwaka 2011.

Umaskini huzidisha ukosefu wa ulingano kwenye kumaliza elimu ya msingi

Ukosefu wa usawa wa kijinsia kwenye kumaliza elimu ya msingi mara nyingi umeonekana zaidi kwa watoto maskini zaidi kuliko wale matajiri zaidi. Nchi za Jamhuri ya Watu wa Lao, Musumbiji na Uganda, ambazo zilifikia usawa wa kijinsia kwenye elimu ya msingi kwa wasichana matajiri zaidi tangu mwaka 1999, wasichana maskini zaidi bado wako nyuma ya wavulana maskini zaidi.

Ukosefu wa ulingano wa kijinsia katika kumaliza elimu ya msingi bado umeenea sana miongoni mwa watoto maskini zaidi

Ukosefu wa ulingano wa kijinsia ni mkubwa zaidi na hubadilika zaidi kwenye elimu ya sekondari

Ukosefu wa usawa wa jinsia katika nchi nyingi huonekana zaidi kwenye elimu ya sekondari kuliko shule za misingi. Kwa mwaka 2012, 63% ya nchi zenye takwimu zilikuwa bado kufikia usawa wa jinsia kwenye uandikishwaji kwenye shule za sekondari. Uwiano wan chi zenye ukosefu wa usawa wa jinsia kwa wavulana na wasichana zilikuwa sawa zikiwa na takribani 32% kila moja. Nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia ya Kusini na Magharibi, wasichana waliendelea kuwa wachache zaidi kwenye uandikishwaji wa sekondari. Nchi za Amerika ya Kusini na Caribbean, zilikuwa tofauti, ni wavulana 93 tu ndio

Huko Amerika ya Kusini na Caribbean, ni wavulana 93 tu ndio wameandikishwa kwa kila wasichana 100


waliandikishwa kwa kila wasichana 100, kiwango ambacho ni sawa na cha mwaka 1999.

Kukuza mazingira wezeshi

Utetezi endelevu wa dunia kwa miaka ya hivi karibuni umesababisha usaidizi usio wa kawaida wa serikali na asasi za kiraia kwenye usawa wa jinsia na usawa kwenye elimu. Serikali zimepitisha marekebisho ya sheria na sera; zikitilia mkazo zaidi jinsia kwenye mifumo ya elimu ya kitaasisi, mipango na bajeti; na zilitoa msaada mkubwa sana kwenye jamii nyingi.

Ujumuishi wa masuala ya jinsia na uandaaji wa bajeti hutoa mlengo

Ujumuishi wa masuala ya jinsia hulenga kufanya usawa wa kijinsia kuwa wazo kuu kwenye miundo na



Credit: Darryl Evans/Agence VU

utendaji kazi wa taasisi na mashirika kwa ujumla kuliko kuachwa kuwa suala linalojitemegea ama sekta. Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo kwa Wanawake (UN Development Fund for Women), sasa UN Women, huhamasisha uandaji bajeti wenye kuzingatia masuala ya jinsia kwenye nchi zaidi ya 60 duniani kote. Hata hivyo, nchi nyingi bado hazina rasilimali za kutosha kutekeleza badiliko hilo, vitengo vya jinsia kwenye taasisi nyingi havipewi umuhimu unaostahili, msaada kwenye utetezi hautoshi na utekelezaji wake huathiriwa na ubaguzi uliokomaa.

Mabadiliko ya sheria na sera huimarisha maendeleo

Kwenye muhtasari wa UNESCO uliotolewa hivi karibuni, nchi wanachama 40 kati ya 59 hutaja kutoa hakikisho la kuwapa wasichana na wanawake haki ya elimu au kupiga marufuku ubaguzi wa jinsia kwenye katiba zao, sheria au sera. Hata hivyo, taasisi za kijamii huendelea kudhoofisha usawa wa jinsia. Sheria au vitendo za/vya kibaguzi za urithi bado zipo/vipo, na matukio ya ndoa za mapema bado ni mengi mno.

Kuongeza uhitaji na kuunga mkono haki za elimu

Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na asasi za kiraia zimejitahidi kuondoa viziwi vya kiuchumi na kijamii kwenye kusoma na kupunguza mapengo ya kijinsia kwa njia kuu tatu: kuhamasisha maadili na mitazamo chanya kwenye elimu ya wasichana kupitia kampeni za kuhamasisha jamii na utetezi; kuchochea ufutwaji wa gharama za shule; na kuzikabili ipasavyo ndoa na mimba za utotoni.

Kubadilisha mitazamo na kuhamasisha misaada kwa ajili ya elimu ya wasichana

Kampeni za kitaifa zimetumika kama sehemu ya mifumo mipana ya sera ili kubadilisha mitazamo ya wazazi/walezi na kujenga misingi katika kusaidia elimu ya wasichana. Kampeni ambazo zimefanikiwa huhusisha wabia kutoka sekta mbalimbali, huungwa mkono na mipango na sera za kitaifa, na moja kwa moja huhusisha mashirika na jamii zile za mashinani kabisa.

Kupunguza gharama za elimu

Gharama zinazohusiana na shule zinaweza kuwaathiri wasichana kwa namna isiyolingana. Ufutwaji wa ada na utoaji wa ufadhili wa masomo vinaweza kupunguza gharama za moja kwa moja za masomo, na posho za pesha zinaweza kuzipunguzia familia gharama zisizo za moja kwa moja. Hata hivyo, masuala ya usawa bado yanatia hofu. Nchini Bangladesh, kwa mfano, pamoja na mafanikio yaliyotajwa kwenye programu ya kutoa posho kwa wasichana wa vijijini wanaosoma shule za sekondari, wasichana kutoka familia tajiri zaidi na kaya zinazomiliki ardhi, walinafaika kwa namna isiyowiana.

Ndoa za mapema na mimba za utotoni

Kuingia kwenye ndoa mapema na ndoa za utotoni huwazuia wasichana kuendelea na masomo, lakini maendeleo kuelekea ukomeshaji wa dunia wa ndoa za utotoni yamekuwa si ya kuridhisha. Takwimu kwa 2000-2001 zilionyesha kwamba kwenye nchi 41, asilimia 30 au zaidi ya wanawake wenye umri kati ya 20 na 24 waliolewa wakiwa na umri wa miaka 18. Sheria peke yake inaweza isuzuie kabisa matendo haya. Thathmini ya Sheria ya Ndoa ya 1974 nchini Indonesia iaonyesha kuwa sheria hiyo haikuleta tofauti yeyote kwenye mwelekeo wa ndoa za utotoni. Matukio ya ndoa za utotoni yamekuwa yakipungua kwa kasi kwenye baadhi ya nchi, hata hivyo, nchini Ethiopia, kwa mfano, matukio ya ndoa za utotoni yalipungua kwa zaidi ya 20% kati ya 2005 na 2011 kutokana mabadiliko kwenye sheria, kampeni za utetezi na zile za kijamii.

Kupanua na kuboresha miundombinu ya shule

Malengo ya usawa na uwiano wa jinsia yamekuwa ama ni moja kwa moja au si moja kwa moja yakisaidiwa na sera ili kuongeza upatinaji na usawa wa miundombinu ya shule/ elimu. Kuongeza kwa ugavi mashuleni, ikiwa ni pamoja na shule za wasichana, na kuboresha hudumashuleni – hususani huduma za maji na usafi (vyoo, maji machafu na takataka) – vinaweza kuboresha mahudhurio ya wasichana.

Kupunguza umbali wa kwenda shule

Ujenzi wa shule kwenye jamii zilizotengwa (zenye uhaba) umesaidia kushinda viziwi kwenye elimu ya wasichana vinavyohusiana na umbali. Jimbo la Ghor nchini Afghanistan, kwenye vijiji ambavyo vilichanguliwa kiholela kujengewa shule za msingi, uandikishwaji uongezeka kwa 42% na uandikishwaji wa wasichana 17% zaidi ya ule wa wasichana, na hivyo kufuta pengo la kijinsia.

Kuboresha huduma za maji na usafi

Utoaji wa huduma salama na zilizotengwa kwa wasichana ni mkakati mhimu katika kuboresha mahudhurio ya wasichana shuleni na kukuza mazingira yenye usawa zaidi shuleni. Huduma za maji na usafi kwenye nchi nyingi zinazoendelea zimeimarika kwa zaidi ya muongo mmoja, lakini maendeleo hayo yamekuwa ya polepole: kati ya nchi 126 zenye takwimu, wastani wa asilimia kwa shule za msingi zenye huduma bora za usafi uliongezeka kutoka 59% mwaka 2008 hadi 68% mwaka 2012.

Ujenzi wa shule na kuboresha miundombinu ya shule kunaweza kuboresha mahudhurio ya wasichana

Sera za elimu za nchi zina-zoendelea mara nyingi hupuuzwa uandikishwaji wa wavulana na uwekano wa kumaliza

Sera za kuboresha ushiriki wa wavulana pia zinahitajika

Wakati uwezekano wa wasichana kuanza shule ni wa chini kuliko wavulana, wavulana kwenye nchi nyingi wako kwenye hatari zaidi kushindwa kuendelea na kumaliza mzunguko wa elimu. Viwango vya wale wanaoacha shule miongoni mwa wavulana vina athari kubwa zaidi kwa mahusiano (uwiano wa) ya kijinsia. Utafiti wa 2009 na 2010 huko Brazil, Chile, Croatia, India, Mexico na Rwanda ulibainisha kwamba wanaume wenye elimu ndogo zaidi waliotoa mitazamo yao kuhusu ubaguzi wa kijinsia, walionekana kuwa na vurugu zaidi nyumbani na, kama walikuwa na watoto, uwezekano wa kujihusisha na malezi ya mtoto ulikuwa mdogo zaidi.

Sababu kadhaa zinazochangia uwezekano wa wavulana kuacha shule

Idadi kubwa ya wavulana huacha shule mapema kwa sababu ya umaskini na kutakiwa au kupenda kufanya kazi, pamoja na kuchelewa kuanza, kupata alama mbaya darasani na kukosa ari ya kusoma, pamoja na sababu nyingine kama mila za kabila na aina nyingine za kutengwa.

Sera zinazoangazia tatizo la wavulana kuacha shule ni chache

Sera za elimu za nchi zinazoendelea mara nyingi haziangazii uboreshwaji wa uandikishwaji wa wavulana shuleni na jinsi wanavyomaliza elimu yao, hata kwenye nchi zenye viwango vya juu vya ukosefu wa usawa kwa

wavulana. Nchi za Caribbean wamekuwa watekelezaji wazuri wa mbinu shirikishi na uingiliaji kati kama vile ushauri, utoaji wa nafasi ya pili, makongamano ya mafunzo na ya kijamii yenye lengo la kutoa suluhisho la tatizo la watoto kuacha shule.

Mazingira sawa shuleni na darasani


Usawa wakijinsia kwenye elimu si tu huhitaji usawa kwenye upatikanaji, lakini pia usawa kwenye mchakato wa kujifunza, matokeo ya kielimu na matokeo ya nje (ya elimu). Zipo sababu nne za msingi katika kuboresha ubora wa elimu, hususani kwa wasichana: kuongeza idadi na ubora wa walimu, kuondoa upendeleo wa kijinsia kwenye mitaala na vitabu vya kufundisha; kufanya vitendo vya darasani vizingatie zaidi jinsia kupitia mafunzo, na kudhibiti vurugu zenye mwelekeo wa kijinsia.

Kuajiri walimu wa kike

Uwepo wa walimu wa kike unaweza ukapunguza hofu ya usalama kwa wazazi na kuongeza mahitaji ya elimu kwa wasichana, hususani kwenye nchi ambazo bado zina vikwazo vya kitamaduni na kijamii kwenye uandikishwaji wa wasichana. Kwa ngazi ya dunia, idadi ya wanawake wanaofundisha shule za msingi imeongezeka tangu mwaka 1999, kutoka 58% hadi 63% mwaka 2012. Kwenye elimu ya sekondari, wastani wa dunia unabaki kuwa 52%. Hata pale ambapo walimu wanawake ni wengi zaidi; kiuwiano, wanawake wanaopanda kwenye nafasi za uongozi ni wachache kuliko wanaume.

Kielelezo cha 8: Tangu 1999, idadi ya walimu wa kike imeongezeka, na ndio wenye idadi kubwa zaidi ya walimu wapya kwenye nchi kadhaa

Asilimia ya walimu wa kike kwenye elimu ya msingi, 1999 na 2012; asilimia ya walimu wa kike kama walimu wapya 2009-2012



Mafunzo ya uzingatiaji wa jinsia katika vitendo darasani

Mitazamo ya walimu, vitendo na matarajio ya wavulana na wasichana darasani vinaweza kukuza ubaguzi wa kijinsia na kuathiri shauku, ushiriki (kwa wasichana na wavulana) na matokeo ya elimu. Kwenye mifumo mingi, uchunguzi wa darasani unaonyesha walimu wa jinsia zote mbili wakiwasiliana zaidi na wavulana, na hivyo kuwafanya wasichana waendeleo kuwa watazamaji tu. Elimu ya mwalimu kuhusu ushirikishwaji, mbinu za ufundishaji zenye kuzingatia hisia za kijinsia na udhibiti wa darasa vinaweza kupunguza upendeleo na kujenga mazingira ya shule yenye kufaa zaidi. Hata pale ambapo sera zipo, hata hivyo, kukosekana kwa mikakati iliyo wazi, utekelezaji na usimamizi mbovu, na tathmini duni mara nyingi huzuia ufanisi wa sera hizo.

Mageuzi ya mitaala na vitabu ili kukuza usawa wa kijinsia

Licha ya jitihada za kuongeza ulinganifu wa kijinsia, upendeleo kwenye vitabu bado umeenea kwenye nchi nyingi, sababu mojawapo ni kukosekana kwa utashi wa kisiasa na ufadhili kwenye jamii iliyo pana zaidi. Mitaala inayozingatia jinsia ina nguvu ya kusaidia ukuaji wa elimu na kukuza mahusiano chanya ya kijinsia. Elimu ya kina ya jinsia ni eneo muhimu kwenye mtaala linaloweza kukuza usawa wa kijinsia, lakini programu za elimu ya jinsia zinaweza zisiweze kupambana na mienendo ya kijinsia inayoambatana na afya ya uzazi.

Kukabili unyanyasaji wa kijinsia shuleni

Unyanyasaji wa kijinsia kwenye mifumo ya shule umeenea kote. Mara nyingi wavulana hujihusisha kwenye vurugu za kimwili, huku wasichana wao hupatwa mara kwa mara na manyanyaso na maonevu ya kijinsia, zinazosababishwa na wanafunzi na walimu wa kiume. Uonevu wa kibaguzi (unaohamasishwa na tofauti za kijinsia) na uonevu wa kimtandao ni maeneo yanayoleta hofu. Nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara zimekuwa mbele kutengeneza sera zitakazokabili unyanyasaji wa kijinsia shuleni, hususani vurugu za kingono/ kijinsia. Klabu na programu za wasichana zinazohamasisha amani miongoni mwa wavulana na wasichana zimeonyesha mabadiliko chanya ya mitazamo. Lakini kiujumla, kuna ushahidi mdogo ya kwamba kuongezeka kwa ufahamu wa matukio ya unyanyasaji wa kijinsia shuleni kunapelekea uchukuaji wa hatua madhubuti za kukomesha unyanyasaji huo.

Kusaidia usawa katika matokeo ya kujifunza

Kufikia usawa wa kijinsia kwenye elimu si tu huhitaji kupunguza ukosefu wa usawa kwenye fursa za elimu, lakini pia kwenye matokeo yake. Tathmini za elimu za kikanda na kimataifa zinaonyesha kwamba kwenye nchi nyingi wasichana hufanya vema zaidi kwenye kusoma na wavulana kwenye hisabati, ingawa pengo kwenye hisabati linapungua. Matokeo kwenye sayansi yana tofauti nyingi zaidi, huku kukiwa hakuna tofauti kubwa kati ya wavulana na wasichana kwenye nchi nyingi.

Kwenye mazingira duni zaidi, mafanikio ya wasichana bado ni magumu

Kwenye baadhi ya nchi maskini zaidi, ambapo wasichana wana historia ya kukumbana na vikwazo kwenye ushiriki sawa wa elimu, bado wanaendelea kukabiliwa na kasoro kwenye upatikanaji wa stadi muhimu za msingi. Kwenye maeneo ya vijijini nchini Pakistan, mapengo ya kijinsia ni madogo kwa wanafunzi wa darasa la 5, wakati mwingine hupendelea wasichana zaidi. Hata hivyo, pale ambapo wasichana walio nje ya shule hawazingatiwi, matokeo ya wasichana ni mabaya zaidi kwa watoto wenye umri wa miaka 10 hadi 12, hususani kwenye majimbo na wilaya masikini zaidi.

Kupambana na mafanikio duni ya wavulana

Hofu kuhusu mafanikio duni ya wavulana kwenye matokeo ya elimu, hasa kwenye kusoma, imeongezeka tangu mwaka 2000. Lakini ni nchi chache tu ndizo zina mifumo mipana ya sera katika kuikabili hofu hii. Mikakati na uingiliaji kati mdogo kwenye kufundisha na kujifunza ambayo inaweza kukabili mafanikio duni ya wavulana huhusisha mkazo kwenye stadi zinazohawilishika, mbinu za darasani zinazoendeleza kujifunza kwa vitendo, na shule zenye kuhamasisha heshima na ushirikiano.

Uwakilishi wa wanawake kwenye ualimu hupungua kadiri ngazi ya elimu inavyopanda

KADI YA RIPOTI 2000–2015

LENGO 6 Ubora wa Elimu

Kuboresha nyanja zote za ubora wa elimu na kuhakikisha matokeo na vipimo vya elimu inayotolewa vinafikiwa na wote, hasa kisomo na stadi muhimu za maisha

<p><i>Alama za kimataifa*</i></p> <p>*kati ya nchi zenye takwimu</p>	<p>Uwiano wa mwanafunzi na mwalimu ngazi ya msingi</p> <p>*wastani</p>	<p>Uwiano wa mwanafunzi na mwalimu aliyefunzwa ngazi ya msingi</p> <p>*wastani</p>
<p><i>Mafanikio</i></p> <p>✓✓</p>	<p>Upatikanaji na kujifunza hakuna kubadilishana</p> <p>k.m. Kenya</p> <p>42% 2000, 62% 2007</p> <p>watoto wanaomaliza elimu ya msingi</p> <p>watoto wanaofikia kiwango cha chini zaidi kwenye hisabati</p> <p>Uwiano wa mwalimu/mwanafunzi</p> <p>Katika elimu ya msingi uwiano wa mwanafunzi/mwalimu ulishuka kwenye nchi 121 kati ya 146</p> <p>Kongo na Mali zilipun uwiano wa mwanafunzi/mwalimu kwa wanafunzi 10 kwa mwalimu, huku uandikishwaji ukiongezeka maradufu</p>	
<p><i>Jithada zilizofanyika</i></p> <p>✓</p> <p><i>Changamoto zilizopo bado</i></p> <p>X</p>	<p>Tathmini za kitaifa za kupima mafanikio ya elimu</p> <p>283 1990-1999, 1,157 2000-2013</p> <p>Uhaba wa walimu waliofunzwa mwaka 2012, kwenye moja ya tatu ya nchi</p> <p>chini ya walimu wa msingi 75% walipata mafunzo</p>	<p>Programu za hifadhi za kijamii</p> <p>nchini Mexico, kwa watoto na watu wazima, ambazo programu zilielekezwa kwa familia maskini, zilisaidia kuboresha matokeo ya elimu</p> <p>Sera za kuboresha mafunzo ya walimu nchini Nepal zilisaidia kupunguza uwiano wa mwanafunzi/mwalimu kwenye shule za msingi</p> <p>Uhaba wa vifaa/ nyenzo</p> <p>Ufungufu wa kujifunza huanza mapema</p> <p>Uhaba wa kiada na zana za kufundishia, pamoja na samani za darasani</p>
<p><i>Mafanikio yanayotofautiana</i></p>	<p>Walimu waliofunzwa</p> <p>Chini ya 50%</p> <p>nchini Angola, Benin, Equatorial Guinea, Guinea-Bissau, Senegal na South Sudan</p>	<p>Elimu kwa lugha nyingi</p> <p>unahitaji kuwa endelevu ili kuboresha elimu</p> <p>Mapengo baina ya mijini-vijijini</p> <p>yamepungua kwenye nchi 8 za Amerika ya Kusini, lakini 6 bado ziko nyuma kwenye elimu</p>
<p><i>Mapendekezo kwa baada ya mwaka 2015</i></p>	<ol style="list-style-type: none"> 1. Wanahitajika Walimu wengi zaidi waliofunzwa, zana bora za kufundishia na mitaala inayofaa 2. Tathmini za elimu zinahitajika ili kusaidia utoaji wa elimu bora na matokeo yenye usawa <p><i>Jithada zaidi zinahitajika</i></p>	

LENGO 6 Ubona wa Elimu

Kuboresha vipengele vyote vya ubora wa elimu na kuhakikisha ubora wa vyote ili kwamba matokeo ya elimu yaliyotambuliwa na kupimwa yanafikiwa na wote, hasa kwenye kisomo na stadi muhimu za maisha

Wakati nchi nyingi zimekuwa na mafanikio ya kuvutia kwenye upatikanaji wa elimu tangu Dakar, kuimarika kwa ubora si mara zote umeshika kasi. Mabadiliko makubwa kwenye utiliaji mkazo kuelekea ubora na elimu yanaelekea kuwa ya kati zaidi kwenye mfumo wa dunia wa baada ya 2015, kwani, kama Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji ilivyoonesha, watoto 250 milioni hawakuwa wamepata nafasi ya kujifunza mambo ya msingi-ingawa 130 milioni miongoni mwao wamekuwa shuleni angalau kwa miaka minne.

Inawezekana kuboresha upatikanaji sanjari na usawa kwenye elimu

Kadiri uandikishwaji unavyoongezeka, watoto wanaoingia kwenye mifumo ya shule wana uwezekano mkubwa kutoka kwenye makundi ya pembezoni, yenye ulemavu au wale walioathiriwa na utapiamlo na umaskini. Wanafunzi wapya pia wana uwezekano wa kutoka kaya zenye wazazi wenye kisomo cha chini au pale inapozungumzwa lugha isiyo rasmi. Athari za mambo haya zingebashiri ongezeko la uandikishwaji kwenye ngazi za chini zaidi za elimu. Lakini matokeo kutoka tathmini nyingi zaidi za elimu za kikanda na kimataifa haziaksi hili.

Kwenye baadhi ya nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara, idadi ya watoto wanaoanza na kumaliza shule ilipanda kati ya mwaka 2000 na 2007. Wakati huo huo, matokeo ya elimu ama yaliboreshwa au yalibaki yalivyokuwa. Kwenye elimu ya sekondari, vivyo hivyo, upatikanaji na usawa Uunaweza kuongezeka bega kwa bega. Nchini Mexico, uandikishaji wa watoto wenye miaka 15 uliongezeka kwa takribani 12% kati ya 2003 na 2012 huku wastani wa alama kwenye hisabati kwenye Programu ya OECD ya kutathmini wanafunzi wa kimataifa (PISA) uliongezeka kutoka pointi 385 hadi 413.

Maendeleo ya matokeo ya kujifunza ni lazima yafuatiliwe

Mikakati madhubuti katika kutathmini na kufuatilia maarifa na stadi huhitaji tathmini kubwa za elimu kulingana na sampuli za tafiti ambazo hutoa taarifa za nchi nzima kuhusu matokeo ya elimu. Tathmini nyingi zaidi za kitaifa zimekuwa zikifanyika tangu Dakar: kutoka 283 mwaka 1990-99 hadi 1,167 mwaka 2000-13. Kiwango cha kufanya tathmini si tu kiliongezeka miongoni mwa nchi tajiri zaidi pekee, lakini pia kiliongezeka miongoni mwa nchi maskini.

Tathmini nyingi za kitaifa hutoa wito kwa mamlaka za elimu kuboresha viwango vya maarifa na umahiri wa mwanafunzi. Mapitio ya tafiti 54 yanaonyesha kuwa uwigo wa sera za elimu zitokanazo na takwimu za kitaifa ni mpana, kuanzia kwenye mageuzi ya mtaala na mapitio ya vitabu vya kiada hadi elimu ya ualimu na mafunzo yanayoendelea, maendeleo ya zana za mafunzo, ushiriki wa wazazi, viwango vya utendaji na mgawanyo wa rasilimali katika kusaidia shule zenye matokeo hafifu.

Tathmini zinazoongozwa na raia zimepiga hatua

Mashirika ya Vyama vya kiraia yanazidi kushiriki kwenye shughuli za tathmini na kuchangia kuboresha sera za taifa za elimu. Tathmini kuhusu stadi a kusoma na kuandika na kuhesabu zilozingatia kaya ziliongozwa na raia zilianzia India mwaka 2005 na zimetumiwa pia Pakistan (tangu 2008), Kenya, Uganda, na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2009), Mali (2011) na Senegal (2012). Kwa pamoja, nchi hizi zilifikia zaidi ya watoto milioni 1 mwaka 2012.

Kumekuwa na tathmini zaidi ya 1000 za kitaifa zilizofanywa tangu mwongozo wa Dakar

Tathmini hutumika kupima mafunzo kwa madarasa ya awali

Kati ya 2007 na 2014, zaidi ya nchi 60 zilifanya tathmini moja au zaidi ya uwezo wa kusoma kwenye madarasa ya awali (EGRAs). Hadi katikati ya mwa 2014, zaidi ya nchi 20 zilikuwa zimefanya tathmini ya hisabati kwenye madarasa ya awali (EGMAS). Matokeo yanaashiria hatari: watoto wengi hutumia miaka miwili au mitatu shuleni pasipo kujifunza kusoma neno moja, na shule nyingi hazifundishi wanafunzi wake hesabu za msingi kwenye miaka yao ya awali. Matokeo ya EGRA/EGMA yamesababisha serikali na wafadhili kufikiri kwa upya juu ya sera ili kwamba wanafunzi wafkie angalau viwango vile vya chini kabisa kwenye kusoma na hisabati.

Tathmini za kikanda na kimataifa huchangia upimaji wa usawa katika kujifunza

Pamoja na ongezeko la matumizi ya tathmini za kitaifa, nchi nyingi zimeendelea kuunganisha ulinganishi wa mafanikio ya mwanafunzi baina ya nchi na nchi, na baina ya mfumo na mfumo. Tafti za Amerika ya Kusini PERCE, SERCE na TERCE huruhusu tathmini ya vipengele vinavyohusiana na ustadi wa kitaaluma wa wanafunzi- kulingana na mazingira y a utaratibu , mitaala na familia-na wa maendeleo ya jumla ya kitaifa, ikiwa ni pamoja na kupunguza ukosefu wa usawa. Programu ya OECD ya PISA hukusanya taarifa za watoto wenye umri wa miaka 15 ambazo huwezesha kuhusisha ukosefu wa usawa kwenye asili ya kijamii na stadi za kusoma , kuandika na kuhesabu.

Nchi nyingi za OECD zimeanzisha uboreshaji wa sera na mipango ikiwa ni majibu ya moja kwa moja kwa matokeo ya PISA. Tathmini za elimu pia zimeathiri mitaala na ubora wa mafunzo kwenye nchi nyingi. Hata hivyo, Tathmini za kikanda na kimataifa zinaweza kuleta matatizo. Kuchapisha milingano kunaweza kukatisha tamaa ya ushiriki wa nchi maskini zaidi ambako ni wanafunzi wachache tu ndio hujifunza mambo ya msingi. Baadhi ya nchi zimebadilisha maudhui yaliyokusudiwa ya masomo yanayohitajika na kuimarisha ubora wa mitaala uliopimwa kwenye PISA.

Kuwekeza katika ualimu ni lazima

Mwongozo wa Dakar ulisitiza kwamba, ili kufikia ELIMU KWA WOTE, serikali zinahitaji kuboresha upatikanaji na upangaji wa walimu wenye ujuzi na hamasa. Ili kuvutia na kuajiri walimu wazuri, watunga sera wanahitaji kuboresha elimu ya ualimu , kuwapanga walimu vizuri zaidi, kutoa vivutio kwa kuwapa mishahara sahihi, na kutengeza mifumo inayovutia kukua kitaaluma.


1. Kwa kufuata mtiririko huo, utafiti wa kwanza linganishi na fafanuzi wa kikanda , wa pili na wa tatu uliofanywa na Maabara ya Amerika ya Kusini kwa ajili ya Tathmini wa Ubora wa Elimu

Pamoja na maendeleo, upungufu w walimu bado ni tatizo kubwa

Tofauti kwenye uwiano wa wanafunzi/mwalimu katika kanda imebaki kuwa kubwa. Kwa mwaka 2015, nchi 29 kati ya 161 zenye takwimu, uwiano wa mwanafunzi/mwalimu kwenye elimu ya msingi ulizidi 40:1. Miongoni mwa nchi hizi, 24 ni za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Uwiano wa Mwanafunzi wa shule ya msingi/mwalimu ulishuka kwenye nchi 121 kati ya 146 zenye takwimu kwa mwaka 1999 na 2012. Marekebisho mengi yalifanywa na nchi ambazo tayari zilikuwa na uwiano wa mwanafunzi/mwalimu ulio chini ya 40:1. Kwenye sekondari za chini, ambapo nchi 105 zilizokuwa na takwimu kwa mwaka 2012, 18 zilikuwa na uwiano juu ya 30:1. Kati ya 1999 na 2012, uwiano uliongezeka na kuwa wanafunzi 6 kwa mwalimu mmoja nchini Ethiopia, Gambia, Guinea, Mali na Myanmar. Uwiano wa mwanafunzi wa sekondari ya juu/mwalimu haukubadilika au ulishuka kwenye nchi nyingi zenye takwimu kwa miaka kumi iliyopita.

Kielelezo 9: Tofauti ya uwiano wa mwanafunzi/mwalimu kwenye kanda nyingi umebaki kuwa mkubwa

Uwiano wa mwanafunzi/mwalimu, dunia na kanda zilizochanguliwa, 1990-2012



Ni walimu wangepi wa shule za msingi walihitajika ili kufikia lengo la elimu kwa wote ifikapo mwaka 2015?

Kati ya 2012 na 2015, walimu milioni 4 wangekuwa wamehitajika kufikia ELIMU YA MSINGI KWA WOTE: 2.6 milioni kuchukua nafasi za walimu waliostaafu, waliobadilisha kazi, waliokufa au kuaacha kazi kwa ugonjwa, na 1.4 milioni kuziba mapungufu, kukabiliana na ongezeko la uandikishwaji na kudumisha uwiano wa mwanafunzi/mwanafunzi kuwa chini ya 40:1. Baadhi ya kanda na nchi zingekuwa zimehitaji walimu wa ziada kwa

Dunia ina upungufu wa walimu milioni 4 ili kuwaingiza watoto wote shuleni ifikapo 2015

shule za msingi kuliko nyingine. Hii ni changamoto kubwa kwa kanda, hasa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambazo zilikuwa na uhitaji wa 63% ya walimu wa ziada waliohitajika. Miongoni mwa nchi 93 zilizokuwa zinahitaji walimu wa ziada, nchi 29 tu ndizo zilizokuwa na mwelekeo wa kufanikisha hilo ifikapo mwaka 2015, nchi 64 zikibaki na upungufu.

Walimu waliopata mafunzo: Upungufu mkubwa zaidi.

Kuongeza idadi ya walimu haitakuwa suluhu ya kutosha; ubora wa elimu unahitaji kuongezwa, pamoja na walimu wenye mafunzo na waliohamasika. Nchi nyingi zimeajiri idadi kubwa ya walimu ambao hawana sifa. Miongoni mwa nchi 91 zenye takwimu mwaka 2012, asilimia ya walimu wa shule za msingi ambao mafunzo yao yalikitidhi viwango vya kitaifa ilikuwa kati ya 39% Guinea-Bissau hadi zaidi ya 95% katika nchi 31. Makadirio yaliyofanyika kwa nchi 46 yalionyesha kwamba 12 kati yake zingekuwa na chini ya 75% ya nguvukazi ya walimu wenye mafunzo yanayokidhi viwango vya kitaifa kwa mwaka 2015.

Mapengo ya usawa kwenye upangaji wa walimu yanahitaji kushughulikiwa

Jumla ya idadi ya walimu na wastani wa uwiano wa wanafunzi na walimu inaweza kuficha mgawanyo usio sawa wa walimu kwenye nchi, na kuibua wasiwasi wa usawa. Kwa ujumla kuna pengo linaloonekana kuwepo kati ya serikali na wahudumu wasio wa serikali. Katika nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikijumuisha Kongo, Rwanda, na Uganda uwiano wa wanafunzi na walimu kwa shule za msingi za umma unazidi ule wa shule za binafsi kwa wanafunzi 30 au zaidi. Wanafunzi wanaosoma shule za kimaskini wanafundishwa na walimu ambao hawajaandaliwa vema kuliko shule tajiri zaidi. Zaidi ya mwongo mmoja uliopita, serikali zimejitahidi kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu kwa namna mbalimbali, ikiwa ni pamoja na, upangaji wa walimu kufanyika makao makuu, vivutio kama vile nyumba za walimu, maslahi ya kifedha na kuwapandisha madaraja kwa mserekeru, na kuajiri walimu wenyeji.

Matumizi ya walimu wa mikataba yanaongezeka, lakini pia yanatia wasiwasi.

Katika kukabiliana na uhitaji wa walimu zaidi kutokana na ongezeko la uandikishwaji, serikali za nchi nyingi ziliamua kuajiri walimu wengi wa mikataba. Mwishoni mwa mwaka 2000, baadhi ya nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na walimu wengi wa mikataba mifupi kuliko walimu watumishi wa umma. Walimu wa mikataba hukabiliwa na mazingira duni ya kufanyia kazi, usalama mdogo wa kazi na mishahara duni kuliko wenzao wenye ajira ya kudumu. Kwa sehemu kubwa hawana kabisa mafunzo au wana

mafunzo ya chini ya mwezi mmoja. Je, walimu hawa wanaweza kuwa na ufanisi kama walimu watumishi wa umma? Nchi za Niger na Togo, walimu wa mikataba kwa ujumla wamekuwa na matokeo hasi au yaliyochanganyika kwenye mafanikio ya mafunzo ya lugha ya Kifaransa na hisabati darasa la 5, ingawa nchini Mali wamekuwa na matokeo chanya. Walimu wa mikataba huonekana kuwa na ufanisi zaidi pale ushiriki wa jamii au wazazi unapokuwa na nguvu.

Mafanikio ya kufundisha na kujifunza yana uhusiano na rasilimali zilizopo.

Kuna mambo matatu yanayochangia ubora kwenye kufundisha na kujifunza; ugavi, usambazaji na matumizi ya zana za kujifunzia; eneo salama, linalofikika na lenye huduma zinazofaa; na muda unaotumika darasani.

Kuendeleza matumizi ya zana bora za kufundishia na kujifunzia.

Kazi muhimu ya vitabu vya kiada katika kuboresha mafanikio ya wanafunzi imechangia kuinua sera za elimu, na kuna ushahidi mkubwa wa kuthibitisha hili. Mifumo ya manunuzi na usambazaji unaofanywa na serikali kuu inazidi kubadilishwa na kupelekwa kwa wadau wa sekta binafsi. Jamii ya kimataifa inafanya kazi muhimu sana ya kusaidia kutengeneza na kusambaza vitabu kwa ajili ya nchi nyingi zinazoendelea. Uboreshaji wa vitabu vya kiada ni jambo muhimu ili kuendana na maendeleo ya karibu zaidi kwenye elimu na maeneo ya masomo.

Kuhamasisha mazingira rafiki kwa mtoto awapo shuleni.

Watoto wengi wanasoma katika mazingira ambayo si mazuri kujifunzia- wanakosa maji ya bomba, vifaa safi na salama vya kunawia mikono, na vyoo safi. Watoto pia wanaweza kukumbana na ubaguzi, unyanyasaji na hata vurugu. Kwa miaka 15 iliyopita, nchi kadhaa zimetumia mfumo wa shule ulio rafiki kwa mtoto, lakini tathmini ya mazingira rafiki ya mtoto shuleni katika nchi za Guyana, Nicaragua, Nigeria, Ufilipino, Afrika Kusini, na Thailand ilianisha changamoto za kiutekelezaji. Miundombinu duni, ukosefu wa m matengenezo na ukosefu wa mafunzo yanayofaa kwa wakuu wa shule na walimu, ndio matatizo makubwa.

Kutumia muda vizuri darasani.

Kuongeza muda wa kufundisha imeonekana kunaweza kuboresha ufahamu wa wanafunzi na kuleta matokeo yenye tija. Mashirika ya kimataifa yamependekea kwamba wanafunzi wa shule ya msingi wajifunze kati ya masaa 850 na 1000 kwa mwaka, lakini wastani wa muda ulioelekezwa kwa vipindi vya darasani kwa shule za msingi na sekondari ya chini duniani kote umepungua kwa mwongo uliopita na kufikia chini ya masaa 1,000. Katika nchi nyingi, hususan kwenye jamii

Mgawanyo usio sawa wa walimu ndani ya nchi huchochea ukosefu wa usawa

maskini, shule za kutwa zinakabiliwa na tatitizo la walimu watoro, walimu kuchelewa kuajiriwa, mafunzo kazini kwa walimu, migomo na vita.

Michakato ya kufundishia na kujifunza ni muhimu

Vipengele vinne vya kufundishia na kujifunza vinachangia upatikanaji wa elimu bora: mtaala husika na jumuishi mwelekeo wa ufundishaji ufaao na ulio mwafaka, matumizi ya lugha- mama, na matumizi ya teknolojia ifaayo.

Kuandaa mtaala stahiki

Msukumo unaoongezeka wa kuboresha ushindani wa kiuchumi, umesababisha serikali ziboreshe mitaala yake kwa namna nyingi, huku msisitizo mkubwa ukiwa kwenye umahiri na si kwenye maarifa yaliyomo. Kumekuwa pia na msukumo wa kufanya maudhui yaendane na mahitaji ya wakati husika ya watu na jamii. Kwa baadhi ya maeneo, walimu hawakuhusishwa kwenye uandaaji wa mitaala, wakaachwa wakiwa

wamepoteza imani na mfumo wa juu-chini. Hivyo, walikosa uelewa wa madhumuni ya mabadiliko, na mabadiliko hayo yalikosa msingi wa uhalisia wa mazingira ya darasani.

Matumizi ya mikakati madhubuti ya kufundishia

Kwa kipindi cha mwongo mmoja uliopita kumekuwa na mabadiliko kutoka kwenye kumtegemea mwalimu hadi kufikia njia shirikishi. Lakini utekelezaji wake unaweza kuwa mgumu. Changamoto zake ni pamoja na kukosa mazingira rafiki, mafunzo kwa walimu na maandalizi, vitabu na vifaa vya kufundishia, na madarasa makubwa kupita kiasi. Walimu wamekuwa wakifundisha kwa kadiri walivyofundishwa, pasipo msaada madhubuti na endelevu. Hata hivyo, kwa kutumia mbinu mpya za kufundishia kwa mazingira ya ndani, walimu wanaweza kutengeneza mazingira yanayomlenga mwanafunzi, hata katika mazingira mabovu

Muktadha unaomlenga mwanafunzi unaweza kutengenezwa kwa kurekebisha mbinu za mwalimu na kuzifanya ziendane na muktadha husika



Credit: Poulomi Basu

Kuhamia kwenye sera ya matumizi ya lugha nyingi

Lugha ya kufundishia shuleni ni muhimu sana katika kukuza ubora wa kufundisha na kujifunza. Katika nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia ya Kusini Mashariki, kumekuwa na mlolongo wa matumizi makubwa ya lugha za kienyeji. Nchi za Amerika ya Kusini zina sera za elimu zinazounganisha tamaduni kwa kutumia lugha mbili. Hata hivyo wazazi na walimu mara nyingi huona kwamba lugha-mama hazitoi fursa ya kutosha kwa ajili ya mendeleo ya kielimu na ajira.

Matumizi ya teknolojia kusaidia ujifunzaji.

TEHAMA ina umuhimu katika kusaidia kufundisha na kujifunza, lakini tafiti zake zi zimekuwa tata Mintarafu mfiko wa matumizi hayo. Njia inayofaa kuunganisha matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya elimu bado ni changamani. Nchi nyingi zimeshindwa kuwezesha kusambaa kwa matumizi ya kompyuta kujifunzia, kwa sababu tu shule hizo hazina umeme au mtandao wa intaneti. Pia ufanisi wa TEHAMA unahitaji walimu waliopata mafunzo. Simu zimekuwa muhimu sana kwenye mifumo ya kufundishia na kujifunza inayotumia TEHAMA, kwa sababu hazihitaji miundombinu kama ile ya kompyuta, mitandao yake inapatikana sehemu kubwa na nyingi zina mtandao wa intaneti na zina uwezo wa kucheza video.

Ugatuaji wa madaraka katika utawala wa elimu

Kuhamishia mamlaka ya kufanya maamuzi shuleni huwaongezea majukumu wakuu wa shule, walimu, na wazazi. ugatuji wa mamlaka kwenye elimu unakusudia kuongeza ubora na kuimarisha uwajibikaji baina ya shule na jamii. Kiuhalisia, utekelezaji wa mbinu ya ugatuji wa madaraka umekuwa haufanani. Matokeo yanategemea mambo kadhaa ya ndani kwenye eneo husika kama vile

mgawanyo wa fedha, rasilimali watu, uongozi imara wa shule, ushiriki wa wazazi na msaada kutoka kwa maofisa wa serikali.

Kuhusika kwa huduma za sekta binafsi katika kuboresha elimu.



















Shule za binafsi zimeongezeka sana tangu mwaka 2000. Wanafunzi wa shule za binafsi mara nyingi hufaulu zaidi ya wale wa shule za umma, pengine ni kwa sababu wanafunzi kutoka familia tajiri ndio wanaosoma shule za binafsi. Wanafunzi matajiri zaidi na wale wenye uwezo mkubwa na wanaosoma shule zenye mitandao bora ndio hunufaika zaidi, wakati shule za umma zikiendelea kuhudumia jamii kubwa ya maskini. Ni kama hakuna ushahidi kwamba shule za binafsi zinatoa mbinu bora za kuboresha elimu. Kimsingi, shule za umma ndizo zenye nafasi zaidi ya kuwa wabunifu kwenye mitaala, wakati shule za binafsi lazima zizingatie matakwa ya wazazi ili kupata matokeo mazuri ya mitihani.

Karibu hakuna ushahidi kuonyesha kwamba shule za binafsi zinaongeza ubora wa elimu

KADI YA RIPOTI 2000–2015

FEDHA

Hamasisha uwajibikaji thabiti wa kisiasa wa kitaifa na kimataifa kwenye mpango wa elimu kwa wote endeleva mipangokazi ya taifa na ongeza uwekezaji kwenye sekta ya elimu

<p><i>Alama za kimataifa*</i></p> <p>*kati ya nchi zenye takwimu</p>	 <p>Mwaka 1999, kati ya nchi 116 zenye takwimu</p> <p>18 zilitumia 6% au zaidi ya Pato Ghafi la Taifa kwenye elimu</p>	 <p>Mwaka 2012, kati ya nchi 142 zenye takwimu</p> <p>39 zilitumia 6% au zaidi ya Pato Ghafi la Taifa kwenye elimu</p>	
<p><i>Mafanikio</i></p> 	<p>Serikali nyingi, hasa maskini zaidi ziliongeza matumizi kwenye elimu</p> <p>(k.m. Brazil, Ethiopia, Nepal)</p> 	<p>Ushiriki thabiti wa vyama vya kiraia umewezesha mafanikio</p> <p>k.m. ugawaji wa vitabu bora zaidi vya kiada nchini Phillipines uliwzesha kuokoa Dola za Kimarekani 1.84 milioni</p> 	<p>Uwekaji kipaumbele kwenye matumizi ya elimu</p>  <p>64% ya nchi zimefikia lengo hili pamoja na viwango imara vya ukuaji wa uchumi</p>
<p><i>Jitihada zilizofanyika</i></p> 	<p>Uwazi na uwajibikaji Mashirika ya kiraia umesaidia kusisitiza umuhimu wake</p> 	<p>Kwenye nchi 38 matumizi yameongezeka</p> <p>↑ kwa 1%</p>  <p>au zaidi ya Pato Ghafi la Taifa (1999-2012)</p> <p>Ufadhili wa serikali na wahisani</p>	<p>Kupunguza pengo la matumizi viwango vya matumizi ya kila mwanafunzi kati ya elimu ya msingi na ile ya juu vimefikwa kwenye nchi 30</p>  <p>1999 2012</p>
<p><i>Changamoto zilizopo bado</i></p> 	<p>Gharama za vifaa vya kufundishia</p> <p>Kwenye nchi 12 za Afrika, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilitumia 56% ya bajeti ya ndani ya taifa</p> 	<p>Ufadhili wa serikali na wahisani</p>  <p>Ukiondoa elimu ya msingi, kiasi kikubwa hutumiwa kwenye maeneo mengine ya elimu yasiyohusiana na ELIMU KWA WOTE</p> 	<p>Misaada ya kibinadamu</p> <p>Mwaka 2013, kati ya fedha zote zilizokuweko kwa ajili ya misada ya kibinadamu, ni 2% tu ilitumika kwenye elimu</p> 
<p><i>Mafanikio yanavyotofautiana</i></p>	<p>Ugawaji wa rasilimali unahitaji kuwa na ufanisi na usawa zaidi</p> 	<p>Utoaji wa misaada wenye ufanisi zaidi</p> 	<p>Usaidizi wa kifedha usiofuata mifumo iliyopo</p> <p>katika kufadhili maeneo ya elimu yenye uhitaji wa rasilimali (k.m. uwekezaji binafsi, ufadhili wa mashirika, n.k.)</p> 
<p>Mapendekezo kwa ajili ya kipindi kufuatia mwaka 2015</p>	<ol style="list-style-type: none"> 1. Maeneo ya elimu yaliyopuuzwa, kama vile elimu ya awali, elimu kwa waliokuwa wameikosa awali na watu wazima kujua kusoma na kuandika, yanapaswa kupewa kipaumbele na serikali na wafadhili 2. Zinahitajika zana bora zaidi za uchunguzi ili kuelewa namna matumizi yanavyofanyika <p><i>Uwajibikaji zaidi unahitajika</i></p>		

SURA YA 8 Fedha

Hamasisha dhamira madhubuti ya kisiasa ya kitaifa na kimataifa kwa ajili ya mpango wa elimu kwa wote, tengeneza mipango-kazi ya kitaifa na ongeza ipasavyo uwekezaji kwenye elimu ya msingi.

Mwongozo wa Dakar wa utekelezaji ulitoa wito kwa serikali na wafadhili kuongeza fedha ili kuharakisha mendeleo kuelekea malengo ya Elimu kwa Wote. Ulihamasisha wafadhili kusaidia jitihada za serikali kuongeza ufadhili wa elimu ya msingi na kutekeleza kwa ufanisi kadiri iwezekanavyo. Pia mpango huo ulitoa wito kwa nchi kuwajibika zaidi kwa wananchi.

Ahadi iliyotolewa huko Dakar kwamba hakuna nchi itakayokwamishwa kufikia malengo ya ELIMU KWA WOTE kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali ni moja ya mambo makubwa yaliyoshindikana kwa kipindi chote cha mpango wa ELIMU KWA WOTE. Wafadhili walishindwa kutimiza ahadi zao. Jitihada za serikali maskini kuongeza bajeti za elimu kwenye elimu ya msingi ni za kupongezwa, lakini kwa ujumla, bado kuna mengi ya kufanya ili kufanikiwa kuyapa kipaumbele matumizi ya elimu. Msaada wa kifedha kutoka serikalini na wafadhili kwa ajili ya malengo mengine ya ELIMU KWA WOTE ni kidogo mno na maendeleo yake yamekuwa dhaifu.

Mabadiliko katika ahadi za taifa za kifedha kwa ajili ya ELIMU KWA WOTE tangu Dakar

Mwongozo wa Dakar ulizichukulia serikali za kitaifa kama ndio wafadhili wa ELIMU KWA WOTE. Tarajio hilo limejitokeza hata kwenye kanda tegemezi za misaada: matumizi ya ndani ya umma hudumaza misaada kutoka nje.

Mwaka 2006, Baraza la Juu la ELIMU KWA WOTE lilipendekeza kwamba serikali zitumie 4% hadi 5% ya mapato ya taifa kwenye bajeti ya elimu. Na kwamba ndani ya bajeti ya serikali asilimia 15 na 20 zitengwe kwa ajili ya elimu.

Mwenendo wa kutoa kipaumbele kwa elimu umechanganywa. Kwa dunia, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya elimu ni 5% ya mapato ya serikali kwa mwaka 2012. Kwa nchi za kipato cha chini wastani ulikuwa chini ya 4%. Katika ya nchi 142 zilizokuwa na takwimu, 96 zilitumia 4% ya mapato au zaidi kwenye elimu

(ikijumuisha nchi 14 za kipato cha chini na 18 za kipato cha kati), na kati ya hizo nchi 96, 39 zilitumia 6% au zaidi kwenye elimu.

Matumizi ya elimu si mara zote yaliendana na ukuaji wa kiuchumi na ongezeko la uandikishwaji

Ukuaji wa uchumi kwa mwaka 1999 hadi 2012 uliambatana na ongezeko halisi la matumizi kwenye elimu. Wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao ni asilimia 4 ulizidiwa na ongezeko la matumizi kwenye elimu ambayo ni wastani wa 6% kwa mwaka. Tofauti na huko Asia ya Kusini na Magharibi, wastani wa ukuaji wa kiuchumi kwa mwaka 1999 na 2012 ulikuwa 4.5%, huku matumizi ya serikali kwenye elimu yakiongezeka juu kidogo ya 4.9% kwa mwaka.

Elimu haipewe kipaumbele kwenye bajeti nyingi za kitaifa.

Katika mgao wa matumizi ya serikali, matumizi kwenye elimu yamebadilika kidogo tangu mwaka 1999. Mwaka 2012 wastani wa dunia ulikuwa 13.7% ikipungua kutoka kwenye lengo la 15% hadi 20%. Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ndizo zilizotenga kiasi kikubwa cha mgao wa matumizi kwenye elimu (18.4%), ikifuatiwa na Asia ya Mashariki na Pasifiki (17.5%). Asia ya Kusini na Magharibi ilitenga 12.6%

Mgao mdogo wa bajeti ya elimu huelekezwa kwenye elimu ya awali.

Kama mgao wa jumla wa matumizi ya serikali kwenye elimu, matumizi ya dunia kwenye elimu ya awali yalikuwa 4.9% mwaka 2012. Amerika ya Kaskazini na Ulaya Magharibi zilitenga 8.8% ya bajeti ya elimu kwenye elimu ya awali wakati nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilitumia 0.3%

Mwaka 2012, kiasi kilichotolewa kwa ajili ya elimu kama sehemu ya Pato Ghafi la Taifa kilikuwa ni 5%.

Kuna tofauti kubwa kwenye ufadhili wa elimu ya msingi.

Malengo ya ELIMU KWA WOTE na yale ya maendeleo ya milenia yalisisitiza uhitaji wa kutoa elimu ya msingi bure na yenye ubora, yakihitaji uwekezaji mkubwa na utoaji kipaumbele kwenye bajeti ya elimu ya msingi. Mbali na hili, kati ya nchi 56 zenye takwimu za mgao wa matumizi kwenye elimu ya msingi mwaka 1999 na 2012, ni nchi 12 tu ndizo ziliongeza mgao.

Katika nchi nyingi maskini, mishahara ya walimu inachukua mgao mkubwa zaidi wa bajeti ya shule za msingi.

Wastani wa mishahara ya walimu ulikuwa 82% ya jumla ya pesa iliyotengwa kwa ajili ya elimu ya msingi kwa nchi za kipato cha chini na kati. Nchi za kipato kikubwa zilitenga asilimia 64%. Kwenye nchi nyingi, hii hubakiza rasilimali chache sana kwa ajili ya maeneo mengine, kama vile kufikia malengo ya ubora na ufanisi. Utafiti wa Benki ya Dunia wa mwaka 2003 na mpango wa ELIMU KWA WOTE vilisisitiza matumizi ya moja ya tatu ya fedha ya elimu kwenye matumizi nje ya mishahara. Kwa mwaka 2012, nchi 36 za kipato cha chini na cha kati, zilizokuwa na takwimu, mgao uliotumika kwa ajili ya kununua vitabu vya kiada na vifaa vingine vya kujifunzia ulikuwa 2%; nchi 16 zilitumia chini ya 1%. Ni Kuwait na Malawi pekee ndizo zilizotumia 5% au zaidi.

Nchi nyingi ziliongeza matumizi ya fedha kwenye elimu ya sekondari

Idadi kubwa ya wanafunzi wanaoingia shule za sekondari humanisha rasilimali za ziada. Miongoni mwa nchi 61 zilizokuwa na takwimu juu ya matumizi ya fedha za umma kwenye elimu kulingana na pato la taifa, kwa mwaka 1999 na 2012, matumizi ya fedha kwa ajili ya elimu ya sekondari yaliongezeka. Kati ya hizo, nchi 156 zilikuwa za kipato cha chini na cha kati.

Rushwa bado ni janga

Rushwa serikalini imeonekana kuleta matokeo hasi katika kuleta usawa kwenye huduma za kijamii ikiwemo elimu. Mwongozo wa Dakar ulibainisha, 'rushwa ni kikwazo kikuu cha matumizi sahihi ya rasilimali kwa ajili ya elimu na inapaswa kushughulikiwa mapema. Mashirika ya kijamii duniani yamekuwa msaada sana kwenye mapambano dhidi vitendo vya rushwa. Pamoja na jitihada hizo kwa mwongo mmoja uliopita, rushwa kwenye elimu imeendelea kuwepo, na gharama yake kwa sehemu kubwa imekuwa ikilipwa na maskini ambao siku zote hawana uwezo wa kuchagua kwenda kupata huduma kutoka sekta binafsi.

Usawa na ujumuishi kwenye matumizi ya elimu

Haitoshi kuelekeza tu, rasilimali zaidi kwenye elimu; rasilimali hizo ni lazima zitumike kwa usawa. Hili inahusisha matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya makundi mengine tofauti na utekezaji wa malengo ya ELIMU KWA WOTE, kama vile watu maskini zaidi, walemavu na wale wanaoishi kwenye maeneo yaliyotengwa na wale wanaotoka kwenye makundi madogo. Hata hivyo, nchi nyingi huendelea kugawa fedha kwa viwango sawa kwa kila mtoto, na hivyo kushindwa kuzingatia tofauti zilizopo kwenyeshule na kanda, na mahitaji ya kundi lenye hali ngumu.

Kwa nchi nyingi za kipato cha chini, urazini wa kutumia fedha zaidi kwenye elimu ya msingi ni mkubwa, kiwango ambacho kwa sehemu kubwa kinaweza kufikiwa na familia maskini. Lakini kwa wastani mwaka 2012, nchi za kipato cha chini, matumizi kwa mwanafunzi wa elimu ya juu yalikuwa mara 11 zaidi ya mwanafunzi wa shule ya msingi. Katika nchi ambazo zinategemewa kuwasaidia maskini kwa kutumia fedha za umma, faida ya elimu, inaendelea kuwa kwa ajili ya watoto wa matajiri.

Kaya huchangia jitihada za taifa za elimu, hususan pale serikali zinapobana matumizi.

Tatizo katika nchi nyingi sio uhaba wa fedha za nchi kwa ajili ya elimu bali ni mzigo mkubwa wa gharama zinazobebwa na kaya. Kwa ujumla, kwa kadiri nchi inavyokuwa maskini zaidi ndivyo kaya zinavyobeba mzigo mkubwa zaidi. Miongoni mwa nchi 50 za kipato cha chini, kati na juu, zilizokuwa na takwimu katika kipindi cha mwaka 2005-2012, matumizi ya kaya kwenye elimu yalikuwa ni 31% ya kipato chote. Miongoni mwa nchi 25 zilizotenga fedha kidogo kwa ajili ya elimu, familia zilichangia 42% ya matumizi yote, wakati miongoni mwa nchi 25 zenye kipato kikubwa, familia zilichangia 27%.

Misaada ya kimataifa ya maendeleo

Baada ya mwaka 2000 kulikuwa na matarajio makubwa kwamba wafadhili wangeongeza msaada wa kifedha kwenye elimu, kulingana na malengo yaliyowekwa kwenye malengo 6 ya ELIMU KWA WOTE. Wakati msaada wa elimu ukiongezeka kwa 6% kwa mwaka, kwa wastani, msaada wa kifedha kwenye elimu haukubadilika, haukuzidi 10%. Kinyume chake, msaada wa kifedha kwa ajili ya afya uliongezeka kutoka 9% hadi 14%.

Kwa ujumla, msaada kwenye elimu uliongezeka kwa kasi hadi mwaka 2010, lakini ukashuka kwa 10% (jumla ya dola za Kimarekani 1.3 bilioni) kati ya mwaka 2010 na 2012.

Mwaka 2012, nchi za kipato cha chini zilitumia mara 11 zaidi kwa kila mwanafunzi wa elimu ya juu kuliko kwa mwanafunzi wa elimu ya msingi.

Utoaji wa misaada kulingana na kiwango cha elimu.

Misaada kwenye elimu ya msingi, ambayo huhusisha moja ya malengo 6 ya ELIMU KWA WOTE, uliongezeka zaidi mwaka 2009 na 2010. Kisha kati ya mwaka 2010 na 2012 utoaji wa misaada ulishuka kwa 15%, au Dola za Kimarekani 921 milioni. Katika hali tofauti, misaada ya elimu ya juu (baada ya kumaliza elimu ya sekondari) ilishuka kwa asilimia 6. Kwa kiwango kamili, kwa mwaka 2012, misaada kwenye elimu ya juu ulikuwa mkubwa kuliko ule wa msingi.

Msaada wa kifedha kutoka nje ulilenga zaidi kwenye elimu ya msingi, ukipuuza malengo ya ziada ya ELIMU KWA WOTE. Kama mgao wa misaada yote kwenye elimu ya msingi, misaada kwa ajili ya stadi za maisha kwa vijana na watu wazima na kwa elimu ya awali ulishuka. Mikakati ya wafadhili ililenga kidogo sana kwenye elimu ya watu wazima, elimu ya masafa, elimu isiyo rasmi, na elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.

Utoaji msaada kikanda

Utoaji wa misaada kwenye elimu ya msingi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, sehemu ambayo ina zaidi ya nusu ya watoto ambao hawajaenda shule, uliongezeka kwa kasi kuanzia mwaka 2002 na

ukapungua kuanzia mwaka 2009. Kwa wastani, kutoka mwaka 2002 hadi 2004, 47% ya misaada wote uliotolewa kwa ajili elimu ya msingi ulielekezwa kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, lakini kufikia mwaka 2010-2012, kiwango hicho kilishuka kwa 31%. Huko Asia ya Kusini na Magharibi, mgao wa elimu ya msingi haukubadilika sana, ukiongezeka kutoka 21% hadi 22%.

Utoaji wa misaada kwa maskini

Wakati 93% ya watu maskini zaidi mwanzoni mwa miaka ya 1990 waliishi katika nchi zenye kipato cha chini, kwa mwaka 2012, 72% waliishi katika nchi zenye kipato cha kati. Kwa sasa 59% ya watoto ambao hawajaenda shule wapo kwenye nchi za kipato cha kati. Hata hivyo, nchi hizo kwa sehemu kubwa zinahitaji pesa kwa ajili ya huduma muhimu-nchi za kipato cha chini na mataifa tete- hupaswa kupewa kipaumbele. Hata hivyo, mgao kwa ajili ya elimu ya msingi utapungua kwa nchi za kipato cha chini kutoka 40% hadi kufikia 34% kwa zaidi ya mwongo mmoja.


Mabadiliko ya utoaji msaada tangu mwaka 2000

Kuna wakati misaada ilitoka kwenye akiba ya wafadhi wa OECD, lakini tangu mwaka 2000, uchumi unaokua umerasimisha njia mbadala za dunia za

Msaada kwenye elimu ya msingi ulidorora mwaka 2010

Kielelezo 10: Ufadhili kwenye malengo ya ELIMU KWA WOTE nje ya elimu ya msingi haujaongezeka

Jumla ya ahadi za ufadhili wa elimu, wastani wa miaka mitatu, 1995-2012



Maelezo: Takwimu za kabla ya 2002 ni za ahadi za msaada, kwani takwimu za matumizi hazikuwepo. Kutokana na kubadilikabidilika kwa ahadi za misaada, grafu inaziwasilisha kama wasitani wa miaka mitatu

Chanzo: OECD-DAC (2014).

kuendeleza ushirikiano, kama vile kituo cha IBSA cha kupunguza umaskini na njaa, kilichoundwa mwaka 2004 kwa nchi za India, Brazil, Afrika Kusini; pia Benki Mpya ya Maendeleo (New Development Bank) iliyoanzishwa nchi za Brazil, China, India, Russia na Afrika Kusini.

Wafadhili hawajatimiza ahadi yao ya kufadhili elimu kwa ufanisi zaidi

Tangu Dakar, kumekuwa na dhamira thabiti ya kisiasa kwa ajili ya kuboresha sio tu idadi bali pia usimamizi wa misaada ya kimataifa. Azimio la Paris kuhusu Matumizi Sahihi ya Misaada mwaka 2005 lilichukuliwa kama ahadi isiyokuwa ya kawaida katika kuboresha utoaji wa misaada. Lakini miongoni mwa malengo 13 ya ufanisi

kwenye misaada, ni lile linalohusua kuandaa na kuratibu misaada ya kiufundi ndilo lilifikiwa hadi mwaka 2010.

Kukosekana kwataratibu za kimataifa za misaada hukwamisha uratibu wa kufaa wa ufadhili.

Uratibu wa dunia ungeweza kuwaruhusu wafadhili wa elimu kupeleka misaada mahali ambapo panahitajika zaidi. Lakini mifumo iliyopo ya uratibu wa dunia na kitaifa haijasaida ipasavyo. Mkutano wa nne wa Baraza la Juu la ELIMU KWA WOTE uliofanyika Busan, Jamhuri ya Korea, mwaka 2011, ulitilia mkazo kutumia taasisi za kimataifa na mifuko ya kimataifa kuongeza ushirikiano, hata hivyo misaada mingi ya kimataifa kwa ajili ya elimu ya msingi inaendela kuzingatia eneo na sekta.



Credit: Ami Vitale/Panos Pictures

Ubia wa Dunia umekuwa bora zaidi katika kuzilenga nchi zenye uhitaji.

Ubia wa Dunia kwa ajili ya Elimu (The Global Partnership for Education -GPE)- awali ulijulikana kama Jitihada za Haraka za ELIMU KWA WOTE (EFA Fast Track Initiative), ulioanzishwa mwaka 2002- ulifanya kazi muhimu ya kuratibu misaada ya dunia ya elimu, lakini ufadhili wa kifedha kufanikisha jambo hilo ukakosekana. Badala yake, umeelekeza nguvu zake zaidi kwenye nchi zenye uhitaji hasa. Kwa wastani, mwaka 2010 na 2012, zaidi ya 81% ya misaada yote ya GPE ilielekezwa kwa nchi za kipato cha chini, ikilinganishwa na 42% kutoka kwa wanachama wa Kamati ya Misaada ya Maendeleo ya OECD (Development Assistance Committee).

Mikakati ya misaada inahitaji kupanuliwa zaidi ya kufikia upatikanaji.

Matokeo ya misaada yanayoonekana zaidi ni kuongezeka kwa idadi ya uandikishwaji, hasa kwa shule za msingi. Matokeo ya misaada ya kigeni kwenye usawa wa jinsia yamekuwa ya kiwango cha chini zaidi. Hata hivyo, mambo yanayowafanya wasichana washindwe kujiunga na shule – kama vile umasikini, shule kuwa mbali, kutoonekana faida ya wasichana kwenda shule, imani za kitamaduni- zinapaswa ziangaziwe zaidi na watoaji wa msaada.

Wajibu wa misaada ya kibinadamu kwenye sekta ya elimu.

Pamoja na majanga ya muda mrefu kutokea mara kwa mara, sekta ya elimu kwa mwongo uliopita imejitahidi kuvutia misaada ya kibinadamu kwamba kuwekeza kwenye elimu ni kuokoa maisha. Hata hivyo, msaada wa elimu unaendelea kutelekezwa ndani ya mfumo ulioko ambao hauna rasilimali za kutosha.

Mwaka 2012, serikali, mashirika ya Umoja wa Mataifa, sekta binafsi na mashirika ya kijamii yalitoa wito wa kuongeza maradufu misaada ya kibinadamu pamoja na ya elimu angalau ifikie 4% ya fedha zote za misaada. Pamoja na hili, mwaka 2013 sekta hii ilipokea 2% tu.

Mashirika yasiyo ya kiserikali yanatumia rasilimali zake vema zaidi katika kufanikisha malengo yaliyopuuzwa ya ELIMU KWA WOTE.

Fedha zinazotolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali kwenye elimu zimeongezeka hadi kati ya Dola za Kimarekani 2.6 na 5.2 bilioni. Mashirika haya yamekuwa watoaji muhimu wa huduma za msingi kwa baadhi ya nchi, na matumizi yao kwenye elimu yanaonyesha kwamba malengo yao yanaendana na yale ya ELIMU KWA WOTE ambayo yamepuuzwa na serikali na wafadhili, kama ilivyo kwa elimu isiyo rasmi na ECCE.

Ufadhili wa kifedha usio wa kimapokeo uungekuwa muhimu zaidi

Ufadhili usio wa kimapokeo umeongezeka zaidi hadi kufikia zaidi ya Dola za Kimarekani 50 bilioni. Mwaka 2010, kampuni inayoongoza kwenye mchango-ubunifu wa kifedha kwa ajili ya maendeleo Ubunifu wa Fedha kwa ajili ya Maendeleo (Innovative Financing for Development) ilipendekeza mbinu tisa za kupanua ufadhili wa elimu; kodi ya miamala ya kifedha, dhamana za elimu kwenye fedha za ndani, mifuko ya miradi, dhamana za ughaibuni, michango ya hiari kutoka kwa wahamiaji, kubadilishana madeni, ushuru kwenye michezo, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na michango midogomidogo. Mbinu kama hizo zimezalisha zaidi ya Dola za Kimarekani 7 bilioni kwa ajili ya mfuko wa afya tangu mwaka 2002, lakini ni chache ambazo zimetumia kwenye ufadhili wa sekta ya elimu.

Mwaka 2013, sekta ya elimu ilipokea 2% tu ya misaada ya kibinadamu

Mapendekezo

1. Ongeza msisitizo juu ya malezi na elimu awali

Nchi zote zinapaswa kuwa na angalau elimu ya awali ya lazima ya mwaka mmoja kama sehemu ya mzunguko wa elimu ya msingi, na serikali zihakikishe kuwa mahitaji yote ya lazima yanakuwepo.

Pale ambapo bajeti za serikali haziwezi kupeleka huduma kwa wote, basi wanapaswa kulenga zaidi makundi ya wale wasiojiweza.

Programu zisizo rasmi za elimu ya awali za kijamii zisaidiwe pale ambapo uwezekano wa programu rasmi ni adimu.

Malezi na ufundishaji vinapaswa kuwa na ubora unaofaa na wafanyakazi wawe wamefundishwa namna ya kuchochea ufahamu wa watoto wadogo na kutoa msaada wa hisia -kijamii .

Nchi zinapaswa kujitahidi kuvutia walezi na walimu zaidi na bora kwa kuboresha hadhi na mishahara yao kwa kiwango cha walimu wa shule za msingi.

2. Fanya kila uwezalo kuwawezesha watoto wote wamalize shule ya msingi

Serikali zinahitaji kuendeleza mipango halisi ya kutuma pesa, yenye masharti nafuu na yenye kulenga miradi, ili kuziwezesha kaya maskini kumudu gharama za shule kama vile ada zisizo rasmi, sare na usafiri.

Ili kuboresha ushiriki shuleni na kupunguza idadi ya wanafunzi wanaoacha shule, serikali zinapaswa kutekeleza programu za sekta-changamani kwenye maeneo kama vile afya na lishe, pamoja na kuwekeza kwenye miundombinu ya barabara, maji na umeme.

Serikali zinapaswa kuandaa mipango ya dharura ili kukidhi mahitaji ya elimu kwa watoto kwenye matukio ya dharura na maeneo ya vita.

3. Boresha upatikanaji wa stadi za kazi na maisha miongoni mwa vijana na watu wazima

Serikali zinahitaji kuhakikisha kwamba vijana wote, hususan wale maskini zaidi, wanapata stadi za msingi kupitia upatikanaji wa elimu ya bure na ya lazima ya sekondari ngazi ya chini.

Kwa kutambua ukweli kwamba kuchanganya masomo na kazi huathiri nafasi za watoto za kupata stadi za msingi, nchi zote lazima ziridhie, kutangaza na kutekeleza Mkataba wa 138 wa Shirika la Kazi Duniani, ambao unaweka wazi umri wa chini zaidi kwa mtoto kuweza kuajiriwa.

Watunga sera ni lazima wazitambue na kuzipa kipaumbele stadi zinazopaswa kufikiwa mwishoni mwa kila hatua ya elimu rasmi.

Serikali zinapaswa kupima ni aina gani ya elimu au mafunzo – pamoja na programu za kazi na mafunzo na uanagenzi – inafaa zaidi na inawezesha usawa katika upatikanaji wa stadi.

Ili kukidhi mahitaji ya watu wazima wenye viwango duni vya elimu, serikali zinapaswa kupanua fursa kwa ajili kujiendeleza kielimu, zaidi na elimu ya watu wazima.

4. Wawezeshe watu wazima wote kutambua haki yao ya kujua kusoma na kuandika na kuhesabu

Sera na mikakati ya kisomo zinapaswa kuunganisha sera za maendeleo zilizopo na mahitaji ya jamii, afya, maendeleo ya jamii, ubunifu wa kilimo na uraia hai.

Matumizi ya simu za kiganjani na vifaa vingine vya TEHAMA kuwezesha kujua kisomo na kudumu shuleni yaungwe mkono kupitia ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

Nchi zinapaswa kuimarisha mipango ya kisomo kwa kubainisha viwango vya stadi vinavyopaswa kufikiwa na watu wazima na kupima na kufuatilia ushiriki na matokeo.

5. Badili mlengo kutoka kwenye usawa kwenda kwenye mlingano

Ili kufanya mazingira ya kujifunzia yawe na usawa zaidi, ni muhimu kulenga kwenye rasilimali ili kuhakikisha kwamba vifaa vya kufundishia na huduma za maji na usafi (kwa kuondoa maji machafu na takataka) vinaridhisha.

Serikali zinahitaji kuhakikisha kwamba programu za mafunzo tarajali na mafunzo kazini zinahusisha mbinu za kwa walimu kuzitumia kwenye ufundishaji na usimamizi wa darasa. Programu hizi lazima ziandaliwe kwa makini kwa kuzingatia kukosekana kwa usawa kulikojitokeza katika mazingira ya ndani.

Mitaala lazima iangazie hisia za kijinsia na ijumuishe mafundisho ya afya ya uzazi na ujinsia

6. Wekeza kwenye ubora wa elimu

Serikali zinapaswa kuwekeza vya kutosha katika utoaji wa elimu bora. Sera zinazoweza uanataluma (umahiri) wa mwalimu na motisha zipewe kipaumbele. Madhara yasababishwayo na kuajiri walimu wa mikataba ziangaliwe kwa uangalifu.

Walimu wasaidiwe kwa kupewa maudhui za kufaa na jumuishi za mitaala ambayo inaweza kuboresha kujifunza, na kuwawezesha wanafunzi wazito kuelewa. Watu wote wapewe rasilimali za kutosha za kujifunzia, hususani vitabu vya kiada.

Mitindo na njia za kufundishia zierendane zaidi na tofauti za kitamaduni na miktadha ya darasa. Kwenye jamii za lugha nyingi, sera za lugha kwenye elimu ni muhimu ili kupata elimu yenye ufanisi.

Mifumo ya utawala lazima ichanganye mipango madhubuti ya kitaasisi na dhamira ya usawa.

Serikali inapaswa kupitisha sera sahihi zitakazoweza walimu kupangwa kwenye maeneo yenya uhitaji.

Muda wa shule ulio bora na wa kutosha, ambao walimu na wanafunzi watautumia kikamilifu kwenye shughuli za mafunzo, ni wa muhimu sana.

Nchi lazima ziimarisha uwezo wao wa kufanya tathmini zinazoonisha vipaumbele vya kitaifa na kusaidia juhudi za kuwezesha elimu bora, ufundishaji madhubuti na matokeo sawa ya kujifunza kwenye maeneo tofauti ya masomo.

7. Peleka ufadhili wa elimu na elekeza rasilimali kwa waliopembeza zaidi

Serikali zinapaswa kuhamasisha zaidi rasilimali za ndani ili kuwa na chanzo cha fedha endelevu kwa ajili ya mpango wa elimu baada ya 2015. Nchi zenye kipato cha chini na cha kati-chini zitahitaji kutumia 3.4% ya Pato la Taifa kwenye elimu ya awali, msingi na sekondari ngazi ya chini, au 5.4% ya Pato la Taifa kwenye ngazi zote za elimu.

Rasilimali za elimu ya umma zinahitaji kuhamishiwa kwenye elimu ya awali, elimu isiyo rasmi na kisomo cha watu wazima ili kuyanufaisha makundi ya pembezoni. Wafadhili wanapaswa kuongeza misaada yao ya kifedha kwenye elimu na kuhakikisha kwamba malengo ya misaada hiyo yameainishwa vema. Uratibu wa maendeleo ya dunia na misaada ya kibinadamu lazima uhusishe nchi ambazo zinahitaji zaidi misaada hiyo.

Kufuatia pengo la Dola za Kimarekani 22 bilioni, wafadhili watahitaji kuongeza msaada kwenye elimu ya awali, msingi na sekondari ngazi ya chini katika nchi za kipato cha chini na kati kwa angalau mara nne.

Uwekezaji kwenye zana za uchunguzi ambazo zitafuatilia rasilimali zote za elimu utasaidia serikali na wafadhili kutathmini vizuri zaidi jinsi makundi ya vipato mbalimbali yanavyonufaika kutokana na matumizi rasmi na kuhakikisha kwamba watoto maskini zaidi hawaachwi nyuma.

8. Imarisha mlengo kuhusu usawa

Ili kushughulikia usawa kwanza kabisa, serikali zinahitaji kubadili namna wanavyotumia taarifa kwenye upangaji wa shughuli zao za elimu.

Serikali zinapaswa kuweka kipaumbele kwenye matumizi ya takwimu zilizogawanywa kutoka kwenye tafti za shule, kaya na soko la ajira ili kuboresha mipango yao ya elimu na kuelekeza rasilimali kule zinakohitajika zaidi.

9. Shughulikia upungufu mkubwa kwenye takwimu ili kuboresha zaidi ufuatiliaji

Ni jambo muhimu kuboresha msingi wa maarifa kuhusu mifumo ya taifa ya elimu ili kuziba mapengo makubwa ya takwimu muhimu kuanzia masuala ya ubora, hadi stadi za kisomo hadi ufadhili wa kifedha. Jambo hili linahitaji kufanyiwa kazi kwenye viwango vya pamoja, programu za kujenga uwezo na uratibu wa takwimu.

Ushirikiano wa karibu unahitajika ili kufuatilia maendeleo ya elimu kwa wakati na baina ya nchi na nchi, kulingana na njia ambazo tathmini za kitaifa za kujifunza masomo mbalimbali zinaweza kuhusishwa.

Serikali zinapaswa kutunga miongozo yao ya ufuatiliaji kwenye ukusanyaji wa takwimu kuhusu hadhi ya kielimu katika makundi mbalimbali.

Upatikanaji, kuaminika na ulinganifu wa takwimu za kisomo lazima ukuzwe ili kuboresha mipango na uandaaji wa sera.

Huku kipindi cha RIPOTI YA DUNIA YA UFUATILIAJI kinaelekea ukingoni, kuna uhitaji endelevu wa kuwa na ripoti inayojitegemea ya dunia ya ufuatiliaji wa elimu.

10. Tatua changamoto za uratibu ili kudumisha kiwango cha juu cha kuongwa mkono kisiasa kwa ajili ya elimu

Mikakati ya utekelezaji wa sera ya elimu unahitaji uwe imara kiufundi na uvutie utashi wa kisiasa. Ni lazima iwe na malengo yanayoeleweka na kuweko na ari na uwezo wa kiufundi. Ni lazima ifadhiliwe kwa pamoja na ifanyiwe tathmini ya mara kwa mara, kwa kusaidiwa na wanasiasa na kuongwa mkono na mashirika yenye ushawishi mkubwa.

Kuna haja ya kuwepo kwa mifumo iliyo wazi ya uwajibikaji ili kuziwajibisha serikali na wafadhili pale wanaposhindwa kufikia lengo au kushindwa kutimiza ahadi zao.

Elimu ndio ufunguo wa kufikia malengo mengi zaidi ya ajenda ya maendeleo ya baada ya 2015, kuanzia matumizi endelevu, afya hadi amani kwenye jamii. Programu na mbinu za elimu zinapaswa kupitiwa upya ili kufikia malengo haya.



Credit: Tuan Nguyen

ELIMU KWA WOTE 2000-2015:

MAFANIKIO NA CHANGAMOTO

Toleo la 12 la Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote – likiashiria muda wa mwisho wa 2015 kwa malengo sita yaliyowekwa na Baraza la Elimu la Dunia huko Dakar, mwaka 2000 – linatoa maelezo ya kina ya mafanikio ya dunia. Kama ambavyo jamii ya kimataifa inavyojiandaa kwa ajili ya ajenda mpya ya maendeleo na elimu, ripoti hii inatoa hesabu ya mafanikio ya nyuma na kuaksi changamoto zijazo.

Ziko dalili nyingi za maendeleo yenye kuonekana. Hatua kuelekea elimu ya msingi kwa wote imeimarika, ukosefu wa usawa wa kijinsia umepunguzwa kwenye nchi nyingi na serikali zinaongeza msisitizo wao katika kuhakikisha kwamba watoto wanapata elimu bora. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizi, dunia ilishindwa kutimiza ahadi yake ya ELIMU KWA WOTE. Mamilioni ya watoto na kundi-rika la balehe hawajapata fursa ya kuweko shuleni. Watoto na kundi-rika hilo ni wa jamii maskini na zisizojiweza zaidi. Hawa ndio wanaochangia kwa kiasi kikubwa ile hali ya kushindikana kufikia malengo ya ELIMU KWA WOTE.

ELIMU KWA WOTE 2000-2015: Mafanikio na changamoto hutoa tathmini ya kina ya maendeleo ya nchi kuelekea malengo ya ELIMU KWA WOTE na huonyesha kazi iliyosalia. Inaonyesha sera zinazofaa na kutoa mapendekezo kwa ajili ya ufuatiliaji na kutathmini malengo ya elimu baada ya mwaka 2015. Pia inawapa watunga sera chanzo chenye mamlaka ya kutumia katika kutetea elimu iwe ndio msingi wa mfumo wa maendeleo ya dunia ya baada ya mwaka 2015.

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote ni chapisho lililohaririwa kwa uhuru kama zana muhimu ya msingi lenye shuhuda na ambalo hutoa mchango wa pekee kwa serikali, watafiti, vyombo vya habari, wanafunzi na wabobezi wa elimu na maendeleo. Ripoti hii imetathmini maendeleo ya elimu kwenye baadhi ya nchi 200 na mabara karibu kila mwaka tangu 2012. Kazi hii itaendelea kwa kipindi chote cha utekelezaji wa ajenda ya maendeleo endelevu ya baada ya mwaka 2015, kama Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu.

Mojawapo ya mabadiliko makubwa tangu mwaka 2000 ni sera inayoagiza kila mtoto aende shule. Hii imesaidia kila mtu kufaidi matunda ya elimu. Sera hii inaweza kuwa imewanyang'anya wakulima nguvu-kazi yao, lakini imewapa mbegu kwa ajili ya maisha bora ya badaye.

– Sonam, mwalimu huko Bhutan.

Wazazi ambao hawawezi kuandika barua, hutumia simu za kiganjani au 'ATM' (za benki) kufanya kila wanachoweza katika kuwapatia elimu watoto wao ili wasije kamwe wakatengwa kwa sababu ya kutojua kisomo, yaani kusoma, kuandika na kuhesabu.

– Omovigho Rani Ebireri, Chuo Kikuu cha Maiduguri, Nigeria

Niliacha kwa sababu ya yale yaliyokuwa yakifanywa na waasi. Waliharibu shule zetu, hatukuweza tena kuendelea kwenda shuleni. Hawakupendezwa na jinsi ambavyo baadhi ya wasichana walivyokuwa wakivaa. Walituzomea kwa kelele, wakisema kwamba tulikuwa tunavaa vibaya. Walivunjavunja madawati ya shule, waliharibu vitabu na vitu vyetu. Shule inapaswa kuwa ni mahali pa kujifunzia mambo.

– Sita, mwanafunzi nchini Nigeria.

Kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 5 anapaswa kuhudhuria shule ya awali. Elimu ya awali ipewe kipaumbele.

– Martha Isabel Castano, Mwalimu wa shule ya msingi, Colombia



United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

UNESCO
Publishing



www.unesco.org/publishing

www.efareport.unesco.org